# TAMADUNI ZA IMANI ZA ULIMWENGU

shepherds
GLOBAL CLASSROOM

Shepherds Global Classroom ipo kwa ajili ya kuujenga mwili wa Kristo kwa kutoa mtaala kwa ajili ya kuwaendeleza viongozi wa Kikristo duniani kote. Tunalenga kuongeza programu za mafunzo ya asili kwa kuweka chombo cha mtaala wa kozi 20 mikononi mwa viongozi wa kiroho wanaotoa mafunzo katika kila nchi duniani.

Kitabu hiki kinapatikana bure kwa njia ya kupakua kutoka katika https://www.shepherdsglobal.org/courses

Mwandishi Mkuu: Dr. Stephen K. Gibson

Hakimiliki © 2023 Shepherds Global Classroom
Ilitafsiriwa kutoka Toleo la Tatu la Kiingereza.

Haki zote zimehifadhiwa.

Nyenzo za wahusika wengine zilizotumika ni hakimiliki ya wamiliki husika ambazo zimeshirikishwa na kutumika humu chini ya leseni mbalimbali.

Tafsiri ya Maandiko “yaliyonukuliwa” kutoka chapisho la Kiingereza kwa ajili ya chapisho hili la Kiswahili yanatoka katika Biblia Takatifu ya Kiswahili, “Swahili Union Version Bible” (SUVB®).” Yametumika kwa kibali. Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa kuhusu vibali:**

Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa na kutawanywa bure kikiwa kimechapishwa na katika mifumo ya kidigitali chini ya miongozo ifuatayo: (1) Maudhui yaliyoko kwenye kitabu hiki hayawezi kubadilishwa kwa namna yeyote ile; (2) Nakala zinazopatikana haziwezi kuuzwa kwa ajili ya kupata faida; (3) Taasisi za elimu zina uhuru wa kutumia na kukinakili kitabu hiki, hata kama wanalipisha ada za masomo ya ziada; na (4) Kitabu hiki hakiwezi kufanyiwa tafsiri pasipokuwepo na kibali na usimamizi wa Shepherds Global Classroom.

# Yaliyomo


Muhtasari wa Kozi ........ 5

(1) Misingi ya Ukristo ........ 9

(2) Kuelewa Migogoro ya Kidini ........ 13

(3) Umomoni ........ 23

(4) Mashahidi wa Yehova ........ 33

(5) Iglesia ni Cristo (Inglesia ni Kristo) ........ 39

(6) Eastern Lightning (Mwangaza wa Mashariki) ........ 45

(7) Imani Potofu za Kiapokaliptiki (Nyakati za Mwisho) ........ 51

(8) Uhindu ........ 57

(9) Ubudha ........ 63

(10) Utao ........ 71

(11) Uislamu ........ 77

(12) Uyudaizimu ........ 83

(13) Dini ya New Age ........ 89

(14) Dini za Asili ........ 95

(15) Voodoo ........ 99

(16) Kuelewa Usabato ........ 105

(17) Kuelewa Romani Ukatoliki ........ 113

(18) Kuelewa Uorthodox wa Mashariki ........ 119

(19) Kuelewa Theolojia ya Mafanikio ........ 125

Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho ........ 135

Maswali ya Rejea ........ 143

Vyanzo Vinavyopendekezwa ........ 147

Rekodi ya Mazoezi ........ 151

# Muhtasari wa Kozi

| Imani Potofu Ambazo Zinajifananisha na Ukristo | Dini Zisizo za Kikristo | Tamaduni Tofauti za Kikristo |
| --- | --- | --- |
| Umomoni | Uhindu | Usabato |
| Mashahidi wa Yehova | Ubudha | Uromani Katoliki |
| Iglesia ni Cristo (Inglesia ni Kristo/Kanisa la Kristo) | Utao | Uorthodoxy wa Mashariki |
| Eastern Lightning (Mwangaza wa Mashariki) | Uislamu | Theolojia ya Mafanikio |
| Imani potofu ya Kiapokaliptiki | Uyudaizimu | |
| | Dini ya New Age | |
| | Dini za Asili | |
| | Voodoo | |

**Mchanganuo wa Kozi**

Kozi hii inaelezea Imani za msingi na historia ya Imani potofu na tamaduni za dini 17 zilizochaguliwa, ikizilinganisha na Ukristo wa kihistoria wa Kiprotestanti na kutathmini mafundisho yao na matendo yao kupitia Biblia. Mwanafunzi ataandaliwa ili kujibu upotovu wa dini zisizo sahihi na kumlinda Mkristo kutokana na uongo au upotofu.

**Malengo ya Kozi**

1. Kumsaidia Mkristo kuelewa mafundisho ya msingi ya baadhi ya Imani potofu zenye ushawishi na tamaduni za kidini.
2. Kumsaidia Mkristo kuelewa kwa nini baadhi ya mafundisho ni hatari.
3. Kuwaandaa wachungaji ili kulinda makundi yao kutokana na ushawishi wa Imani potofu

4. Kuwafundisha Wakristo kutumia majibu ya kibiblia ili kujibu makosa ya kidini
5. Kutoa mwongozo wa kivitendo kwa ajili ya kuwahubiria washirika wa tamaduni za dini nyingine

**Maelezo na Mwongozo kwa ajili ya Kiongozi wa Darasa**

Wakati ambapo Maandiko yameandikwa katika mabano au ndani ya andiko kuu, darasa linatakiwa kusoma maandiko hayo kabla ya kuendelea.

Masomo kuhusiana na makundi ya kidini (Somo la 3 – 19) kwa ujumla yanafuata mpangilio ulioelezewa katika mwongozo ufuatao. Masomo mawili ya kwanza ni juu ya mada maalumu.

Mwongozo huu unaelezea namna ambavyo darasa linaweza kufundishwa kwa kiwango cha juu kabisa cha ubora. Kiongozi wa darasa ni lazima atunze kiwango hiki kwa ajili ya wanafunzi ambao wanatamani kupata cheti kutoka Shepherds Global Classroom. Kwa makundi mengine ambayo hayataweza kufikia mahitaji haya, mwalimu anaweza kuweka mahitaji ambayo yako ndani ya uwezo wao, na kuwapatia vyeti tofauti.

Tunatarajia kwamba kila somo linachukua masaa mawili ili kulimaliza kikamilifu. Endapo kundi linakutana kwa kipindi kifupi, somo linaweza kugawanywa katika mikutano miwili.

**Mpangilio wa Shughuli za Kundi**

**(1) Ripoti ya Mjadala kuhusu Injili** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 20, endapo kuna ripoti kadhaa)

Wanafunzi ambao wamemaliza zoezi la mazungumzo kutoka somo la nyuma wanatakiwa kutoa taarifa. Wanachopaswa kufanya tu ni kuelezea Habari ya mazungumzo yao. Wanafunzi wengine wanaweza kutoa maoni yao kwa ajili ya matumizi ya mbeleni. Usiwaruhusu wanafunzi kumkosoa kupita kiasi mwanafunzi anayetoa taarifa.

**(2) Muda wa Marudio Drasani** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 5-10)

Kiongozi wa darasa anatakiwa kuuliza maswali ya rejea kwa ajili ya somo lililopita, kisha maswali machache ya rejea kutoka katika masomo ambayo yameshasomwa tayari. Kusudi la hii ni kumsaidia mwanafunzi kuwa na kumbukumbu ya muda mrefu na kurekebisha kutoelewa kwa namna yeyote ambako wanaweza kuwa nako. Maswali ya rejea yanawasaidia kukumbuka taarifa za muhimu zaidi. Mwezeshaji anaweza kulifanya somo kuwa lenye ufanisi kwa kutumia maswali ya rejea. Maswali ya rejea yanapatikana mwishoni mwa kozi hii.

**(3) Kukutana kwa Mara ya Kwanza**

Mtu mmoja asome kifungu cha maneno chenye kichwa "Kukutana kwa Mara ya Kwanza." Hili linatakiwa lifanyike pasipo kuchangia lolote wala majadiliano. Habari mara nyingi hazina hitimisho ili kutengeneza hamu ya kutaka kujua zaidi kuhusiana na kundi linalosomwa.

Katika hali chache, ushuhuda mwishoni mwa somo ni kuhusiana na mtu yule yule ambaye ametajwa katika Kukutana kwa Mara ya Kwanza.

**(4) Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 15)

Someni kifungu kilichoelekezwa kwa Pamoja kwa sauti. Wanafunzi kadhaa wanaweza kupokezana kusoma mistari. Kisha muwe na dakika chache za ukimya kwa ajili ya wanafunzi kuandika kifungu cha maneno cha ufupisho na kuorodhesha maelezo (maelekezo mahususi yanapatikana katika kila somo). Baada ya kuandika, waache wanafunzi kadhaa wasome kile walichokiandika ili kwamba kila mmoja ajifunze kutoka kwa mwingine.

**(5) Kujifunza Kundi la Dini** ((Muda Unaokadiriwa: Dakika 40)

Jifunze taarifa zilizotolewa kuhusiana na kundi la dini. Kiongozi au mtu mwingine katika kundi anaweza kusoma na kuelezea nyenzo kwa kundi. Wanafunzi tofauti wanaweza kusoma na kuelezea nukuu katika mstari wa pambizo.

**Maswali ya Majadiliano** na **mazoezi ya ndani ya darasa** yameoneshwa kwa alama ►. Kiongozi wa darasa anatakiwa kuuliza swali na kuwapa wanafunzi muda wa kujibu. Kadhaa yatakuwepo katika kila somo.

Maandishi ***Yaliyokolezwa na yenye mwandiko uliolala*** yanapinga au yanakanusha mafundisho na desturi zisizo sahihi za kundi la kidini. Baada ya kusoma ukweli kuhusiana na kundi la dini, rudi nyuma na kusoma tena maelezo na andiko lililotolewa.

**(6) Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 20)

*Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* ni sehemu ya nyenzo katika kozi hii ambayo imeandikwa baada ya masomo. Kwa wakati huu katika somo, tazama mada katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* zilizoorodheshwa chini ya sehemu hii. Wanafunzi wasome maandiko pamoja na kuhakikisha wameelewa namna ambavyo mistari inathibitisha dondoo. Kila mwanafunzi anapaswa aoneshe kwamba anaweza kuthibitisha dondoo kutoka katika maandiko. Baadhi ya dondoo zinatumika katika masomo kadhaa. Sio lazima kurudia kitendo kile kile katika dondoo ile ile endapo mwanafunzi anajifunza vizuri.

**(7) Uinjilisti** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 10)

Sehemu hii inatoa baadhi ya mambo ya kivitendo ya kukumbuka wakati tunaongea kuhusiana na kundi mahususi la dini. Katika baadhi ya masomo sehemu hii imeunganishwa pamoja na sehemu "Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*"

**(8) Ushuhuda**

Mtu mmoja asome sehemu ya nyenzo yenye kichwa "Ushuhuda." Shuhuda ni matukio halisi, ingawaje wakati mwingine majina yamebadilishwa.

**(9) Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2** (Muda Unaokadiriwa: Dakika 20)

Mwishoni mwa kipindi cha kujifunza, soma tena kifungu cha Andiko kilichotolewa. Subiri kwa dakika chache ili kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe ambao kifungu kinatoa kwa ajili ya mshirika wa kundi la dini linalofundishwa. Waruhusu wanafunzi wachache washirikishe kile walichokiandika.

**(10) Zoezi**

Kila wakati hitimisha muda wa somo kwa kuwakumbusha wanafunzi kutengeneza ratiba ya fursa ya kuwasilisha injili. Wanafunzi wanatakiwa kuwa na mazungumzo na washirika wa dini ambazo zinasomwa, kama inawezekana. Wanatakiwa kujaribu kuwasilisha injili na kweli nyingine za kikristo. Kama haiwezekani kwa wao kuwapata washirika wa kundi la dini mahususi, wanapaswa kumtafuta mtu mwingine ambaye yuko tayari kusikiliza maudhui au mada ya injili. Wanapaswa kuelezea imni ya msingi ya dini, kisha watoe mwitikio wa kibiblia. Wanatakiwa kujiandaa ili kuliamdia darasa kuhusiana na mazungumzo yao.

Kila mwanafunzi anatakiwa kutoa taarifa ya mazungumzo kuhusiana na dini 10 wakati wote wa kozi hii. Ripoti ya maandishi ya kila mazungumzo inatakiwa kuelezea sifa za dini husika ambazo ni muhimu kwa mwinjilisti kuzifahamu. Katika ripoti, mwanafunzi ataelezea kile ambacho alikiwasilisha katika mazungumzo, na ni kwa namna gani mtu mwingine aliitikia. Ripoti ya kila mazungumzo inatakiwa kuwa na urefu wa kurasa mbili. Mwalimu anatakiwa kuelezea zoezi hili mara kadhaa wakati wa masomo machache ya kwanza. Ripoti nzuri zilizoandikwa na wanafunzi zinatakiwa kuoneshwa katika kundi kama mifano.

Mazungumzo 10 na mazoezi ya kuandika ni mazoezi ya msingi kwa kozi hii. Fomu itatolewa karibu na mwisho wa kitabu hiki kwa ajili ya mwalimu kutumia ili kutunza rekodi.

**(11) Vyanzo Vinavyopendekezwa**

Endapo mwanafunzi anataka kujifunza zaidi kuhusiana na kundi lolote la dini anapaswa aangalie Vyanzo Vinavyopendekezwa karibu na mwisho wa kitabu ili kuona vyanzo vinavyopatikana.

# Somo la 1
# Misingi ya Ukristo

## Utangulizi

Katika Kozi hii tunachunguza tabia za kiimani za makundi mengi ya kidini. Ni muhimu kwanza kuelezea Misingi ya Ukristo kabla ya kujadili makosa ya kiimani. Ukristo wa kweli ni nini? Mafundisho yapi ya msingi ni muhimu kwa Theolojia ya Kikristo na yenye kutusaidia sisi kutambua misingi ya makundi ya kidini?

## Historia muhimu ya Ukristo

Kuna Ukristo mmoja na kanisa moja la kweli kwa sababu kuna Mungu mmoja tu na Injili moja ya kweli. Kanisa limejengwa juu ya msingi: Ukweli uliofunuliwa kwenye (1) huduma za mitume na (2) Maisha, Huduma, Ujumbe, na upatanisho wa Yesu Kristo. Kuna msingi mmoja na kanisa moja la duniani kote.

Umoja wa kanisa la kiulimwengu haimanishi kwamba kanisa lote ni shirika moja. Hakuna shirika moja linalo timiza kusudi la Mungu kwa Kanisa kila mahali duniani. Yesu aliwaambia Mitume wake wasitarajie Wakristo wote kuwa kwenye shirika moja (Marko 9:38-39). Shirika ambalo linadai kuwa ndiyo kanisa pekee la Mungu duniani kote halipaswi kuaminiwa.

Umoja wa Kanisa la kiulimwengu inamaana kwamba makanisa yote ya mahali lazima yashike mafundisho ya Kikristo ambayo yalikuwa ya muhimu mwanzoni mwa kanisa la Agano Jipya. Katika kipindi cha Karne za kwanza, kanisa liliandika Imani ya Mitume, Kanuni ya Imani ya Nikea, na Kanuni ya Imani ya Kalkedoni kuelezea mafundisho ambayo yamekuwa muhimu kwa Ukristo tokea mwanzo. Kanuni ya Imani ni tamko la msingi kwa Imani za Kikristo.

Mafundisho kuhusu Utatu, Uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu, Upatanisho wa Kristo, na wokovu kwa neema kupitia Imani ni Msingi kwa Ukristo wa Asili.

Kozi hii haikuandaliwa kutetea dhehebu fulani. Mafundisho yaliyotetewa ndani ya kozi hii ni jumuishi. Mafunzo ya Utatu kama yalivyo elezwa kwenye historia ya Nikene, Kalkedoni, na Imani ya Atanasi za Ukristo wa mwanzoni; Mamlaka dhahiri ya Biblia; na Mafundisho ya Kiinjili ya Neema, Imani, na Wokovu.

## Mambo ya Muhimu katika Injili

Mambo yafuatayo ni ya umuhimu katika Injili. Inawezekana kabisa kwa mtu kuokoka pasipo kuwa na uewelewa kamili juu ya mambo haya. Hata hivyo, kupinga moja wapo ya mambo haya kunaondoa msingi wa Injili. Mtu au Shirika linalo pinga moja wapo ya mambo haya muhimu litakuwa au atakuwa linajaribu au anajaribu kuanzisha injili nyingine, kuamini njia zisizo sahihi za wokovu.

Unapomshirikisha mtu fulani Injili, kuna baadhi ya mambo fulani ya muhimu yatakuwepo kutokana na makosa ya kile mtu huyo tayari alikiamini mwanzoni. Kwa mfano, kama anaamini kwamba wokovu ni kupitia Shirika fulani pekee, ataamini kwamba vigezo vya kuwa mshirika wa Shirika hilo ni vya lazima ili kupata wokovu. Anapaswa kujua kwamba mtu binafsi anapokea msamaha na anakuja kwenye mahausiano ya moja kwa moja na Mungu.

**(1) Mungu akaumba mtu kwa mfano wake ili kwamba awe na mahusiano naye (Mwanzo 1:27, Matendo ya Mitume 17:24-28).**

Ukweli huu unaonesha kusudi la kuwepo kwetu na lengo la wokovu wetu. Ukweli huu unapingana na Dini ambazo haziamini katika Mungu mwenye nafsi ambaye anawapenda watu wote. Ukweli huu unaonyesha tatizo halisi lililopo duniani; watu hawapo kwenye mahusiano na Mungu.

► Vipi endapo kama mtu haamini kwamba Mungu anampenda yeye?

**(2) Watu wa kwanza walitenda dhambi na wakatengana na Mungu (Mwanzo 3:3-6, 8, Isaya 59:2).**

Hii inaonesha Asili ya dhambi na sababu ya hali ya sasa ya ulimwengu. Ulimwengu una mateso na huzuni kwa sababu ya dhambi. Bado kuna furaha na kusudi kwa sababu ya muundo wa Mungu, lakini Ulimwengu haupo vile ambavyo Mungu alipanga uwe.

► Vipi endapo mtu asipo amini kwamba dhambi ni tatizo dhahiri kwa ulimwengu?

**(3) Kila mmoja wetu ametenda dhambi dhidi ya Mungu (Warumi 3:10, 23).**

Kila mmoja wetu ana hatia ya dhambi ya kukusudia dhidi ya Mungu. Hakuna mtu ambaye mara zote amefanya kile kilicho sahihi.

► Vipi endapo kama mtu akafikiri anaweza kujihesabia haki kwa mambo aliyoyafanya?

**(4) Kila mtu ambaye hatapata Rehema atahukumiwa na Mungu na kulaaniwa kwenye adhabu ya Milele (Waebrania 9:27, Warumi 14:12, Ufunuo 20:12).**

Hii inaonesha ulazima na uharaka wa uhitaji wa wokovu kwa kila mtu binafsi.

► Vipi endapo mtu haamini kwamba kuna Mungu mwenye haki ambaye atahukumu dhambi zake?

**(5) Mtu hawezi kufanya jambo lolote ili kulipia dhambi zake alizozitenda dhidi ya Mungu (Warumi 3:20, Waefeso 2:4-9).**

Kazi nzuri na Vipawa haviwezi kulipa kwa dhambi kwa sababu dhambi ni dhidi ya Mungu asiye na mwisho ambaye kila kitu ni mali yake yeye.

► Vipi kama mtu akiamini kwamba lazima ajitengenezee uthamani ili apate msamaha wa dhambi?

**(6) Lazima kuwe na misingi ya msamaha kwa sababu dhambi ni jambo dhahiri na Mungu ni mwenye haki (Warumi 3:25-26).**

Mungu anataka kusamehe, lakini endapo kama atasamehe tu pasipo msingi, dhambi itaonekana ni jambo la kawaida sana, na Mungu ataonekana kuwa si mwenye haki.

► Kwa nini kifo cha Yesu ni Muhimu?

**(7) Yesu, mwana wa Mungu, aliishi Maisha makamilifu na alikufa kama sadaka ili sisi tupate kusamehewa, tumefanywa kuwa wenye haki mbele za Mungu mtakatifu, na kuwa na Maisha ya milele (**Yohana **3:16, Warumi 5:8-9, 1 Petro 2:22, 24).**

Kwa sababu Yesu ni mwana wa Mungu, sadaka yake ina uthamani wa milele na inatoa msingi wa msamaha kwa kila mmoja ulimwenguni. Kama angekuwa mtu wa kawaida, sadaka yake ingekuwa na uthamani wenye mipaka. Kama asingekuwa Mungu, asingekuwa na uwezo wa kutukomboa kabisa, na hivyo ni lazima tutafute njia nyingine ya wokovu.

► Kwa nini baadhi ya Dini zinafundisha watu kwamba ni lazima waokolewe kupitia kazi zao?

**(8) Yesu alifufuka kimwili kutoka wafu, akithibitisha utambulisho wake kama mwana wa Mungu na kuonesha nguvu zake ili kutupa uzima wa milele (Yohana 11:25-26, Yohana 20:24-28, Warumi 1:4, Ufunuo 1:18).**

Mafundisho potofu ambayo yanapinga ufufuko wa Yesu kwa kawaida yanapinga pia uungu wake na utoshelevu wa sadaka yake ya wokovu. Kisha wanabuni njia nyingine za wokovu.

► Ni mambo gani ambayo tunayajua kwa sababu ya Yesu kufufuka kutoka wafu?

**(9) Sadaka ya Yesu ni toshelevu kwa wokovu (Waefeso 2:8-10, 1 Yohana 2:2).**

Wokovu ni kwa Neema, Kwa Imani, katika Kristo pekee, na sio kwa matendo mema. Dini nyingi zinafundisha kwamba mtu anaweza kupata wokovu wake kwa sehemu. Hili linawaweka watu chini ya udhibiti wa mashirika ya kidini ambayo wao kusema nini wafanye ili wapate kuokolewa.

► Kwa nini baadhi ya watu wanafikiri kwamba hawawezi kuokolewa pasipo taasisi zao za Kidini?

**(10) Mungu anaokoa kila mtu anayekiri kwamba ni mwenye dhambi, anatubu dhambi yake, na kuiamini Injili (Marko 1:15, 1 Yohana 1:9).**

Hakuna taasisi ya kibinadamu yenye haki ya kuongeza kitu kwenye mahitaji ya wokovu au kutoa njia zingine za wokovu.

► Mtu wa aina gani ana haki ya kuamini kwamba ameokoka?

**(11) Toba ina maana kwamba mtu anatubu kwa ajili ya dhambi zake na kwa hiari anajiona mwenye hatia kwa dhambi zake (Isaya 55:7, Ezekieli 18:30, Ezekieli 33:9-16, Mathayo 3:8).**

Toba haimaanishi kwamba mtu akiyafanya maisha yake yawe makamilifu mbele za Mungu Mungu atamkubali. Mungu pekee ndiye anayeweza kumwokoa asiyeamini kutoka nguvu za dhambi zake. Toba inamaanisha kwamba mtu amezitubia sana dhambi zake kiasi kwamba yupo tayari kubadirika kwa kutozifuata tena. Kama mtu hayupo tayari kubadirika kwa kuziacha dhambi zake, huyo hawezi kuokolewa.

► Kwanini mtu hawezi kusamehewa pasipo toba?

**(12) Mwenye kutubu, Mwenye dhambi aaminiye hupokea wokovu pale anapo mwomba Mungu kumwokoa (Warumi 10:13, Matendo ya Mitume 2:21).**

Kila mtu anaweza kufikia rehema za Mungu kwa sababu ya Yesu. Hakuna Taasisi au wakala wa kibinadamu ambaye ni muhimu kwa mtu kupokea msamaha wa Mungu. Mtu anaupokea yeye binafsi na anaanza mahusiano ya moja kwa moja na Mungu.

► Kwa namna gani tunatambua kwamba mtu anaweza kuwa Mkristo katika kipindi cha muda fulani?

# Somo la 2
# Kuelewa Migogoro ya Kidini

## Utangulizi

► Kwanini migogoro ya kidini inatokea? Je migogoro ya kidini ni ya lazima, au inaweza kuepukika?

► Baada ya majadiliano mafupi kuhusu maswali haya, darasa litapaswa kutazama maandiko rejea yafuatayo: 1 Timotheo 3:15, Yuda 1:3; Mathayo 16:6, 12; Tito 1:9; na 1 Petro 3:15. Jadili kwa ufupi ni nini maandiko haya yana ashiria nini katika migogoro ya kidini.

Yesu alimwambia mwanamke msamaria kisimani kwamba tatizo la kuabudu kwa wasamaria lilikuwa kwamba hawakujua nani wanayemwabudu (Yohana 4:22). Ufahamu wa mwanadamu kwa Mungu ni sifa ya muhimu sana na hakika ndiyo msingi wa dini zake zote. Hakuna kosa lingine lililo dhahiri kuliko kutokuwa sahihi juu ya namna Mungu alivyo.

Inawezekana kabisa kumwabudu pasipo kuamini kitu chochote kuhusu Yeye. Kama mtu anaufahamu usio sahihi kuhusu Mungu, ataheshimu sifa ambazo Mungu hana na atashindwa kuheshimu sifa ambazo Mungu yuko nazo. Tabia binafsi za Mwenye kuabudu zitabadilika kuendana na tabia ambazo yeye anafikiri kwamba Mungu anazo.

Mtu hawezi kuweka Imani yake kwa Yesu kwa ajili ya wokovu pasipo kuamini kuamini kitu kuhusu Yesu. Kama mtu ataamini vitu visivyo sahihi kuhusu Yesu, akawa na fundisho lisilounga mkono Injili. Anaweza akaamini Injili ya uongo ambayo haiwezi kumwokoa yeye.

Kanisa lina wajibu wa kusimamia kweli. Mtume Paulo amesema kwamba kanisa ni nguzo na msingi wa kweli (1 Timotheo 3:15). Ili kusimamia kweli, Kanisa lina wajibu wa kuuelezea na kuutetea. Mtume Yuda anatuambia sisi kwamba wakati watu wanafundisha mafundisho potofu, sisi tunapaswa tu "mwishindanie imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu" (Yuda 1:3).

Fundisho potofu ni kama ugonjwa ambao unasambaza madhara yake (2 Timotheo 2:17). Fundisho potofu linafananishwa na chachu, ambayo hatua kwa hatua inaathiri donge la mkate (Mathayo 16:6).

Mungu anawaita wachungaji kuwa viongozi katika kutetea kweli. Paulo alimwambia Tito kwamba mchungaji anatakiwa kufundisha Neno kama lilivyofundishwa na pia kuwakemea wale wanaolipinga (Tito 1:9). Na pia akasema kwamba kwa sababu ya wapotoshaji, jumuiya nzima iliondolewa kutoka kwenye kweli (Tito 1:10-11).

Kozi hii sio kuhusu mafundisho ambayo yanagawa makanisa tofauti ya Kikristo kwenye makundi kama vile Wamethodist, Wabaptisti, au wapentekoste. Makanisa haya kiujumla

yanakubali juu ya mafundisho muhimu ya kibiblia yaliyomo ndani ya *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* nyuma ya Kozi hii. Badala yake, Kozi hii inatazama katika makundi ya kidini ambayo yanakana mafundisho ambayo ni msingi wa Imani ya Kikristo.

Katika somo hili tutajifunza njia nane muhimu ambazo wakristo wanapaswa kujiandaa kwazo kwa ajili ya kukabiliana na migogoro ya kidini.

Ni lazima wawe na:

1. Uzoefu binafsi katika Wokovu.
2. Kuwa imara katika fundisho la Kibiblia.
3. Kufahamu hatari ya makosa.
4. Kufahamu washirika wa Imani potofu.
5. Kufahamu asili ya dini za uongo.
6. Shirikisha Injili.
7. Kulionesha Kanisa kwa kielelezo.
8. Kutegemea Roho Mtakatifu.

## Uzoefu binafsi katika wokovu

► Kwa nini ni muhimu kwa mtu kuokoka kabla hajaingia katika mabishano ya Kidini?

Kama mtu atakuwa yeye binafsi bado hajapata uzoefu wa Neema ya Mungu,

1. Atakosa ufahamu wa kiroho wa kweli.
2. Hatokuwa na nguvu na hekima ya Roho Mtakatifu katika jitihada zake.
3. Atakuwa na nia mbaya katika migogoro ya kidini.

## Kuwa imara katika fundisho la Kibiblia

Kufahamu mafundisho ya msingi ya Ukristo yanawezesha muumini kusimama imara katika Imani, hata kama atakutana na mafundisho potofu (Waefeso 4:14). Kujifunza fundisho la Kibiblia pia kuna mwandaa Muumini kuweza kuwa vizuri katika kuwahimiza wengine kwa kukosoa fundisho potofu na kuuelezea ukweli. Hii ndio sababu kwa nini, fundisho potofu limeelezewa kote ndani ya kozi hii, imeonekana katika utofauti na Neno la Mungu. Unapotumia maandiko na mafundisho yaliyofundishwa kwenye *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* kukanusha upotoshaji wa walimu wa uongo, Imani yako itaimarishwa.

Kila mwamini anapaswa kusoma na kujifunza maneno yote ya Mungu (2 Timotheo 3:15-17). Ni upanga ambao Mungu ameutoa kwa ajili ya ushindi wa kiroho (Waefeso 6:17).

Utaratibu wa kusoma mafundisho ya Imani ya Kikristo pia ni njia muhimu ya kuimarishwa kiroho. *Misingi ya Imani ya Kikristo* ni kozi ya kwanza ya kimafundisho ya kikanuni inayotolewa na Shepherds Global Classroom, lakini pia kozi zingine pia zinapatikana.

Ni muhimu kwa muumini mpya kuimarishwa katika fundisho sahihi, lakini pia wafuasi wa Yesu waliojidhatiti wanaendelea kufuatilia ukuaji katika Kweli ya Mungu kupitia Maisha yao (Wafilipi 1:9).

## Fahamu Hatari za Makosa

Lazima tujiandae kuhoji dhidi ya makosa ya kidini. Makosa ya kidini yana matokeo dhahiri kwa sababu:

**(1) Sio kila Dini inakwambia kuamini katika Mungu na Kwenda Mbinguni.**

Baadhi ya Dini haziamini katika Mungu mkuu ambaye ni nafsi (Ubudha). Mamilioni ya watu wa Dini hawaamini wanaweza Kwenda mbinguni ambapo wataendelea kuwa kama watu (Wabudha na zaidi Wahindu).

**(2) Baadhi ya Dini huzalisha tabia mbaya na vitendo vya Kishetani**.

Dini wakati mwingine imethibitisha vitendo viovu vya mwanadamu, kama vile Hitla kuwaua mamilioni ya wayahudi. Dini kuchochea magaidi wa Kiislamu kuwaua maelfu ya watu.

**(3) Maoni ya kidini sio jambo la jaribio binafsi**.

Mtu hapaswi kuchagua maoni ya dini yake kama vile anachagua pipi aipendayo. Kila dini inadai kufafanua uhalisia. Kama watu ni halisi, na kama ulimwengu ni halisi, na kama Mungu ni halisi, basi baadhi ya dini hazipo sahihi katika namna zinavyoelezea uhalisia. Kwa mfano, kama kuna Mungu mkuu ambaye atauhukumu ulimwengu, basi watu wanaoabudu mapepo na kuruhusu mapepo kuongoza maisha yao (animism na Voodoo) hawatakuwa wameandaliwa kwa hukumu. Mtu hapaswi kuchagua tu dini anayopendelea, bali ile ambayo inaendana na uhalisia.

**(4) Ni jambo la muhimu namna gani kwamba mtu anamfafanua Mungu.**

Kama mtu anazungumza kuhusu kitu fulani ambacho sio halisi, haijalishi anakifafanua namna gani. Lakini kama Mungu ni halisi, baadhi ya Mawazo kumuhusu yeye ni sahihi, na baadhi si sahihi. Kama tu vile ambavyo itakuwa si sahihi kwa baadhi ya taarifa zitengenezwa kuhusu wewe, baadhi ya taarifa si sahihi kumuhusu Mungu, kwa sababu yeye ni halisi. Kwa sababu Yesu ni Mungu na imepaswa aabudiwe, itakuwa ni kosa la kutisha kusema kwamba yeye ni mtu tu, kama dini nyingi zifanyavyo.

**(5) Hatima ya umilele wa mtu inategemea Ukweli**

Wakati ambapo watu wanatumainia kitu fulani kwa ajili ya wokovu ambalo kiuhalisia haliwezi kuwaokoa, ni lazima sisi tujaribu kubadirisha fikra zao kabla hawajapotea moja kwa moja.

► Pitia orodha ya sababu tano za namna ambavyo makosa ya kidini yana matokeo makubwa. Ona kama ni sababu ngapi unaweza ukazikumbuka pasipo kutazamia kitabu.

Nyumba ya mtu Tajiri ilikuwa inaungua. Ndani yake kulikuwa na vitu vingi vya thamani ambavyo alihitaji kuviokoa. Watu walipokuja kusaidia, walihofia kuingia ndani ya nyumba iliyokuwa ikiungua. Mmiliki wa nyumba kwa haraka aliwapatia makoti ya plastiki ya kuzuia mvua. Akawaambia makoti yalikuwa yameundwa maaalumu kwa ajili ya kuwalinda wao

dhidi ya moto. Kwa kumwamini, wakaingia ndani ya jengo na kujaribu kutoa nje vitu alivyovitaka. Baadhi yao walifariki kwa sababu makoti hayakuweza kuwalinda. Imani yao haikuweza kuwalinda kwa sababu waliamini kitu ambacho hakikuwa cha kweli.

Mungu ni halisi, na mbingu na kuzimu ni halisi. Kutakuwa na hukumu ya mwisho juu ya dhambi zote, na kila mtu atakwenda mbinguni au kuzimu milele. Kama mtu ana dini ambayo inamsababisha atumainie vitu visivyo sahihi, matokeo yake yatakuwa mabaya na ya milele. Dini yake haitamwokoa kama sio ya kweli. Na ndio maana ni lazima pawepo na mahojiano ya kidini.

## Fahamu washirika wa Imani potofu

Ni muhimu kufahamu ni kwa jinsi gani washirika wa Imani potofu wanafikiri na kujisikia. Kama tutadharau mahitaji yao, tunaweza kushindwa kuwapatia Injili katika namna ambayo itavuta umakini wao.

Fikiri kuhusu namna ambavyo kwa mara ya kwanza ulikuja Kanisani. Pengine sio kwa sababu mtu fulani alikushinda katika mahojiano. Kwa hiyo, tusifikiri kwamba tutambadirisha mtu aliye naswa kwenye Imani potofu kwa kumshinda kwenye mahojiano pekee.

Sababu ni muhimu sana kama njia ya kuthibitisha Ukweli, lakini sababu pekee haibadirishi kujidhatiti kwa mtu.

Kipengele hiki kinatoa sababu za watu ambao wamechagua kujiunga na dini za Imani potofu. Sababu hizi sio lazima zimuelezee mtu ambaye dini yake ni sehemu ya utamaduni wake.

► Unajua nini kuhusu watu ambao wamejiunga na Imani potofu? Ni sifa zipi ambazo mara nyingi huwa nazo?

### (1) Washirika wa Imani potofu wanaamini viongozi wao ndio vyanzo pekee vya Ukweli.

Yeye anaweza kufikiri kwamba anapata Imani yake kutoka kwenye mafundisho ya mwanzilishi na maandiko ya Imani potofu, lakini anayatafsiri hayo kulingana na kile viongozi wanamwambia. Hivyo ndivyo ambavyo anaweza kupuuzia mikanganyiko katika maandiko ya Imani potofu na mafunuo.

Viongozi wa Imani potofu wanafundisha mafundisho ya kipekee ambayo hayapatikani sehemu nyingine kwa kusudi la kubakia kuwa chanzo pekee cha ukweli kwa washirika wao. Wanatoa mamlaka ya mwisho, iwe kwa maandishi au kwa kuishi, ambayo inachukua nafasi ya Biblia katika utendaji, hata kama wanadai kuamini Biblia.

### (2) Washirika wa Imani potofu hawaliamini kanika la Kikristo kiujumla.

Washirika wa Imani potofu wamefundishwa kwamba makanisa ya kikristo ni maasi, hayana ukweli, na hayana baraka za Mungu. Viongozi wa Imani potofu mara kwa mara wameyadhihaki makanisa ya Kikristo. Kinyume chake, makanisa halisi ya kikristo

yanatambua kwamba makanisa mengine pia yana ukweli kwamba ni muhimu kwa mtu kumjua Mungu na kufika mbinguni.

Baadhi ya viongozi wa Imani potofu wameendeleza utoaji wa mafunuo mapya, ili kwamba waamini ndiyo chanzo cha ukweli.

**(3) Mshirika wa Imani potofu hana ufahamu wa historia ya Kanisa na Utamaduni**

Washirika wa Imani potofu wana uelewa mdogo wa jinsi gani Kanisa limekabiliana na mambo ya kale. Hawaelewi ni kwa namna gani Biblia ilitunzwa. Hawajui mafundisho yapi ni msingi wa Injili na ni muhimu kwa ukristo. Wanafikiri kwamba Kanisa limekuwa si sahihi juu ya mafundisho mengi kwa Historia yake. Hawawezi kutambua kwamba kwa kuyapinga mafundisho ya msingi wamekuwa sehemu ya dini mpya.

**(4) Washirika wa Imani potofu wanatarajia mateso na migogoro.**

Kama ukibishana na mshirika wa Imani Potofu, watachukulia kwamba umedanganywa, mjinga, unafuata nia mbaya, na pengine unashikiliwa na shetani.

Washirika wa Imani potofu wanatarajia kuteswa na watu wa dini zingine. Kama mtu atawatenda wao vibaya, hilo linawathibitishia wao kwamba wapo sahihi.

**(5) Mshirika wa Imani potofu ana Imani ambazo zinapingana kila moja.**

Inafikirika kwamba mshirika wa Imani potofu hutunza Imani yake katika vyumba tofauti. Yeye halinganishi Imani toka kwenye chumba kimoja na chumba kingine. Anashangazwa pale ambapo watu wanapomwonyeshea mwingiliano huo, na yeye hajisikii uhitaji wa kufanya utatuzi.

**(6) Mshirika wa Imani potofu alishawishiwa na mazoea zaidi kuliko kufikiri.**

Washirika wa Imani potofu wanaonekana kutumia fikra wakati ambapo wana wasilisha mafundisho yao kwa watu wa nje. hata hivyo, kufikiri kwao kumeegemea zaidi kwenye upofu wa kitumaini wa Imani potofu. Fikra zimetengenezwa kuunga mkono kile ambacho wamekwisha kiamini.

Yeye amekubali Imani potofu kwa sababu amejihisi kupendwa na kukubaliwa na washirika, au kwa sababu ya namna alivyojisikia kwenye wakati wao wakuabudu, au kwa sababu ya uzoefu binafsi wa kiroho. Baada ya kuingia kwenye mahusiano na Imani potofu, akaanza kuyapokea mafundisho yao pasipo kuyatathimini. Wakati watu wa nje wanapobishana juu ya mafundisho, yeye anahisi kwamba hawafahamu nini hali gani amekutana nayo. Anafikiri kama angeweza kuwafanya wavuke mabishano na waingie kwenye ile hali, wangeweza kushawishika.

**(7) Mshirika wa Imani potofu anaamini injili tofauti.**

Kumfanya mtu kuwa mwaminifu, Imani potofu haiwezi kuwa pekee kwenye mafundisho madogo pekee; Lazima iwe na upekee kwenye kitu muhimu. Na ndio maana sasa utofauti

wa mafundisho ya Imani potofu yanajumuisha injili tofauti. Mshirka wa Imani potofu anaamini kwamba wokovu ni kupitia Imani potofu pekee.

**(8) Mshirika wa Imani potofu hana utosholevu wa Kiroho.**

Kwa sababu bado hajaokoka, hana uhakika wa msamaha; hana ushindi dhidi ya nguvu ya dhambi; hana furaha ambayo inayokuja kutokana na kuwa na mahusiano na Mungu; na hana ushirika wa kweli wa kikristo na washirika wenzake wa Imani potofu. Anahitaji kusikia Injili.

## Fahamu asili ya Dini za Uongo.

► Dini za uongo zinatokea wapi?

Kufikiri kwamba dini ya uongo inatokana na nia ya kupata faida, kutoka kwenye mazoea mabaya, au kutoka kwenye mapepo ni kutokufahamu utata wa kidini. Katika kuitikia dini za uongo, sisi ni lazima tufahamu vipengele vya chimbuko zake.

**(1) Mawazo ya kibinadamu**

Dini za uongo mara kwa mara zimeanzishwa na kufafanuliwa na watu wenye uwezo mkubwa wa akili ambao wamewaza kuhusu Imani za kidini pasipo ufunuo wa kimungu wala uongozi wa Roho Mtakatifu (1 Wakorintho 2:6-9).

**(2) Nia ya faida binafsi**

Sio walimu wote wa kidini ni wakweli. Biblia inafundisha kwamba mafundisho potofu yamefundishwa na watu ambao waliharibu ufahamu wao, waliukataa ukweli, na ni wanafki (1 Timotheo 1:5-6, 19, 1 Timotheo 4:2). Baadhi ya viongozi wa kidini wamekuwa matajiri kwa mafundisho yao potofu (2 Petro 2:1-3).

**(3) Upofu wa Kiroho**

Watu ambao hawapo kwenye mahusiano na Mungu wamepofushwa Kiroho. Si kwamba tu wanakosa mtazamo wa Kiroho, lakini pia mtazamo wao wa kiasili haupo sahihi (2 Wakorintho 4:3-4).

**(4) Kuukataa ukweli**

Roho mtakatifu ni mwaminifu katika kuuthibitishia ulimwengu wa dhambi, haki, na hukumu (Yohana 16:7-11). Mtu ambaye anaukataa ukweli anafanya uchaguzi kwa hiari, kwa hiyo, ushawishi na maelezo havitoshi kubadili ufahamu wake. Biblia inasema kwamba mtu ambaye anaendelea na makosa ya mafundisho muhimu anapaswa akataliwe kutoka kanisani kwani anatenda dhambi (Tito 3:10-11).

**(5) Hali ya kiroho**

Dini ya uongo sio ibada isiyo na kitu. Mapepo yanahusika katika ibada ya uongo. Biblia inatuambia kwamba watu wanaoabudu sanamu wanaabudu mapepo (1 Wakorintho 10:20-21). Hii ni kwamba watu walio kwenye dini za uongo wanaweza kuwa na hali hii ya kiroho.

**(6) Ufunuo potofu**

Mafundisho ya Dini potofu sio yote huanzishwa na mwanadamu. Biblia inatuambia sisi kwamba kuna mafundisho yanayotoka kwa mapepo (1 Timotheo 4:1).

► Kuna kama sababu sita ambazo zinaweza kuichangia kwenye uundwaji wa Dini potofu. Zipi miongoni mwa hizi unaweza kuzikumbuka pasipo kutazama katika kitabu?

**Tabia za kiujumla za Imani potofu**[1]

- Kundi linaonyesha bidii na kujitoa pasipo kuulizwa kwa uongozi wake wa kibinadamu, na linazingatia mfumo wake wa kiimani na utendaji kama ukweli halisi.
- Swali, mashaka, upinzani vinavunjwa moyo, au kuadhibiwa kabisa.
- Kundi hutumia matendo ya kubadili ufahamu (kama vile kutafakari, kunena kwa lugha na ibada ya kufurahi).
- Viongozi ndio wanaamuru washiriki wawaze vipi, watende, na kuhisi (kwa mfano, washirika lazima wakati mwingine wapate ruhusa kuwa kwenye mahusiano, kuoa au kubadili kazi. Viongozi walishapendekeza nini cha kuvaa, wapi pa kuishi, na kama washirika wanaweza kuwa au kutokuwa na watoto).
- Kundi linadai umaalumu, hadhi tukufu kwa ajili yake, viongozi wake, na washirika wake (Kwa mfano, kiongozi anachukuliwa kama mtu maalumu au Masihi).
- Kiongozi hawajibiki kwa mamlaka zozote.
- Uongozi unashawishi hisia za aibu na/au hatia ili kuwadhibiti washirika.
- Utii kwa uongozi au Kundi unahitaji washirika kukata mahusiano na familia na marafiki, na kwa kiasi kikubwa kubadili malengo binafsi.
- Kundi limeshughulishwa na kuleta washirika wapya.
- Kundi linashughulishwa na kutengeneza pesa.
- Washirika wanatazamiwa kujitolea kupita kiasi kwa kundi na shughuli zinazohusu Kundi.
- Washirika wanatiwa moyo au wanatakiwa kuishi/au kuhusiana na washirika wa Kundi pekee.

[1] Imechukuliwa kutoka https://www.apologeticsindex.org/268-characteristics-of-cults. Ilipatikana Juni 3, 2020.

## Shirikisha Injili

Ni vizuri kujifunza tabia maalumu za Imani potofu na jinsi gani tunaweza kukanusha makosa. Hata hivyo, ni muhimu zaidi kushirikisha Injili.

Upatapo nafasi kushirikisha Injili, usipoteze muda kubishana juu ya mambo madogo madogo. Usimchukize mshirika wa Imani potofu kwa kubishana kuhusu ukweli wa kihistora juu ya Imani potofu yake ambayo huwezi kuthibitisha. Lenga kwenye mambo ambayo ni ya muhimu kwa Injili, na usimruhusu akwepe mambo hayo pasipo kujibu.

Mazungumzo yanapoisha, ni muhimu sana wawe wamesikia ujumbe wa namna ya kuokoka. Mabishano kuhusu mambo mengine hayataweza kuwaokoa hata kama utatoa hoja vizuri kuliko wao.

Wakati unaongea na mshirika wa Imani potofu, ni muhimu kwa mkristo kuonyesha uwazi na kumjali huyo mtu. Mkristo atapaswa kuwa kama mtu ambaye anajali kuhusu rafiki yake. Mkristo atakuwa na hasira katika namna vile tu rafiki anahasira kwa ajili ya mtu aliye umizwa. Kama mshirika wa Imani potofu anakuona wewe kama adui, atakataa kushawishika. Kama mahojiano yataonekana kama mashindano, atakataaa kushindwa.

Mkristo ni lazima aonyeshe upendo, kukubaliwa, wasiwasi wa kweli, na uwazi kwa kweli—kuonesha kwamba kweli anataka kufahamu.

## Kuongoza Kanisa

Kanisa la mahali lenye Afya ni ushindi mkuu dhidi ya Imani potofu inayochochewa ndani ya jamii.

Uinjilisti wa washirika wa Imani potofu hauwezi kufanywa kwa watu binafsi kuwashawishi watu binafsi wengine. Kwa kawaida mtu hawezi kubadilisha dini yake pasipo kufikiri juu ya Jamii ya kiimani atakayoiacha na ile atakayoingia. Kama mshirika wa Imani potofu ataanza kuvutiwa na ushuhuda wa Mkristo binafsi, ataitaji kuona jamii ya kiimani ambayo mkristo huyo anaiwakilisha. Ataitaji kuona ni kwa jinsi gani wanaiishi Imani. Ana fikiria kwamba ujumbe anaousikia tayari umeshaunda jamii ya kiimani ambayo ataingia kama atabadilika.

Hii inamaanisha asili ya kanisa la mahali ni muhimu sana. Ili kuvutia mtu ambaye anafikiria kubadili kutoka kwenye jamii tofauti ya kiimani, Kanisa la mahali lazima liwe na sifa fulani.

► Ni tabia zipi za kanisa ambazo zingeweza kuwavutia watu kutoka kwenye imani potofu?

### Sifa za kanisa la mahali lenye mvuto

- Washirika wanaonyesha kwamba mahusiano yao na Mungu ni Halisi na yanawatosheleza. (Washirika wa Imani potofu hawana mahusiano na Mungu.)
- Kanisa linawasilisha mafundisho katika namna zote mbili kama maelezo ya ukweli na kama masharti ya kimahusiano na Mungu. (Mafundisho ya Imani potofu yanapingana na kila moja na hayamleti mtu kwa Mungu.)

- Kanisa linaonyesha kwamba lina furahia kumwabudu Mungu. (Kuabudu katika Imani potofu ni katika mwili, na kishetani.)
- Washirika wa kanisa wanaonesha kusudi la maisha katika mtazamo wa umilele. (Imani potofu inadai kufanyia kazi vipaumbele vya umilele. Kanisa lazima lionyeshe jinsi ya kuishi leo kwa kuyapa uthami yaliyo ya milele.)
- Kanisa linaonyesha kipaumbele cha huduma badala ya malengo ya kiulimwengu .(Imani potofu wanaita kwa kujitoa kihuduma, lakini viongozi wao wana malengo ya kiulimwengu.)
- Ujumbe wa Kanisa unatosheleza uhitaji wa ndani wa Kiroho. (Imani potofu haina Injili ambayo inagusa uhitaji wa kiroho.)
- Kanisa ni Familiya ya Imani ambayo inapenda na kujali washirika wake (Linaweza kudai kujali washirika wake lakini lisiweze kuwa na ushirika wa kweli wa Kikristo.)

► Matendo gani maalumu ungetegemea kuyaona kwenye Kanisa ambalo lina sifa zilizo orodheshwa?

### Kumtegemea Roho Mtakatifu

Siku zote kumbuka kwamba ni Roho Mtakatifu pekee anaweza kusababisha wenye dhambi kujua hatia zao, kuelewa ukweli, na kumtamani Mungu. Mwinjilisti awezi kuwa mtendaji mzuri isipokuwa tu kama ataongozwa na kupakwa mafuta na Roho Mtakatifu.

► Ni kwa namna gani utaweza kufafanua utofauti kati ya mtu anayemtegemea Roho Mtakatifu na Mtu asiye mtegemea Roho Mtakatifu?

# Somo la 3
# Umomoni

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

John alikutana nao kwa mara ya kwanza alipokuwa anapita kati kati ya bustani ya mapumziko alipokuwa naelekea nyumbani kwake. Walikuwa ni vijana wawili wa kiume waliokuwa wamevaa suluali nyeusi na mashati meupe, walikuwa wamevaa vijibao vya majina. Walikuwa na hali ya urafiki na walitaka kuzungumza naye kuhusiana na dini yao. John aliwasikiliza na hakuuliza maswali mengi. Walionekana kutokea katika makanisa ya kawaida na walionekana kuongea mambo yale yale aliyoyasikia kanisani. Walisema wao wanatokea katika kanisa la Yesu Kristo la Mitume wa mwisho, ambalo pia linaitwa Momoni.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Isaya 41 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki kinatueleza nini kuhusu Mungu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Umomoni

### Asili na Historia

Umomoni ulianza na mtu anayeitwa Joseph Smith. Joseph alidai kwamba siku moja katika mwaka 1820, aliomba kwamba Mungu amuoneshe yeye ni kanisa lipi lilikuwa sahihi. Alipokuwa anaomba, aliona maono. Aliwaona watu wawili wakiwa na kanzu nyeupe, ambao walikuwa Yesu na Mungu Baba. Mungu alimwambia kwamba hakuna kanisa ambalo lilikuwa sahihi na kwamba Imani zao ni machukizo.

► Ni mambo gani ambayo si sahihi kibiblia kuhusiana na maono haya?

Joseph alidai kwamba alipata maono ya mwisho yaliyomuelekeza wapi pa kuchimba vibao vya dhahabu vyenye maandishi juu yake. Alitafsiri maandishi haya kwa msaada wa miwani maalumu na akayachapisha kama kitabu cha Momoni. Hakuna mwingine aliyewahi kuona vibao au miwani kwa sababu malaika alivichukua na kuvirudisha mbinguni kwa ajili ya ulinzi.

Joseph alikuwa mshirika wa zamani wa Masonic lodge (kikundi cha watu waliotengeneza taasisi ya siri yenye taratibu, liturujia, na alama zake) na alinakili taratibu za siri za Umomoni kutoka katika maelekezo ya Masory, ikijumuisha viapo vya damu, nywila, na kupeana mikono kwa siri.

***Biblia inasema kwamba mitume hawakuwa na dini ya siri, bali walikuwa wazi kwa kila kitu walichokiamini, ona 2 Wakorintho 4:2 na 2 Timotheo 2:2.***

Kanisa la Momoni liliundwa pale New York mwaka 1830. Katika 1839, walihamia kwanza Nauvoo, Illinois, kisha Missouri. Smith alisema kwamba Missouri palikuwa ndio nchi ya ahadi kwa ajili ya Wamononi, na kwamba hekalu litajengwa ajili ya Independence, Missouri.[2] Hekalu halikuwahi kujengwa na Wamomoni walihama tena. Smith alitoa nabii nyingi sana ambazo hazikuwahi kutimilika.

***Biblia inasema kwamba endapo unabii wa mtu haukutimilika, hatakiwi kuaminiwa kama nabii, ona Kumbukumbu la Torati 18:22***

Smith alisema, "Nina mengi zaidi ya kujivunia kuliko mtu mwingine yeyote anavyoweza kujivunia. Mimi ni mtu pekee ambaye nimeweza kuliweka kanisa pamoja tangu nyakati za Adamu. Wengi kati ya wengi wamesimama na mimi. Sio Paulo, Yohana, Petro, au hata Yesu ambaye aliweza kufanya hivi. Najivuna kwa sababu hakuna mtu aliyefanya kazi kama nilivyofanya mimi. Wafuasi wa Yesu walimkimbia: lakini watakatifu wa mwisho hawajawahi kunikimbia mimi bado."[3]

Joseph alishambulia na kuharibu mashine za uchapishaji za gazeti ambalo lilikemea vikali ndoa zake za mitala. Joseph akiwa gerezani akisubiri kesi yake, kundi la watu walishambulia gereza na kumuua Joseph na kaka yake Hiram.

***Biblia inasema kwamba mchungaji hatakiwi kuwa mtu wa majivuno, mwepesi wa hasira, au mgomvi, ona Tito 1:7***

Smith alimtaja kijana wake kama mrithi wake, lakini baada ya kifo cha Smith wengi walimfuata Brigham Young na wakahamia mji wa Salt Lake, wakiuacha "nchi ya Ahadi."

Wamomoni wanaamini kwamba Ukristo wa kweli uliisha na vifo vya mitume na haukuwepo tena hadi Smith alipoanzisha kanisa la Momoni.

► Ni matukio gani baadhi katika kanisa la Momoni ambayo yanatufanya sisi kuwa na mashaka kwamba ni Ukristo wa Kweli umerejeshwa duniani?

### Ushawishi wa Sasa

Kuna madhenemu mengi tofauti tofauti ya Wamomoni ambayo yamejimega kutoka katika mtembeo wa awali ambao ulianzishwa na Joseph Smith. Baadhi yao ni madogo sana.

Kanisa kubwa la Wamomoni lina makao makuu yake huko mji wa Salt Lake City, Utah na linadai kuwa na washirika karibu milioni 17 ulimwenguni. [4] Wanachapisha machapisho kwa lugha 188.

---

[2] Joseph Smith, *Doctrine and Covenants*, Section 57

[3] Joseph Smith, "26 May 1844 (Sunday Morning)," katika *The Words of Joseph Smith*, ilitafutwa Julai 19, 2024, https://rsc.byu.edu/words-joseph-Smith/26-may-1844-sunday-morning.

[4] Takwimu zote zinatoka katika "Facts and Statistics | Worldwide Statistics," The Church of Jesus Christ of Latter-day Saints, https://newsroom.churchofjesuschrist.org/facts-and-statistics, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

Wana wamisionari wa muda wote karibu 55,000. Wamisionari mara nyingi huwa ni vijana watu wazima ambao wanajitolea kwa mwaka 1½ au 2. Wanaweza kutumwa kokote kule ulimwenguni ambapo Wamomoni wana huduma na hawana uwezo wa kuchagua. Wanafanya kazi bila kuwa na mshahara wowote.

**Mafundisho Magumu ya Wamomoni**

***Ndoa za mitala (ndoa za wake wengi)***

Joseph Smith alidai kwamba ndoa za mitala ziliagizwa na Mungu kama njia ya wanaume kuwa miungu baada ya kifo, lengo kuu la kila Mmomoni. Wanaume wanapaswa kuwa na wake wengi kwa ajili ya umilele, ili kwamba waweze kuujaza ulimwengu mpya kwa namna ile ile ambayo Mungu ameijaza dunia.[5]

***Biblia inasema kwamba mchungaji anapaswa kuwa na mke mmoja tu, ona Tito 1:6.***

Smith alioa wake 27. Mdogo zaidi kwa umri alikuwa na miaka 14. Baadhi yao walikuwa wameolewa na waume wengine, lakini Smith alisema kwamba ndoa zao za awali hazikuwa halali endapo zilifanyika nje ya Umomoni. Kiongozi baada ya Smith, Brigham Young, alikuwa na wake 57 na watoto 165.

***Biblia inasema kwamba mtu anayemuoa mtu aliyetalikiwa anafanya uzinzi, ona Mathayo 5:32.***

Smith alisema kwamba ndoa za mitala lilikuwa ni agano la Mungu la milele, na kwamba lilianzishwa kabla ya misinhgi ya ulimwengu. Baadae mitume wa kanisa la Momoni walisema kwamba ndoa za mitala ilikuwa ni njia pekee ya kuufikia uungu[6] na haitabadilika kamwe.

Wamomoni waliendelea kuwa na ndoa za mitala hadi 1890, wakati ambapo serikali ya United States ilipotishia kutaifisha ardhi ya kanisa kwa sababu walikuwa wanavunja sheria. Kwa wakati huo, nabii wa kimomoni Woodruff akadai kupata ufunuo kutoka kwa Mungu kwamba ndoa za mitala zimemalizika.

► Wamomoni wengi hawana ndoa za mitala kwa sasa. Kwa nini historia yao ya ndoa za mitala bado ni shida kwa wao kuaminika?

***Ubaguzi wa Rangi***

Kulingana na fundisho la Umomoni, kila mwanadamu alikuwa roho mbinguni kabla hajazaliwa. Kulikuwa na vita mbinguni, wale ambao hawakupigana kwa uaminifu kwa ajili ya Mungu, walilaaniwa kwa kupewa rangi nyeusi. Wanaume wote walionukuliwa katika kifungu hiki cha maneno walikuwa maraisi wa kanisa la Momoni na walichukuliwa kuwa manabii wa Mungu. Joseph Smith alisema kwamba ikiwa mtu mweusi ataamini mafundisho ya Umomoni na kutenda sawasawa, baada ya vizazi kadhaa watapata ngozi nyeupe.

[5] Joseph Smith, *Doctrine and Covenants*, Section 132
[6] Brigham Young, *Journal of Discourses,* Volume 11, 269

Brigham Young alisema kwamba ngozi nyeusi na pua bapa ni laana ya Kaini. Alisema hivyo kama kanuni ya milele kutoka kwa Mungu kwamba mtu ambaye ana damu ya Kiafrika hawezi kuwa kuhani. Pia alisema kwamba utumwa wa watu Weusi ni taasisi ya kimungu. Joseph Fielding Smith alisema kwamba watu Weusi wanapata kile wanachostahili hapa duniani kwa sababu ya kile ambacho roho zao zilifanya kabla hawajazaliwa. David McKay alisema kwamba ubaguzi wa rangi wa wanegro haukuanza na kanisa bali na Mungu.

***Biblia inasema kwamba katika Kristo hakuna tofauti ya utaifa, ukabila, ona Wagalatia 3:28.***

Katika Umomoni, mshirika mwanaume anatakiwa kuwa kuhani. Katika sehemu kubwa ya historia yao, Wamomoni hawakuwaruhusu wanaume Weusi kuwa makuhani, ambayo ilimaanisha hawakuwa washirika kamili. Mwaka 1978, kanisa la Momoni lilidai kwamba limepata ufunuo mpya ambao ulibadilisha kila kitu ambacho walikuwa wamekisema kuhusiana na watu Weusi tangu mwanzo, na sasa wanawaruhusu watu Weusi kuwa makuhani.[7]



*Sanamu ya malaika Moroni iko juu ya kila hekalu la Kimomoni.*

► Wamomoni wanadai kuwakubali watu Weusi katika hali sawa na tabaka lingine. Kwa nini historia yao ya ubaguzi wa rangi bado ni tatizo kwa uhalali na uaminifu wao?

### *Nguo ya Ndani*

Washirika wa Momoni wanatakiwa kuvaa nguo maalumu ndani ya nguo zao za nje. Nguo maalumu ni nyeupe na inafunika karibu mwili wote. Inasadikika kwamba inawapatia wao ulinzi wa kiroho. Inawakilisha ahadi yao ya kuwa waaminifu kwa kanisa. Wanatakiwa kuivaa mchana na usiku.

### Mafundisho Potofu ya Wamomoni

Kila mshirika wa Momoni anatakiwa kuamini kwamba Joseph Smith alikuwa nabii wa Mungu na kwamba Kitabu cha *Momoni* ni Agano jingine la Kristo, linalolingana na Biblia kimamlaka. Pia wana kitabu cha mafunuo kinachoitwa *Mafundisho na Maagano* ambapo wanaamini kwamba kimevuviwa kama vile Biblia. Wanaamini kwamba Biblia haitoshi kutengeneza mafundisho yao muhimu.

> "Kwa kadiri lugha chanya inavyoweza kusema, Agano la Kale linathibitisha kwamba Mungu ni wa Milele, hana mwanzo wala mwisho, anapita mipaka ya muda."
> - W.T. Purkiser
> *God, Man, and Salvation*

Wamomon wanadai kwamba dini yao ndio Ukristo wa kweli. Mafundisho yao mengi yanakinzana na mafundisho ya kikristo ya kihistoria yanayounga mkono injili. Ni ngumu

[7] Picha na ErikaWittlieb kutoka Pixabay, ilichukuliwa tena kutoka https://pixabay.com/photos/moroni-angel-statue-prophet-mormon-1467937/.

kugundua upotofu ukiwa unazungumza na mshirika wa Kimomoni kwa sababu wengi hawafahamu yale ambayo manabii wao walifundisha.

Kanisa la Momoni linaamini kwamba wakati fulani Mungu alikuwa mwanadamu kama sisi, lakini anakua hadi kufikia kuwa Mungu kama alivyo sasa.[8] Wanaamini kwamba Mungu Baba ana mwili wa nyama. Ana wake wengi. Watoto wake wanazaliwa kwanza kama roho, kisha wanatumwa duniani ili kuzaliwa kama wanadamu.

Wamomoni, wanasema wanaamini kwamba Yesu alizaliwa na bikira, lakini kanisa la Momoni linafundisha kwamba Mungu Baba alimfanya Mariamu kuwa na mimba kwa kutumia njia ya kawaida kwa kutumia mwili wake.

***Biblia inasema kwamba bikira Mariamu alipata mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, ona Luka 1:34-35 na Mathayo 1:18. Biblia pia inasema kwamba Mungu ni Roho, Yohana 4:24.***

Wamomoni wanaamini kwamba kabla Yesu hajazaliwa, alikuwa roho alikuwa roho kama malaika wengine; hakuwa Mungu.

***Biblia inasema kwamba Yesu ni neno la Mungu na kwamba yeye ni Mungu hata kabla hajaja ili kuzaliwa duniani, ona Yohana 1:1-2, 14.***

Wamomoni wanaamini kwamba Roho Mtakatifu na Yesu ni tofauti na Baba, na kwamba hawako sawa na Baba. Hawaamini Utatu Mtakatifu.

► Kwa maneno machache, ni kwa namna gani utaelezea tatizo katika mtazamo wa Wamomoni kuhusu Mungu?

Wamomoni wanaamini kwamba mwanaume wa kimomoni anaweza kukua na kuwa kama Mungu. Wanaamini kwamba wengi wameshafanya hivi tayari, na kwamba kuna miungu wengi. Mtume Lorenzo Snow alisema, "kama mwanaume alivyo, Mungu alikuwa; na kama Mungu alivyo, Mwanaume atakuwa."

Joseph Smith alisema, "hapa ndipo Maisha ya milele—kumfahamu Mungu pekee mwenye hekima na wa kweli; na unapata kujifunza namna ya kuwa Mungu mwenyewe, na kuwa wafalme na makuhani kwa Mungu kitu kile kile ambacho Miungu wote wamefanya kabla yako."

Wamomoni wanaamini kwamba watu wachache watakwenda katika jehanamu ya milele. Wamomoni wanaamini kwamba watu wanapewa nafasi ya kuukubali Umomoni baada ya kifo. Wamomoni waaminifu watakwenda katika tabaka la juu sana la mbinguni.

***Biblia inasema kwamba watu wengi watatupwa jehanamu Pamoja na Shetani na mapepo, ona Mathayo 25:41.***

---

[8] Joseph Smith katika *History of the Church*, Volume 6, 305

Wamomoni wanaamini kwamba wokovu ni zawadi kwa ajili ya Maisha ya utumishi mwaminifu kwa Mungu. Wamomoni hawadai kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

***Biblia inasema kwamba wokovi ni zawadi ya Mungu, haupatikani kwa matendo ona Waefeso 2:8-9.***

Wamomoni wanaamini kwamba makanisa mengine yote ni ya kishetani, na kwamba hakuna wokovu ispokuwa kupitia kanisa la Momoni. Hakuna umoja unaowezekana kati ya Wamomoni na Wakristo.

► Kwa nini umoja kati ya Wamomoni na Wakristo hauwezekani? Toa sababu mbalimbali.

**Mbinu ya Wamomoni**

Wamomoni huwauliza watu kumuomba Mungu ili kwamba awaoneshe kama kitabu cha Momoni ni kweli na endapo Joseph Smith alikuwa nabii. Watu wengi hudai kuhisi moto ndani ya mioyo kama majibu ya maombi yao. Wanafikiria kwamba hisia za kuchomwa mioyo yao inathibitisha kwamba Umomoni ni kweli. Hisia hiyo haiwathibitishii wao kwamba wameokoka kibinafsi.

***Biblia inasema kwamba hatupaswi kuamini injili nyingine hata kama inasemwa na malaika, ona Wagalatia 1:8.***

Wamomoni wanadai kuamini Biblia, lakini Biblia inakana mafundisho yao. Wanasema kwamba Biblia inamakosa ya kunakili na tafsiri. Wanasema kwamba ufunuo zaidi unahitajika kwa sababu ya makosa katika Biblia. Kwa Mmomoni, mamlaka ya juu ni Ufunuo wa Joseph Smith. Kwa sababu wanaamini alikuwa nabii wa Mungu, wanaamini Imani yote ya Umomoni ambayo inakinzana na Biblia.

"Maandiko matakatifu yanajumuisha kila kitu kinachohitajika kwa ajili ya wokovu. Chochote ambacho hakiko ndani ya Biblia, na ambacho hakiwezi kuthibitishwa na Biblia, hakitakiwi kuwekwa kama tamko la Imani au takwa la wokovu. Tunavichukulia vitabu vya Agano la Kale na Jipya—vile ambavyo mamlaka yake hayatiliwi shaka na kanisa—kuwa Maandiko Matakatifu."

- Imeasiliwa kutoka Articles of Religion
of the Church of England

***Yesu alisema kwamba mbingu na nchi zitapita, lakini maneno yake hayatapita, Mathayo 24:35. Alisema kwamba hakuna Neno la Mungu litakalopotea kabla halijatimizwa, ona Mathayo 5:18. Petro alisema kwamba Neno la Mungu linadumu milele, ona 1 Petro 1:25. Mungu anatarajia sisi tuamini Neno lake kuliko kuangalia ufunuo mpya.***

Wamomoni wanatumia maneno yale yale yanayotumiwa na Wakristo, lakini yanamaanisha kitu kingine. Wanasema kwamba Yesu ni mwana wa Mungu, lakini hawamaanishi kwamba yeye ni Mungu. Wanasema kwamba Roho Mtakatifu ni mshirika wa tatu wa Uungu, lakini hawaamini katika Utatu Mtakatifu.

Wanasema kwamba Yesu alizaliwa na Bikira, lakini wanaamini kwamba Mungu Baba alimpa mimba Mariamu kwa njia ya kawaisa ya kimwili.

Wanasema kwamba Yesu alikufa kama dhabihu kwa ajili ya dhambi zetu, na kwamba wanaweza kuomba kusamehewa, lakini wanaamini kwamba mbingu ni zawadi kwa Maisha ya uaminifu.

Wamomoni wanadai kuwa ni Ukristo halisi. Wanadai kwamba makanisa mengine yote ni ya uongo. Lakini endapo mtu ataelewa na kuamini mafundisho yote ya Umomoni, atakuwa haamini injili ya kimaandiko na si Mkristo.

> "Namwamini... Yesu Kristo Mwana wake wa pekee,
>
> Bwana wetu, Aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu."
>
> - Imani ya Mitume
> (Iliandikwa katika karne ya kwanza ili kufupisha mafundisho ya mitume .)

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno **mlalo na lililokolezwa**.

## Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

► Mafundisho katika orodha ifuatayo yanakataliwa na Wamomoni. Tazama *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* kuona umuhimu wa kila fundisho na uthibitisho wake. Hakikisha umeelewa jinsi gani mistari rejea inathibitisha fundisho.

(1) Biblia inajitosheleza kwa mafundisho.

(2) Kuna Mungu mmoja tu.

(3) Mungu Baba sio mwanadamu.

(4) Mungu hajawahi kubadilika.

(5) Yesu ni Mungu.

(7) Roho mtakatifu ni Mungu.

(8) Mungu ni Utatu.

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani.

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

(13) Wale ambao hawajaokoka watapata hukumu ya milele.

## Uinjilisti

Inaonekama kana kwamba haiwezekani kubadilisha ufahamu wa Mmomoni, lakini ukweli ni kwamba maelfu ya Wamomoni wanaacha makanisa ya Kimomoni kila mwaka.

Jaribu kumuonesha Mmomoni kwamba mafundisho yake muhumu sana yako kinyume na Injili. Tumia Ushahidi uliotolewa katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*. Toa Ushahidi huu kwa yeyote ambaye anaonesha kutaka kujua katika Umomoni.

Usikubali kuomba kwamba Mungu akuoneshe kama Umomoni ni kweli. Haupaswi kumuomba Mungu kukuonesha kitu wakati tayari umeshafahamu kweli. Kuomba kwa namna hiyo kunampa Shetani fursa ya kukupa uzoefu ambao utakuchanganya.

Wamomoni hawana uhakika binafsi wa wokovu. Wengi wao huishi katika hofu kwamba maisha yao hayatakubaliwa na Mungu. Hakikisha kwamba unawashirikisha injili na kuwaambia ni kwa namna gani wanaweza kuwa na uhakika wa wokovu. Hilo ni muhimu kuliko kitu kingine chohcote ambacho unaweza kuwaambia.

Unaweza usione matokeo ya mazungumzo yako. Mwisho wa mazungumzo yenu Mmomoni anaweza asikuambie kwamba amebadilisha akili yake. Hata hivyo, haufahamu matokeo ya muda mrefu ya mazungumzo hayo. Roho Mtakatifu ataendelea kutumia kweli ambayo umeitoa.

## Ushuhuda

Joanna alikua katika kanisa la kimomoni na alishiriki kila kitu walichofanya. Alichukuliwa kuwa mfano mzuri wa kuigwa wa msichana wa Kimomoni. Alipoondoka nyumbani ili kujiunga na Chuo Kikuu cha Idaho, alialikwa ili kuhudhuria kipindi cha kujifunza Biblia. Alienda akiwa na matumaini kwamba anaweza kumshawishi mmoja kuwa Mmomoni. Katika kujifunza Biblia, alijifunza mambo kuhusu Mungu kutoka katika Biblia ambayo alikuwa hajawahi kuyafahamu. Aliona kwamba Wakristo huko walikuwa na ushirika na Mungu ambao yeye hakuwahi kuwa nao. Aliliacha kanisa la Momoni na kuishi kwa ajili ya Mungu hata kama familia yake na marafiki zake wengi wa Kimomoni walimkataa. Mungu alimpatia yeye familia mpya ya Kikristo na marafiki wengi sana kuliko hapo kabla. Joanna anasema, “Kwa wale ambao wameacha kanisa la Momoni na wanafikiria kuhusu kukata tamaa kuhusu Mungu, usifanye hivyo… Mungu bado ana makusudi kwa ajili yako.”

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Isaya 41 tena. Kila mwanafubzi aandike kifungu cha maneno akielezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa mfuasi wa Umomoni. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa Kila Somo

Wakati wote wa kozi hii utakuwa na mazungumzo na wafuasi wa dini mbali mbali na Imani potofu ambazo unajifunza. Utahitaji kuwa na mazungumzo na washirika angalau 10 kutoka makundi mbalimbali ya dini. Unatakiwa kuwasilisha injili na kweli nyingine za Kikristo.

Endapo haiwezekani kwako kumpata mshirika wa kundi la dini unalojifunza katika somo mahususi, unatakiwa kumtafuta mtu mwingine ambaye anaonesha shahuku ya kusikiliza nyenzo.

Baada ya mazungumzo yako, utatoa ripoti.

1. Utaandika ripoti ya kurasa 2 na kuwasilisha kwa kiongozi wako wa darasa. Katika ripoti hiyo unapaswa uelezee Imani za msingi za kundi hilo, majibu ya kibiblia ya Imani hizo, mazungumzo yako na asiyeamini, na mwitikio wao kuhusiana na kile ulichokisema.
2. Utawaambia wana darasa wenzako kuhusiana na mazungumzo mtakapokutana darasani.

Mazungumzo 10 na zoezi la kuandika ndio mazoezi ya msingi ya kozi hii.

# Somo la 4
# Mashahidi wa Yehova

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Waligonga mlango wa Samweli na wakampatia nakala ya gazeti la *Awake*. Wageni walikuwa mwanamke na Watoto wake wawili. Walikuwa wamevaa vizuri na walikua na hali ya urafiki. Andiko la gazeti lilihusu namna ya kuwasaidia Watoto kufanya vizuri shuleni. Mwanamke alisoma mstari katika Biblia, akatoa mafafanuzi juu yake, na kisha akamuuliza Samweli endapo angekuwa na shahuku ya kutembelewa kwa ajili ya kujifunza Biblia. Samweli alisema angefikiria kuhusu hilo.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Waebrania 1 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha andiko kinasema nini kuhusiana na Yesu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Mashahidi wa Yehova

### Historia

Charles Russell alianzisha Chama cha Tracts cha Mnara wa Mlinzi wa Sayuni mnamo mwaka 1881 ili kuchapisha na kusambaza mafundisho ya kipekee. Taasisi ilibadilisha jina na kuwa Mashahidi wa Yehova mnamo mwaka 1931.

Russell aliandika seti ya matoleo sita ya kujifunza maandiko. Alisema kwamba watu watakuwa vizuri sana kwa kusoma vitabu vyake pasipo Biblia kuliko kusoma Biblia pasipo vitabu vyake. Alisema kwamba mtu aliacha kusoma vitabu vyake na kusoma Biblia tu, atakuwa gizani kwa miaka miwili, lakini akisoma vitabu vyake pasipo Biblia, atakuwa nuruni.

***Biblia inasema kwamba Neno la Mungu ni nuru na linatuongoza sisi, ona Zaburi 119:105. Roho Mtakatifu anawafundisha wafuasi wa Kristo hata kama hatuna waalimu wa kimwili, ona 1 Yohana 2:27.***

Mafundisho ya Mashahidi wa Yehova yamebadilika mara nyingi.

Viongozi wa Mashahidi wa Yehova wametoa nabii nyingi ambazo hazijatimia. Kwa mfano, kiongozi wa pili, Rutherford, alitabiri kwamba Abrahamu, Isaka, na Yakobo watafufuliwa na mwaka 1925 na kuishi katika nyumba ya kifahari ambayo ameandaa kwa ajili yao. Hawakuja, lakini aliishi kwenye nyumba peke yake.

***Biblia inasema kwamba endapo unaabii wa mtu usipotimia, hapaswi kuaminiwa kama nabii, ona Kumbukumbu la Torati 18:22.***

Mashahidi wa Yehova wanaamini kwamba makanisa mengine yote ni ya Kishetani, na kwamba hakuna wokovu ispokuwa kupitia taasisi yao.

***Yesu aliwaambia wanafunzi kwamba watumisho wote wa Mungu hawatakuwa katika taasisi moja, ona Luka 9:49-50. Wokovu unapatikana kwa Yesu tu, na si kwa taasisi yeyote, ona Matendo ya Mitume 4:10, 12.***

► Ni mambo gani baadhi ambayo tayari unaweza kuyaona ambayo yanaonesha kwamba Mashahidi wa Yehova si Ukristo wa kibiblia?

**Ushawishi wa Sasa**

Mashahidi wa Yehova wanadai kwamba wana kazi katika nchi 239 na wanachapisha katika lugha zaidi ya 900. Wamechapisha karibu bilioni 40 za vipande vya machapisho.[9] Wana makusanyiko karibu 118,000, na washirikia walio hai zaidi ya milioni 8.[10]

Makao makuu ya Mashahidi wa Yehova yapo huko Brooklyn, New York.

**Mafundisho Magumu ya Mashahidi wa Yehova**

Mashahidi wa Yehova hawashiriki katika uchaguzi wa serikali au kushikilia ofisi yeyote serikalini, kwa sababu wanaamini wao wametengwa kutoka katika ufalme wa dunia hii.

***Katika Biblia, watu kama Nehemia, Modekai, na Danieli walimtumikia Mungu lakini pia walizifanyia kazi serikali za mataifa mengine, ona Nehemia 1:11-2:1; Esta 8:2, Esta 10:3; na Danieli 6:1-3.***

Hawatumikii jeshi na wanaamini kwamba vita haijawahi kuwa sahihi.

Hawasheherekei sikukuu yeyote, ama ni sikukuu ya kitaifa, sikukuu za kikristo, au kumbukizi za kuzaliwa, kwa sababu wanaamini kwamba sherehe zote zinafuata taratibu za kipagani.

Hawakubali kuongezewa damu, hata kama ni kuokoa maisha, kwa sababu maandiko yanayokataza kula damu.

Hawatoi fungu la kumi, na wachungaji wao hawalipwi mshahara.

Mashahidi wa Yehova hawaamini kwamba mtu anaweza akaokolewa mara moja baada ya kuweka Imani yake kwa Kristo. Wanaamini ni lazima ajiunge na taasisi yao, ajifunze mafundisho yao, na aanze kutendea kazi matakwa yao. Wokovu ni mchakato, na wakati mtu anapojua kwamba ameokoka, hana uhakika.

---

[9] "What Is the Watch Tower Bible and Tract Society?" Jehovah's Witnesses, https://www.jw.org/en/jehovahs-witnesses/faq/watchtower-society/, ilitafutwa Aprili 11, 2023.
[10] "Fast Facts—Worldwide," Jehovah's Witnesses, https://www.jw.org/en/jehovahs-witnesses/worldwide/, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

***Katika Agano Jipya, watu walikuwa Wakristo wakati walipotubu na kuweka Imani yao kwa Kristo, ona Matendo ya Mitume 2:41 na Matendo ya Mitume 8:26-39. Hii inawezekana kwa sababu tunaokolewa kwa neema na sio kwa matendo.***

Kila mshirika anatakiwa kurejesha ripoti ya kila mwezi ya kazi ya ushuhudiaji. Mshirika ambaye haleti ripoti ya ushuhudiaji anaondolewa kutoka katoka orodha ya washirika hai na anachukuliwa kuwa hajaokoka.

***Biblia inasema kwamba huko mbinguni Mungu anaorodha ya wale ambao wameokolewa, ona*** **Luka** ***10:20 na Ufunuo 21:27. Orodha hiyo haimilikiwi na taasisi yeyote.***

► Kulingana na Mashahidi wa Yehova, ni kwa namna gani mtu anaokolewa?

Mashahidi wa Yehova hawaukubali msalaba kama alama ya Ukristo, na wanaamini kwamba Yesu alikufa juu ya mti.

Wanasema kwamba fundisho la Utatu Mtakatifu linapaswa kukataliwa kwa sababu haliingii akilini na haiwezekani kulielewa, kana kwamba hakutakiwi kuwa na chochote katika asili ya Mungu ambayo ni zaidi ya uelewa wetu.

Mashahidi wa Yehova wanaamini kwamba Roho Mtakatifu sio Mungu, lakini ni nguvu isiyo ya kinafsi ambayo inatoka kwa Mungu, ikilinganishwa na nguvu ya umeme.

> "Ninamwamini... Bwana mmoja, Yesu Kristo, Mwana wa pekee wa Mungu, amezaliwa na Aliyezaliwa kwa Baba tangu milele yote, Mungu kutoka Mungu, Nuru kwa Nuru, Mungu kweli kwa Mungu kweli, amezaliwa, hakuumbwa, Mwenye umungu mmoja na Baba..... Ninamwamini Roho Mtakatifu, Bwana na Mtoa uzima, aliyetoka kwa Baba na Mwana, anayeabudiwa na kutukuzwa, pamoja na Baba na Mwana, aliyesema kwa manabii."
>
> - Tamko la Imani ya Nikea (Iliandikwa na kanisa mwaka A.D. 325.)

Wanadai wanaamini katika ufufuo wa kimwili wa Yesu, lakini wanaamni kwamba ni roho yake tu ndio iliyofufuka, na si mwili wake.

► Kwa nini mafundiho haya yaitwe "mafundisho magumu"?

Upotofu mkubwa na mbaya zaidi wa mafundisho ya Mashahidi wa Yehova ni kukana uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu.

Mashahidi wa Yehova wanadai kuwa wao ni Wakristo wa Kweli. Wanadai kwamba makanisa yote ni ya uongo. Lakini kama mtu ataelewa na kuamini mafundisho yote ya Mashahidi wa Yehova, hatakuwa anaamini injili ya kibiblia na hivyo si mkristo.

### Mbinu za Mashahidi wa Yehova

Mtu anapokuwa na shahuku ya kujiunga na mashahidi anapaswa kupitia Kujifunza Biblia kwa miezi kadhaa. Anapaswa kufanya mabadiliko katika maisha yake na kufuata kile ambacho anajifunza. Kisha anabatizwa na kuwa "mtoa machapisho," na anatakiwa kugawa machapisho kutoka katika taasisi.

Kwa wastani, mtoaji wa machapicho anatumia masaa 10,000 kabla hajampata mtu mmoja mpya.[11]

Kila mshirika ananunua machapisho kutoka katika taasisi ili kuyasambaza.

Hawaiti mikusanyiko yao makanisa. Wanaamini kwamba makanisa ni ya Kishetani. Wanayaita majengo ya "Jumba la Ufalme."

***Agano Jipya liliandikwa kwa makanisa, ona Ufunuo 1:4 na 1 Wakorintho 14:33.***

Wanajaribu kuthibitisha mafundisho yao kwa watu kwa kutumia Maandiko ambao wanaiamini Biblia pasipo kuifahamu sana. Wamechapisha tafsiri yao ya Biblia inayoitwa *The New World Translation*, yenye mabadiliko ambayo yanaunga mkono mafundisho yao. Wamebadilisha mistari mingi inayoonesha uungu wa Kristo. Tafsiri hii haikutolewa na wasomi wa kweli wa lugha za Biblia.

Wanasema kwamba Yesu ni mwana wa Mungu na mwokozi wa ulimwengu, na kwamba alifanya wokovu uwezekane. Wanafundisha kwamba Yesu ni kitu cha kwanza kuumbwa na Mungu na alikuwa tu mtu mkamilifu, sio Mungu.

> "Ufufuo ulikuwa na ni mtetezi wa Yesu. Kwa huo, utambulisho wa Yesu na utume wake ulithibitishwa."
>
> - Willard Taylor
> God, Man, and Salvation

► Katika Wakolosai 1:16-17, tafsiri ya New World Translation imeongeza neno "vingine," ili kwamba mstari uoneshe kwamba Yesu aliumba vitu vingine vyote, yeye ni kabla ya vitu vingine vyote, na kwa ajili yake vitu vingine vyote vipo. Unafikiri ni kwa nini Mashahidi wa Yehova waliongeza neno hilo?

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

► Mafundisho katika orodha ifuatayo yanakanwa au yanakataliwa na Mashahidi wa Yehova. Tazama *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* ili kuona umuhimu wa kila fundisho na uthibitisho wake. Hakikisha umeelewa ni kwa jinsi gani mistari rejea inathibitisha fundisho

(5) Yesu ni Mungu.

(6) Yesu alifufuka kimwili kutoka kwa wafu.

(7) Roho mtakatifu ni Mungu

(8) Mungu ni Utatu

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani

---

[11] Imepigwa hesabu kutoka namba zilizoripotiwa mnamo "2022 Grand Totals," Jehovah's Witnesses, https://www.jw.org/finder?wtlocale=E&pub=syr22, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu

(13) Wale ambao hawajaokoka watapata hukumu ya milele

## Uinjilisti

Usiwatendee Mashahidi wa Yehova kwa ukali. Kwa sababu wanaamini kwamba wanateswa kwa ajili ya kweli, wanategemea wakristo wa kiinjilisti kuwatendea vibaya. Badala yake, waoneshe upendo wa Kristo na kuwajali. Hii pengine ndio njia yenye ufanisi ya kuwaleta kwa Kristo.

Msibishane kuhusiana na mambo madogo, kama kusheherekea sikukuu au kufanya kazi jeshini. Ni muhimu zaidi kuzungumza kuhusiana na misingi ya injili na uthibitisho wa wokovu.

Kipaumbele ni kiushirikisha injili. Mashahidi wa Yehova hawana uthibisho wa wokovu na mahusiano binafsi na Mungu.

## Ushuhuda

Paulo alilelewa kama Shahidi wa Yehova, na ndugu zake wingi bado wapo katika Imani hii potofu. Akiwa mtu mzima alijitenga mbali na taasisi, lakini bado aliamini kwamba walikuwa sahihi. Mke wake alikuwa mkristo, na aliamua kumthibitishia kwamba Mashahidi wa Yehova walikuwa sahihi. Katika kujifunza kwake aligundua kwamba walikuwa wametoa nabii nyingi za uongo. Alianza kusoma Maandiko na akagundua kwamba Yesu ni Mungu, na si malaika kama ambavyo amekuwa akifundishwa. Alisoma mstari ambao Yesu alisema, “Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima” (Yohana 14:6), na akatambua kwamba alichokuwa anakihitaji si imani ya kidini, bali mahusiano na Yesu.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Waebrania 1 tena. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki kwa Shahidi wa Yehova. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 5
# Iglesia ni Cristo (Inglesia ni Kristo)

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

> "Katika moyo wa Imani ya Kikristo ni tangazo kwamba Bwana wetu Yesu Kristo, mwana wa Mungu wa milele, alifanyika mwili kwa ajili ya wokovu wetu."
>
> \- Willard Taylor
> *God, Man, and Salvation*

Mark alikuwa Mromani Katoliki na aliwahi kuwa padre lakini aliacha upadre. Siku moja alikuwa anaaza kazi mpya. Wakati mtu yule alipokuwa namuonesha namna ya kufanya kazi, Mark aligundua kwamba alikuwa mafuasi wa Iglesia ni Cristo. Mark akasema, "Mimi namshikilia Yesu; Yeye ni Mungu wangu." Yule mtu akamwambia kwamba Yesu sio Mungu, na kwamba mchungaji wake anaweza kuthibitisha kutoka katika Biblia kwamba Yesu alikuwa mpatanishi tu. walimuonesha Mark maandiko mengi, na akachanganyikiwa. Walimshawishi kwamba Yesu sio Mungu.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Ufunuo 1 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha maandiko kinastuambia nini kuhusu Kristo? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Iglesia ni Cristo

### Chanzo na Ushawishi

Jina la taasisi hii inatafsiriwa "Kanisa la Kristo." Kuna taasisi nyingine pia wanatumia maneno hayo hayo katika majina yao.

Iglesia ni Cristo ilianzishwa huko Ufilipino mwaka 1914 na Felix Manalo, mshirika wa awali wa Usabato. Wakati wa kifo chake, mtoto wake alikuwa kiongozi, kisha mjukuu akafuata baada yake.

Iglesia ina mikusanyiko 7,000 katika nchi 164.[12] Mengi yapo huko Ufilipino. Ni taasisi kubwa sana inayojitangaza kuwa ya Kikristo huko Ufilipino ispokuwa kanisa la Romani Katoliki.

Iglesia ni Cristo linafanya kazi ili kuboresha jamii. Imani potofu hujihusisha sana na siasa na kuwaambia washirika au wafuasi wao nani wa kumpigia kura katika uchaguzi. Viongozi wa kisiasa hutafuta idhini au kukubalika kutoka kwa viongozi wa dini. Iglesia iliunga mkono uongozi wa Marcos huko Ufilipino.

[12] "About Us," Iglesia ni Cristo (Kanisa la Kristo), https://iglesianicristo.net/about-us/, ilitafutwa Aprili 11, 2023.



Iglesia ni taasisi au shirika tajiri sana na linasisitiza kuhusu majengo ya kanisa yaliyojengwa kwa ubunifu mkubwa.[13] Iglesia wamejenga kanisa kubwa sana ulimwenguni lenye ukumbi mkubwa sana ndani kwa ajili ya vikao na ibada. Ingawaje wengi wa washirika wao ni masikini, viongozi wao wengi ni wana taaluma kama vile madaktari na wanasheria.

Iglesia wanamiliki vituo vya redio. Wanachapisha gazeti la kila mwezi, *Pasugo: God's Message*. Mara zote Gazeti kinashambulia Uromani Katoliki na makanisa ya kiinjili.

Waongofu wengi wa Iglesia ni wa Romani Katoliki ambao tayari wameamini kuwa Biblia ni kweli lakini hawakuwa na ufahamu mzuri na sawasawa wa Biblia. Washirika wa Iglesia wanawaonesha mistari ya Biblia ili kuwashawishi kuacha mafundisho waliyofundishwa.

Iglesia wana mikusanyiko mikubwa kwenye miji mikubwa duniani. Waongofu wengi wa Iglesia nje ya Ufilipino ni Wafilipino ambao wamehamia kwenda kwenye nchi hizo.

► Kwa nini waongofu wengi wa Iglesia wanatoka kanisa la Romani Katoliki?

**Fundisho la Kanisa na Upatanisho**

Mafundisho muhimu sana ya Iglesia ni kwamba lenyewe ni kanisa la kweli, lililorejeshwa na Felix Manalo. Fundisho hili linasisitizwa kiasi kwamba injili ya Iglesia inaonekana inajumuisha fundisho la kanisa lao na chanzo chake.

Wafuasi wa Iglesia wanaamini kwamba Felix Manalo alikuwa mtunishi wa mwiho wa Mungu. Pia waliamini kwamba Manalo ametajwa mahususi kabisa mara kadhaa katika unabii wa kibiblia, kama vile Isaya 41:9-10, Isaya 43:5-7, Isaya 46:11, na Ufunuo 7:2-3.

Isaya 41:9-10 ni kuhusu mtumishi maalumu wa Mungu aliyepakwa mafuta. Wakristo wanaamini kwamba kifungu hiki kinamrejelea Yesu, Masihi, lakini wafuasi wa Iglesia wanasema kwamba kinamrejelea Felix Manalo. Wanasema kwamba kifungu cha maneno "ncha za nchi" kinamaanisha ni nyakati za mwisho za dunia. Wanaamini Manalo aliutimiza unabii huo kwa sababu alisajili kanisa lake siku ile ile ambayo vita kuu wa kwanza ya dunia ilianza, ambayo ni mwanzo wa nyakati za mwisho za dunia. Maneno *ncha za nchi* katika Biblia kimsingi zinamaanisha mahali ambapo ni mbali kijiografia.

Katika Isaya 46:11, Mungu anasema atamuita ndege mkali kutoka nchi ya mbali kutoka Mashariki ambaye atatimiza kusudi lake. Wasomo wa Biblia wamekuwa wanaelewa kwamba Mungu atatumia nguvu ya nchi ya kigeni ili kuliadhibu taifa la Israeli, ambayo inakubaliana

[13] Picha: "8651Iglesia ni Cristo churches Malolos City 09" na Judgefloro, ilichukuliwa tena kutoka kwa https://commons.wikimedia.org/wiki/File:8651Iglesia_Ni_Cristo_churches_Malolos_City_09.jpg, umiliki wa uma.

na alama ya ndege mkali. Iglesia wanaamini kwamba huduma ya Felix Manalo ilitabiriwa na mstari huu.

Wafuasi wa Iglesia wanaamini kwamba kanisa la Kikristo lilikengeuka mara baada ya kifo cha mitume. Wanaamini kwamba makanisa yote ispokuwa la kwao yamekengeuka, na kwamba Manalo alirejesha kile kilichokuwa kimepotea baada ya mitume kufa.

► Ni kwa namna gani unaweza kujibu madai ya Iglesia, kwamba Manalo ametimiliza unabii mahususi wa Biblia? Tazama mistari anayotumia na zingatia matumizi ya muktadha.

Iglesia wana mafundisho ya kipekee kuhusu upatanisho. Yanamsingi katika agizo la Agano la Kale kwamba mtu hapaswi kuadhibiwa kwa ajili ya makosa ya wengine. Waalimu wa Iglesia wanasema kwamba Yesu hakufa kwa ajili ya dhambi za wengine kwa sababu jambo hilo lingeenda kinyume na sheria ya Mungu. Lakini, kwa sababu Biblia inasema kwamba kanisa ni mwili wa Kristo, ikiwa mtu atajiunga na kanisa hatakuwa mtu mwingine, lakini ni sehemu ya Kristo. Kwa hivyo, Yesu hakufa kwa ajili ya mtu mwingine yeyote alipokufa kwa ajili ya wale walio kanisani. Mafundisho haya ya upatanisho yanalifanya kanisa lao kuwa lenye umuhimu wa juu sana kwa ajili ya wokvu, kwa sababu wao ni kanisa pekee la kweli.

► Elezea ni kwa jinsi gani Iglesia wanadai kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya washirika wa kanisa lao tu.

Nyimbo nyingi za Iglesia ni kuhusu kanisa. Imani yao kwamba wao ni kanisa pekee la kweli inaonekana katika mfano huu kutoka katika mojawapo ya nyimbo zao unaoitwa "Kweli moja, Imani moja":

> Kweli moja, Imani moja
> kanisa Moja, mahali ambapo tunapata neema
> tumaini Moja ndani
> kanisa moja la kweli la Kristo.[14]

## Imani nyingine na Desturi

Viongozi wa Iglesia wana shahuku sana ya kuwabadilisha watu kujiunga na sini yao. Wanasisitiza watu kufanya kazi ya kueneza ujumbe wa kanisa.

Wanaume na wanawake wanakaa pande tofauti za kanisa wakati wa ibada. Milango hufungwa wakati wa kuanza.

Masomo yanayosisitizwa katika nyimbo zao ni kanisa, kuvumilia shida za maisha, na maombi kwa ajili ya msamaha. Wanaomba kwamba Mungu awasaidie kushika amri zake ili wastahili kupokea msamaha.

Viongozi wa Iglesia wanadai kwamba Biblia ni chanzo cha Imani zao. Mtindo wao wa kufundisha ni kutumia mistari mingi katika Biblia yote ambayo inaonekana haina

[14] Maneno ya wimbo "One Truth, One Faith," kutoka https://incmedia.org/one-truth-one-faith/, ilitafutwa Machi 16, 2023.

mahusiano. Wanatumia tafsiri mbalimbali za Biblia na wanaweza kunukuu kutoka tafsiri sita tofauti tofauti ujumbe mmoja. Wanamweza kujaribu kujibu kila swali kwa kutumia andiko. Wengi wa washirika wao wanadai kwamba kilichowashawishi kujiunga ni matumizi ya Imani potofu ya maandiko

> "Sisi, kisha, kwa kuwafuata mababa watakatifu, wote kwa nia moja, tunafundisha watu kukiri mwana mmoja yule yule, Bwana wetu Yesu Kristo, yule yule Mungu kamili katika uungu; Mungu kweli na Mwanadamu kweli."
>
> - Imani ya Chalcedonian (Iliyoandikwa na kanisa mwaka 451 B.K.)

Iglesia hawaamini Utatu au uungu wa Kristo au Roho Mtakatifu.

Washirika wa Iglesia mara zote wanashambulia mafundisho ya Uungu wa Kristo katika machapisho yao. Wanafundisha kwamba Yesu alikuwa mtu maalumu lakini hakuwa Mungu. Wanasema kwamba kama mtu anasema kwamba Kristo ni Mungu, basi hamfahamu vizuri Yesu na hajaokoka.

Wanaamini kwamba, wakati wa kufa nafsi inakufa na haitaendelea kuishi ispokuwa Mungu amemfufua au amemuumba tena mtu. Hawaamini juu ya Jehanamu.

Hawaamini kwamba mtu anaokoka kwa kuweka Imani yake kwa Kristo baada ya kusikia injili ikihubiriwa au kusoma Biblia. Wanaamini kwamba wokovu ni mchakato. Kulingana na Iglesia ni Cristo, ni lazima mtu ajiunge na kanisa na kushika matakwa ya kanisa ili aweze kuokoka. Hata hivyo, hawakuhakikishii kwamba mtu anaweza kuokoka kwa kuwa mshirika wa kanisa. Wanaamini mtu anaweza kupoteza wokovu wake endapo hataishi sawasawa. Kwa sababu ya mafundisho haya, washirika wao wengi huishi katika hofu kwamba hawajaokoka.

► Kwa nini Iglesia ni Cristo hawatoi uhakika wa papo kwa papo wa wokovu?

Iglesia ni Cristo wanadai kuwa wao ni Wakristo halisi. Wanadai kwamba makanisa mengine yote ni ya uongo. Lakini endapo mtu atayaelewa na kuyaamini mafundisho yote ya Iglesia, basi haamini katika Injili ya Kimaandiko na yeye si mkristo.

### Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

► Kwa sababu Iglesia ni Cristo wanadai wanaamini Biblia, Biblia inaweza kutumika kukanusha mafundisho yao. Tumia mafundisho katika sehemu zifuatazo kutoka katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* ili kukanusha Imani potofu hii.

(5) Yesu ni Mungu.

(7) Roho Mtakatifu ni Mungu.

(8) Mungu ni Utatu.

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(11) Tunapokea wokovu kwa imani.

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

(13) Wale ambao hawajaokoka wtapata hukumu ya milele.

### Uinjilisti

Unaweza ukaona kwamba mafundhisho ya Iglesia ni Cristo yanafanana sana na mafundisho ya Mashahidi wa Yehova. Washirika wao wanaishi katika hofu kwamba hawajaokoka bado.

Ni muhimu kusisitiza msingi wa injili. Kumbuka kwamba unazungumza na watu ambao wanategemea mafundisho kwamba wataokoka endapo watakuwa katika kanisa sahihi. Sisitiza Maandiko yanayofundisha uthibitisho au uhakikisho binafsi wa wokovu. Waoneshe kwamba, ni hadi pale watakapoweka Imani yao kwa Kristo kwa ajili ya wokovu, ndipo watakapofahamu kwa hakika ya kwamba wameokoka.

### Ushuhuda

Miguel alikuwa mhudumu katika Iglesia ni Cristo. Alipokuwa anazidi kufahamiana na wachungaji wengine katika kanisa, alikatishwa tamaa kwa kugundua kwamba hawakuwa wakiishi kwa viwango vya maisha matakatifu ambayo waliyahubiri. Waliwahubiri watu wao kwamba wanapaswa waishi maisha matakatifu na ya haki. Kwa Miguel ilionekana kwamba kwa kadiri mtu alivyokuwa anaishi maisha machafu, ndivyo alivyokuwa anahubiri kwa nguvu habari za maisha matakatifu ya haki. Miguel alisema kwamba wachungaji walitaka kuondoka katika taasisi lakini hawakujua namna ya kufanya. Walikuwa wanaogopa mateso. Miguel alifanya maamuzi ya kuondoka katika taasisi na akang'ang'ana au akashikilia mafundisho sahihi.

### Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Ufunuo 1 tena. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki kwa mfuasi wa Iglesia ni Cristo. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

### Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 6
# Eastern Lightning (Mwangaza wa Mashariki)

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Shang Hui alikuwa mchungaji huko China. Alianza kusikia watu wanaacha kanisa ili kujiunga na Kanisa la Mungu Mwenyezi. Hata wazazi wake walikuwa wamejiunga. Alipokutana na washirika wa Imani potofu, walisema, "Jina la Mungu lilikuwa ni Yehova, lakini wakati huo alikuwa ni Yesu duniani. Mungu anaweza kutenda jambo jipya tena, na kuwa Kristo mwingine duniani." Shang alichanganyikiwa kwa mafundisho yao. Alivunjika moyo katika huduma yake kwa sababu Imani potofu ilikuwa inakua kwa haraka.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma 2 Timotheo 3 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha maandiko kinatuambia nini kuhusu dini potofu ya Kikristo? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Eastern Lightning

### Chanzo na Ushawishi

Jina rasmi la Imani Potofu inayoitwa Eastern Lightning ni Kanisa la Mungu Mwenyezi. Dini ilianzishwa mwaka 1989 huko China. Linakadiriwa kuwa na washirika kati ya 100,000 na 1,000,000.

Eastern Lightning wanaamini kwamba Mungu alijifunua Yeye mwenyewe wakati wa Agano la Kale kama Yehova, kisha akaja duniani kama Yesu, na sasa amekiuja duniani katika mfumo wa mwanamke anayejiita Lightning Deng. Jina lake awali lilikuwa Yang Xiangbin. Deng hajioneshi hadharani, na hajulikani namna gani alivyo au yuko wapi. Kiongozi anayeonekana wa Imani potofu ni Zhao Weishan, ambaye anaweza kuwa mume wa Yang.

> "Ufunuo [wa Biblia] sasa umekamilika. Mungu hataongeza chochote katika huo, kwa sababu umajumuisha yote muhimu kwa ajili ya mwanadamu, vyote ilirejelea ulimwengu huu na ule ujao, na ametangaza hukumu kinyume cha wale wanaoongeza au kupunguza chochote kutoka humo."
>
> - Adam Clarke
> *Christian Theology*

***Biblia inatuambia tusiamini wakituambia kwamba Masihi amefichika duniani, ona Luka 17:23.***

Eastern Lightning wanadai kuwa Biblia sasa imepitwa na wakati, na kwamba ufunuo unahitajika. Imani potofu imechapisha vitabu kadha, vikiwemo, *Lightning from the Orient*,

ambacho wanadai kwamba ni ufunuo kutoka kwa Mungu kuja kwa kristo mwanamke. Kitabu kinazungumza na Wakristo na kinawatishia kwa adhabu iliyoelezewa kwa kina.

***Yesu alisema kwamba maneno yake hayatapita kwamwe, ona Marko 13:31.***

Eastern Lightning wanafundisha kwamba Jina la Yesu limepitwa na wakati na halina nguvu, na kwamba Deng ndiye kristo kwa sasa.

***Yesu alitimiliza unabii wote kuhusiana na Maisha, kifo, na ufufuo wa Masihi. Kwa hiyo, Masihi mwingine haitajiki, ona Luka 24:44, Mathayo 16:16 na*** Mathayo ***24:4-5.***

Walitabiri mwisho wa dunia kuwa ni Desemba 21, 2012.

► Ni mambo gani unayoyaona yanayoonesha kwamba taasisi hii si ya Kikristo?

**Shughuli na Mkakati**

Eastern Lightning mahususi kabisa wanalenga makanisa ya Kikristo, hata kuchagua Wakristo wenye nguvu kabisa. Habari zinaelezwa za watu ambao walikuwa kwenye huduma za kikristo kuacha makanisa na kujiunga nao. Washirika wa Imani potofu wanajifanya kujiunga na makanisa na kisha huwapa wachungaji kiasi kikubwa cha fedha endapo watajiunga. Imani potofu haijishughulishi sana na watu wa dini nyingone au makundi mengine.

***Biblia inazunguma juu ya wale ambao wanachukia mema, ona* 2 Timotheo *3:3.***

Imani potofu hutumia ukahaba ili kuwavuta waongovu wenye nguvu. Watu wanaojiunga hutengwa na wenza wao na wanatakiwa kujihusisha na uasherati na uzinzi.

***Wakristo wanatunza utakatifu na wanalinda ahadi na viapo vya ndoa, ona Waefeso 5:3, Waebrania 13:4.***

Washirika wa Eastern Lightning wamekuwa wanajulikana kwa kutumia mateso, kuteka, na uuaji ili kukamilisha makusudi yao. Wanawavamia viongozi wa taasisi za Kikristo. Hukataa waongofu wao kuondoka na kuacha ushirika wao.

***Biblia inasema kwamba Mkristo anapaswa kuwa mpole, akitii sheria, na si mgomvi, ona see Tito 3:1-2.***

Endapo mtu ataonesha anavutiwa na kujiunga, wanampa zawadi, lakini wanamtishia kwa ukali au vurugu endapo mtu hatajiunga. Washirika wa Imani potofu kusimulia kuhusiana na watu kupata magonjwa ya kufisha kutoka kwa Mungu kwa kukataa kujiunga na Imani potofu. Wanajaribu kuwafanya Wakristo waingie katika uasherati, kisha wanamlaghai au kumtishia ili wapate kitu.

***Hekima ya Mungu ni ya amani, ya upole, na safi, Yakobo 3:17.***

Washirika wa Imani potofu wanadai kwamba wanasingiziwa kuhusiana na vurugu, lakini Wakristo wengi na Wamisionari huko China wameshuhudia vitendo vyao.

Washirika wanatakiwa watoe kila kitu ka ajili ya Imani potofu. Wanatiwa moyo kuziacha familia zao na kuishi na watu wa imani potofu na kufanya kazi ya kusambaza ujumbe.

Eastern Lightning wameanza kusambaza taasisi yao katika nchi nyingine. Wanaanza kwa kuwapa watu machapisho katika makanisa ya Kichina.

► Ni kwa namna gani matendo ya kanisa la kweli yanakinzana na matendo ya Eastern Lightning?

> "Yesu akashuka kuzimu; Siku ya tatu akafufuka, akapaa mbinguni, ameketi mkono wa kuume wa Mungu Baba Mwenyezi: Kutoka huko atakuja kuwahukumu watu walio hai na waliokufa."
>
> - Imani ya Mitume

> "Kiini kikuu cha fundisho la upatanisho ni kwamba kifo cha Kristo ni malipizi, kimewezesha chanzo cha wokovu. Kifo cha Kristo kimefanya wokovu wetu uwezekane."
>
> - Thomas Oden
> *The Word of Life*

**Imani**

Wafuasi wa Eastern Lightning wanatambua kwamba Krsito alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, lakini hawamini kwamba mtu anaweza kuokolewa na Kristo pasipo taasisi yao. Ili kuokolewa, mtu anapaswa kuachana na Imani yake kwa Yesu na badala yake amfuate Deng, Kristo mwanamke. Wanakana ufufuo na ujio wa Kristo mara ya pili.

Wanaamini kwamba yeyote ambaye haamini ujumbe wa Deng (Kristo mwanamke) atahukumiwa na Mungu.

***Biblia ilitabiri watu ambao watakataa kweli na kujaribu kuligawa kanisa, ona Yuda 1:17-19.***

> Sasa wajibu wa mtu ni kumfuata Kristo mwanamke, na endapo tu ataikana Imani yake katika Yesu Kristo, achane Biblia yake hadharani, ajiite mwenyewe "mwana wa shetani," "ameshindwa" kwa kujikabidhi kikamilifu kwa maneno yalizungumzwa ya Kristo mwanamke na kisha anakuwa "mshindi," ataingia ufalme wa Mungu ambao umeanzishwa duniani na Kristo mwanamke.[15]

► Ni kwa namna gani tunafahamu kwamba Yesu Kristo na Neno la Mungu bado ni muhimu kwa Mkristo?

[15] "The Development and Beliefs of the Eastern Lightning Cult", China For Jesus, ilitafutwa Novemba 1, 2023, http://www.chinaforjesus.com/EL_development.htm.

Kanisa la Mungu Mwenyezi (Eastern Lightning) linadai kuwa ni Ukristo halisi. Linadai kwamba makanisa mengine yote ni ya uongo. Lakini endapo mtu ataelewa na kuamini mafundisho yote ya Eastern Lightning, haamini injili ya kibiblia na sio mkristo.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno mlalo na lililokolezwa

### Tumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

► Mafundisho katika orodha ifuatayo yanakanwa au yanakataliwa na Eastern Lightning. Tazama *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* kuona umuhimu wa kila fundisho na uthibitisho wake. Hakikisha umeelewa ni kwa jinsi gani mistari rejea inathibitisha fundisho

(5) Yesu ni Mungu

(7) Roho mtakatifu ni Mungu

(8) Mungu ni Utatu

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu

### Uinjilisti

Hata kama mikakati ya vurugu, kutokuwa na maadili, na uongo ya Imani hii potofu inaonekana kama taasisi ya kigaidi, wengi wa wafuasi wake hawafahamu shughuli za viongozi wao. Hasa hasa katika nchi nyingine tofauti na China, watu wanaovutiwa na Imani potofu wanaweza wasiamini mashitaka dhidi yao. Kwa hivyo, ni muhimu kwa Wakristo kuwa na uwezo wa kujibu mafundisho yao.

Haiwezekani mtu kujihusisha kikamilifu na Imani potofu na kuamini mafundisho yao kuwa ya Kikristo. Kwa hivyo, wana njaa ya kiroho ambayo haijaridhishwa. Kipaumbele cha Mkristo ni kuwashirikisha injili.

Watu wengi wanajiunga na Eastern Lightning kwa sababu ya hofu. Tunapaswa kuhubiri kwamba kuwa mwaminifu kwa Imani ni muhimu kuliko hali yeyote duniani. Pia tunafahamu kwamba ufalme wa Mungu utashinda.

### Onyo Maalumu: Usiuache Ukristo wa Kihistoria

Ukristo tangu enzi za kale hata sasa umekuwa na aina mbalimbali za Imani. Hata hivyo, mafundisho ya msingi kuhusiana na asili ya Mungu na asili ya Kristo yalijengwa na kutetewa katika kipindi chote cha kanisa. Mabaraza ya awali ya kanisa yaliandika matamko ya mafundisho ya Kibiblia, na makanisa yote yanahubiri injili yamezingatia mafundisho haya kuwa ni ya muhimu na lazima. Makanisa ya kibiblia yanaonekana kuwa ya tofauti kutoka moja kwenda lingine, na hawakubaliani katika mambo mengi, lakini wanakubaliana katika mambo ya muhimu na ya msingi sana.

Baadhi ya Imani potofu zinasema kwamba makanisa yote ispokuwa la kwao si sahihi katika mafundisho ya msingi na si ya Kikristo halisi. Hawakubaliani si tu katika mambo madogo madogo bali ni katika mambo ya muhimu sana kwa ajili ya injili. Wanayakataa mambo ambayo yanayotofautisha Ukristo na dini nyingine. Imani potofu ambayo inakana mambo muhimu ya Ukristo ni dini nyingine na haitakiwi kuitwa ya Kikristo.

Wakati Imani potofu inasema kwamba iko sawa na kwamba makanisa mengine yote si sawa, tunahitaji kutambua kile wanachomaanisha. Wanasema kwamba mabaraza yote ya kanisa yaliyowakilisha makanisa yote hayakuwa sahihi. Wanasema kwamba mamilioni ya Wakristo walioishi miaka yote hawakuwa sahihi. Wanasema kwamba wanaume na wanawake wote ulimwenguni kote wanaompenda Mungu, wanaoomba, kumwabudu, wanaoshuhudia neema ya Mungu, wanaoteswa, wanaofuata Biblia, na kushirikisha Injili ni waongo. Imani potofu inasema kwamba hawa ni waongo hata katika kweli ya msingi ambayo inamfanya mtu Mkristo.

Imani potofu wako sawa, Mungu hakuchagua kuliongoza kanisa lake katika kweli ya msingi kwa karne nyingi. Endapo Imani potofu wako sawa, ni ajabu kwamba, watu wa kweli, wanaompenda Mungu kila mahali wanayakataa mafundisho yao. Ni kweli kwamba taasisi za kidini zinaweza kuwa za kiulimwengu, zenye nguvu, na tajiri na zisiwe na shahuku ya injili, lakini wanaompenda Mungu na watu wa kiroho kanisani kila mahali wanashikilia kweli muhimu ya masingi ya Biblia.

## Ushuhuda

Lia alijiunga na Imani potofu ya Eastern Lightning kwa sababu alifikiri ni Wakristo, lakini punde akagundua kwamba hawakuwa wakiamini Biblia au Yesu. Aliamua kuondoka, lakini walimpiga miguu yake na chuma bapa, ili kwamba asiweze kutembea. Walisema kwamba wangemuua endapo angeondoka. Baadae alitoroka kwa msaada wa Mkristo. Kwa sasa yupo kanisani anamtafuta Mungu. Bado ana ulemavu ambao umetokana na majeraha kutoka Eastern Lightning.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma 2 Timotheo 3 tena. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa mfuasi wa Eastern Lightning. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa Kila Somo

Jaribu kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Imani hii Potofu inaweza isiwepo katika nchi unayojifunzia. Kama sivyo, wasilisha nyenzo kwa mtu mwingine na upate mwitikio wao. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 7
# Imani Potofu za Kiapokaliptiki (Nyakati za Mwisho)

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Peter alikuwa njiani kuelekea kanisani alipoona alama kubwa: “Siku ya Hukumu, Mei 21, 2011. Biblia imethibitisha!” Peter alifikiri angefanya nini endapo ujumbe huu ni kweli. Aliona kwamba hakukuwa na sababu ya kupeleka Watoto wake shule, au kumalizia ujenzi wa nyumba yake, au kulipa fedha alizokuwa ameazima. Alifikiri pengine angetoa fedha zake zote ili kusaidia kusambaza ujume.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Marko 13 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Ni maonyo gani ambayo Yesu anayatoa katika kifungu hiki? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Imani Potofu za Kiapokaliptiki

### Utangulizi kwa Imani Potofu za Kiapokaliptiki

Kuna mamia ya Imani Potofu za Kiapokaliptiki. Zina utofauti mkubwa na zina majina mengi tofauti tofauti. Mara nyingi zimeanzishwa na mtu ambaye hudai kuwa na ufunuo mpya kuhusiana na yajayo. Baadhi yao hudumu muda mchache tu, washirika wachache, na nyingine zinakuwa kubwa. Baadhi ya taasisi ambazo zipo katika sehemu nyingine za kozi hii zina sifa za Imani Potofu za Kiapokaliptiki. Kwa mfano, Mashahidi wa Yehova mara kadhaa wametoa unabii ili kuwahamasisha washirika wao, lakini nabii hazikutimilika.

### Kwa nini Imani Potofu za Kiapokaliptiki zipo

> “Ndio, ninaamini kwamba ulimwengu huu kama tunavyoufahamu, utafika mwisho.
> kuna wakati nilikuwa sifahamu, lakini historia yote ilikuw inapelekea katika matukio makuu ambayo kila kitu sasa kinaonekana kinapimwa kwa moto. Hii sio tafakari isiyoaminika bali ni ushuhuda wa wazi na unojirudia wa Biblia.”
>
> - Billy Graham

Watu wengi wanahisia kwamba ulimwengu umefikia katika nyakati za matatizo ambazo zitabadilisha kila kitu ambacho tumekifahamu kuwa cha kawaida. Matatizo yanaweza kuelezewa katika namna ya uchumi, ikolojia, vita, siasa, au mabadiliko ya kiutamaduni.

Vitabu vingi vya tamthiria na video nyingi zinaelezea mambo ya mwisho ya kufikirika ambayo yanatokea kupitia majanga ya kiulimwengu, au vita vya nyuklia, au kimondo kikubwa kilichoigonga dunia. Katika

Habari hizi, watu wengi duniani wameuawa, na watu waliopona wameingia katika wakati ambao maisha ni tofauti sana na kitu chochote walichokifahamu

Kwa sababu ya hofu hii na matarajio, watu wanatafuta majibu kuhusiana na namna ya kukabialiana na wakati ujao. Watu wengine wanatafuta maelezo ya kidini. Wanavutiwa na ujumbe wa Imani potofu ya kiapokaliptiki. Imani potofu ya kiapokaliptiki iinaanzishwa na mtu ambaye anadai kuwa ni nabii akiwa na mafunuo mapya. Imani Potofu za Kiapokaliptiki zinajaribu kukutana na hisia na mahitaji ya watu wa kiroho kwa kuelezea hali ya ulimwengu na kile ambacho tunatakiwa kufanya ili kujiandaa.

Imani potofu ya kiapokaliptiki zimekuwepo miaka yote. Mtume aliyetangazwa anayeitwa Montanus aliishi karne ya pili ya kanisa na alitabiri kuhusiana wa haraka wa ufalme wa Mungu na mwisho wa mfumo wa ulimwengu. Katika historia yote ya kanisa kumekuwa na watu ambao wamedai kufahamu muda ambao Kristo atarudi ili kuanzisha ufalme wake na kuwahukumu waovu. Mamilioni ya watu wamedanganywa na wamevunjika moyo.

► Ni mifano gani ya Imani Potofu za Kiapokaliptiki ambazo umeziona au umezisikia?

Viongozi wa Imani Potofu za Kiapokaliptiki hawaitikii matatizo ya wakati huu katika njia ya Kibiblia, hata kama wanadai kuwa ni Wakristo na wanatumia Biblia. Hapa chini bi baadhi ya sifa za Imani nyingi Potofu za Kiapokaliptiki.

**Sifa za Imani potofu ya kiapokaliptiki**

**(1) Huweka tarehe mahususi kwa ajili ya Utabiri wao**

Wanaweza kutabiri ujio wa pili wa Bwana.

***Yesu alisema kwamba hakuna mtu anayefahamu kuhusu kurudi kwake, ona Mathayo 24:36.***

Wanaweza kutabiri mwisho wa serikali za ulimwengu. Wanaweza kutabiri majanga ambayo yataharibu watu waovu ulimwenguni. Wanaweza kutoa muda mahususi ambapo yatatokea. Yanaposhindwa kutokea, wanasema kwamba utabiri wao ulikuwa unamaanisha kitu kingine. Wanaweza kuweka tarehe nyingine mpya. Mara nyingi wanatoa nabii ndogo ndogo nyingi ambazo pia haitimii.

***Biblia inasema kwamba kama utabiri wa mtu usipotimia, hapaswi kuaminiwa kama nabii, ona Kumbukumbu la Torati 18:22.***

**(2) Wana tafsiri mpya ya Maandiko.**

Hutoa maana mpya ya vifungu kadhaa vya maandiko ambayo hakuna hata mmoja alifikiria. Maana ni kitu ambacho hakiwezi kuthibitishwa kimaandiko yenyewe. Wanaojisema manabii hudai kwamba tafsiri ilitolewa kwake kwa ufunuo, ambayo hufanya kuwa ufunuo mpya na sio tafsiri. Huku ni kutumia Biblia vibaya kwa sababu wanasema kwamba Biblia inafundisha dhana zao, lakini kimsingi hutegemea mafunuo yao na huongeza maana kwenye Biblia ambayo hakiuwepo hapo kabla. Watu ambao huamini ujumbe ni wale ambao tayari

wameshaamua kumwamini nabii. Hawafuati mamlaka ya Biblia bali hufuata mamlaka ya kiongozi wa Imani potofu.

***Biblia inasema kwamba maandiko si kwa ajili ya mtu kutoa maana yake mwenyewe. Mungu alivuvia na kudhibiti mchakato wa uandishi ili kwamba imaanishe kile ambacho Mungu alitaka kukisema, ona 2 Petro 1:20-21.***

**(3) Huitaji matendo yasiyo ya Kikristo.**

Huitaji tabia kutoka kwa washirika wao ambazo hazikuwahi kuwa ya Kikristo. Wanaweza kuhitaji kujitenga na jamii na maisha ya kawaida. Wana mtazamo wa chuki kwa wale ambao ni maadui na hata wanaunga mkono machafuko. Wanaweza kutumia nguvu dhidi washirika wao na familia zao. Wanapoingia katika shida kwa sababu ya matendo yao, huita mateso. Wanaamini kwamba Mungu ataingilia kati kimiujiza katika kuitikia Imani yao. Baadhi ya Imani Potofu za Kiapokaliptiki zimeishia katika kujiua.

***Tito 3:1-5 inaonesha ukinzani wa tabia ambazo zinatakiwa kuwa za Kikristo na zile za wenye dhambi.***

**(4) Huwatenga washirika wao na mahusiano mengine**

Baadhi ya Imani Potofu za Kiapokaliptiki huwataka washirika wao kutoa kila kitu kwa taasisi. Washirika wanaishi pamoja katika eneo kubwa na wanatengwa na marafiki na ndugu wowote ambao hawako katika Imani potofu. Wanaweza kufundhiswa kwamba walio nje wote ni maadui. Washirika baadae kuvunjika moyo kwa sababu ushirika huwa hauna misingi katika kweli na hauwezi kuwa ushirika wa kweli wa Kikristo.

***Yesu aliomba kwamba tumo ulimwenguni lakini sisi ni tofauti na ulimwengu kama yeye alivyo, ona Yohana 17:14-16.***

► Swali hili linakuwa utangulizi wa sehemu inayofuata: Ni madhara gani yanatendwa na Imani Potofu za Kiapokaliptiki?

**Madhara ya Imani Potofu za Kiapokaliptiki**

Imani Potofu za Kiapokaliptiki zina madhara kwa namna kadhaa.

1. Huwavuta watu kutoka Makanisa ya Kikristo kuja katika mafundisho ya uongo.
2. Huwavunja moyo washirika wao na kuwasababisha kupoteza Imani kabisa.
3. Hudai kuwa Wakristo, lakini huwa na tabia zisizo za kikristo ambazo huharibu sifa ya Ukristo.
4. Husababisha watu kutilia shaka maandiko kuhusiana na ufalme wa Mungu na Ujio wa Kristo.

**Mwitikio wa Wakristo kuhusiana na Machafuko ya Ulimwengu**

> "Yesu atakuja tena kuwahukumu watu walio hai na waliokufa: ambaye ufalme wake hautakuwa na mwisho."
>
> - Imani ya Mitume

Biblia inazungumzia nyakati kama hizi. Maandiko kama kitabu cha Danieli na kitabu cha Ufunuo wa Yohana viliandikwa katika nyakati za yajayo yasiyojulikana, ghasia katika jamii, vita vya kimataifa, na mateso makali. Zilikuwa ni nyakati ambazo zilijaribu Imani ya watu ambao wanamwamini Mungu. Ilionekana kwamba hatuwezi kudhibiti chochote na kwamba kila kitu kizuri kinaweza kuwa kimeharibiwa.

Dhana kuu ya maandiko ya kinaabii ni kwamba Mungu anatawala na hatimaye ataanzisha ufalme wake na kuwalipa wenye haki.[16] Biblia inathibitisha kwamba nyakati hizo zitakuwa ngumu na uovu utaonekana kutawala wa muda. Waamini wanaitwa kushikilia Imani yao katika Mungu na kuishi kwa uaminifu pasipo kuangalia hali ya ulimwengu. Kama vile maandiko hayo yalivyotumika nyakati hizo, ndivyo ambavyo yanatumika pia nyakati zozote wakati ambapo Imani inajaribiwa.

Kitabu cha 2 Wathesalonike kiliandikwa kwa Wakristo ambao walikuwa wanategemea kurudi kwa Yesu na siku ya hukumu ya Mungu kutokea upesi. Walikuwa wanasikia kwa watu ambao walidai kwamba matukio hayo yamekwisha kutokea (2 Wathesalonike 2:2). Walichanganyikiwa kuhusiana na kile walichotakiwa kukifanya.

Mtume Paulo anaelezea baadhi ya matukio ambayo yatatokea muda mfupi kabla ya kurudi kwa Kristo, yakiwemo kutawala kwa mtu anayeitwa "yule mtu wa kuasi" na "mwana wa uharibifu" (2 Wathesalonike 2:3).

Kilicho muhimu zaidi kwetu sisi ni kuona kwamba Paulo anahitimisha maelekezo kwa waamini katika 2 Wathesalonike 2:15-17. Anawaambia wao kusimama na kuendelea kufuata yale ambayo wamekuwa wakifundishwa. Hawakutakiwa kuacha kanuni za msingi za maisha ya Kikristo kwa sababu ya matukio yeyote ambayo yalikuwa yanakuja. Katika mstari wa 17 anaomba kwamba Mungu awasimamishe au awategemeze katika kila kazi njema

Hata kama mwisho wa ulimwengu uko karibu, si wakati wa sisi kuacha misingi ya maisha ya Kikristo. Mambo ambayo wakati wote wamekuwa muhimu yatakuwa muhimu wakati wote hata mwisho. Tunatakiwa tuwahubirie waliopotea, kushikilia mafundisho ya kweli, kuishi Maisha matakatifu, mahusiano na waamini, kuwatendea wengine mema, na kuonesha upendo kwa watu wote.

► Ni mambo gani muhimu ya kukumbuka kama tunataka kuishi nyakati za kiapokaliptiki (nyakati za mwisho)?

---

[16] Danieli 2:44, Danieli 4:34, Danieli 6:26, Danieli 7:27, Ufunuo 1:7, Ufunuo 6:15-17, Ufunuo 11:15, Ufunuo 17:14, Ufunuo 19:11-21.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa*****.**

## Uinjilisti

Kipaumbele cha kwanza wakati unazungumza na mfuasi wa Imani potofu ni kuhakikisha kwamba anaelewa injili kwa usahihi. Unaweza ukadhania kwamba mfuasi wa Imani potofu anaamini mafundisho ya Ukristo na ameongeza tu baadhi ya nabii za kipekee, lakini mara nyingi Imani potofu zinaweza kuwa zimeenda kinyume au kukana mafundisho muhimu.

Hatua inayofuata ni muhimu kuonesha ni kwa jinsi gani Imani potofu imekwenda mbali na Ukristo wa Kihistoria. Onesha matendo ambayo yasingelikubaliwa katika Ukristo wa Kihistoria (wa mitume). Onesha matendo ambayo yasingelikubaliwa na watu wa Mungu wa kanisa katika karne zote.

Onesha kwamba Mathayo 24:36 inatueleza sisi kwamba siku ya kuja kwa Kristo haijafunuliwa.

Onesha kwamba tafsiri yao ya nabii za kimaandiko zina msingi katika Imani kwa kiongozi wao tu na si katika kanuni za kawaida za kutafsiri.

Onesha kwamba Kumbukumbu la Torati 18:22 linatuambia sisi kwamba mtu hataaminika kuwa nabii endapo mojawapo ya unabii wake ni wa uongo.

## Ushuhuda

Dorcas alilelewa katika familia ya Mashaidi wa Yehova. Akiwa mtoto aliamini mafundisho ya Jengo la Ufalme yalitoka moja kwa moja kwa Mungu. Siku moja usiku, viongozi waliitisha kikao maalumu. Walitangaza kwamba Har-Magedoni ingetokea mwaka 1975. Hiyo ilikuwa ni miaka saba baadae. Dorcas alilia sana usiku ule kwa hofu kwamba nini kitatokea kwa familia yake Har-Magedoni ikifika. Kwa miaka michache baade familia yake na wengine walifanya kazi kubwa sana kwa ajili ya Imani potofu. Waliamini kwamba si muda mrefu umebakia. Gazeti la Imani potofu lilichapisha picha za Watoto, watu wazima, na wazee wakiharibiwa na Har-Magedoni. Siku ya mwisho ya mwaka 1975, watu wengi walikwenda vitandani mwao kulala wakitegemea mwisho utafika usiku ule. Dorcas aliamka asubuhi iliyofuata na alishangaa kuona kila kitu kilikuwa kama kilivyokuwa. Wazazi wake hawakuongea kuhusiana na unabii tena. Dorcas aliacha kwenda katika mikutano ya Imani potofu tena, lakini hakufahamu ni wapi pa kupata ukweli. Miaka mingi baade Dorcas alikutana na mtu ambaye alimuelezea wokovu, na akaokoka.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Marko 13 tena. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ili kuelezea ujumbe wa kifungu hiki cha maandiko kwa mfuasi wa Imani potofu ya Kiapokaliptiki. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

**Zoezi kwa Kila Somo**

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 8
# Uhindu

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Amit alilelewa katika familia ya Uhindu na alishiriki katika taratibu zote za kidini. Akiwa mtoto aliomba kila siku. Alikuwa amedhamiria lakini alisikia utupu wa kiroho. Amit alisoma maandiko ya Kihindu ili kujitahidi kuelewa dini yake vema. Aliambiwa kwamba haijalishi ni Imani gani kwa sababu dini zote zinatupeleka kwa Mungu. Alitaka kutafuta ukweli halisi ambao utamwongoza Yeye kwa Mungu, lakini alijiuliza kama kweli hiyo kweli ipo.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Isaya 46 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Ni tofauti gani ambayo kifungu hiki cha andiko kinatoa kati ya Mungu na sanamu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Uhindu

### Utangulizi kwa Uhindu

Dini ya Uhindu ilianza huko India mapema sana kabla historia yeyote haijabaini. Uhindu hauna mwanzilishi wa kibinafsi na utaratibu ambao ni kwa kila mfuasi. Kuna Wahindu, zaidi ya Bilioni moja[17] lakini wana Imani zinazotofautiana sana. Wahindu wengi hujishughulisha na baadhi tu ya taratibu za dini ya Kihindu.

> "Wazo kwamba Mungu ana hekina isiyo na kikomo ni msingi wa kweli zote. Ni kipengere cha Imani ambacho ni muhimu kwa ajili ya mafundisho yote sahihi kuhusu Mungu."
>
> - Imechukuliwa kutoka A.W. Tozer *The Knowledge of the Holy*

Wahindu wanaamini kwamba dini yao inatokana na maandishi ya kale ya kihindi yanayoitwa Vedas. *Vedas* imeundwa kwa mamia ya matoleo.

Hakuna tamko la mafundisho ambayo yanawakilisha Imani ya kiujumla kwa wote ya Uhindu kuhusu Mungu. Wahindu wengi wanaamini juu ya miungu wengi ambao ni nafsi na wanatenda vyote viwili ubaya na wema. Wahindu wanatumia sanamu au vinyago vingi kuwakilisha miungu na roho ambazo wanaziabudu.

***Yesu alisema tunapaswa kumuabudu Mungu mmoja wa Kweli, ona Luka 4:8.***

Baadhi ya Wahindu wanamuabudu mungu mmoja kama mkuu. Baadhi ya Wahindu wanamwita mungu mkuu *Shiva*; Wahindu wengine wana majina mengine yanayomwelezea

[17] "Religion: Hinduism," Joshua Project, https://joshuaproject.net/religions/5, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

mungu wao mkuu. *Shiva* ana mke na watoto. *Shiva* anafanya yote mema na maovu. Baadhi wanamwita *Shiva* muumbaji, lakini hawamaanishi kwamba ulimwengu uliumbwa wakati fulani mahususi.


> "Nina mwamini Mungu Baba Mwenyezi, muumba mbingu na dunia."
>
> - Imani ya Mitume

Hata wakati Wahindu wanazungumza kuhusu mungu wao mkuu, hawamaanishi sawasawa na kile ambacho Wakristo wanamaanisha wanapomrejelea Mungu. Wakristo wanaamini kwamba Mungu ndiye uhalisia mkuu na muumbaji binafsi wa ulimwengu. Wahindu wanasema kwamba wanaamini katika mungu mmoja, lakini si mungu ambaye anazungumza na kufukiri, ispokuwa kupitia miungu tofauti tofauti ambao wamechukua namna ya kimwili.

***Nabii Yeremia alisema kwamba Mungu aliumba kwa nguvu zake, na miungu yote ya uongo inaangamia, ona Yeremia 10:9-12. Mungu anawasiliana na watu na anatuambia sisi Yeye ni nani, ona Isaya 46:9-10.***

Wahindu wanaamini kwamba kuna uhalisia mkuu usio na nafsi ambao ulitengeneza dunia. Baadi ya Wahindu wanaitwa uhalisia huu Brahman. Wanaamini kwamba kila kitu kinaishi kama sehemu ya Brahman. Wanaamini kwamba Brahman ni nafsi au kitu muhimu katika kila kitu kinachoishi. Wanaweza kusema kwamba wanaamini juu ya mungu mmoja, lakini wanamaanisha ni kwamba kila kitu kinachoishi ni kimoja, na ni mungu.

***Mwanzo 1 inasema kwamba Mungu aliumba kila kitu kwa agizo lake. Yeye ni tofauti na vitu alivyoviumba, ona Mwanzo 1:1.***



Wahindu wanaamini kwamba kiongozi yeyote mkubwa anayewafaidisha watu baadaye anaweza kuwa mungu. Kila mtu ni udhihirisho wa Brahman, lakini mungu ni nafsi ambayo inamdhihirisha Brahman Zaidi kuliko wengine.[18]

► Nini ni baadhi ya tofauti kati ya dhana ya Ukristo na Uhindu kuhusu Mungu?

Wahindu wanadai kuwa wavumilivu kuliko dini zingine. Wana msemo unasema kwamba "Kweli zote ni moja." Wanasema kwamba zipo njia nyingi kufikia lengo, hata kama dini tofauti tofauti zina dhana tofauti tofauti ya Maisha ambayo mtu anapaswa aishi na lengo ambalo anatakiwa kujaribu kulifikia. Hawamaanishi kwamba "kweli zote ni moja" katika namna ambayo dini nyingine mbalimbali zinaelekeana au zinategemeana kidhana. Wanamaanisha kwamba kweli zote ni maonesho ya kweli kuu ambayo haiwezi kuwekwa katika maelezo.

***Mtume Paulo anasema wajibu wa msingi wa mchungaji ni kufundisha fundisho la kweli, ona Tito 1:9. Dini zote si sasawasa, ona 1 Timotheo 1:3-6.***

---

[18] Picha na Ganesh Chaturti kutoka Unsplash, ilitafutwa tena kutoka https://unsplash.com/photos/Mawa0oZ3YKs.

Wakristo wanaamini kwamba hata kama Mungu ni mkuu kuliko tunavyoweza kuelewa, amefunua baadhi ya maelezo ya kweli kuhusiana na Yeye. Endapo dini inakinzana na kweli ambayo Mungu ameifunua kuhusiana na Yeye, dini hiyo si sahihi.

Baadhi ya Wahindu wanaamini kwamba Yesu alikuwa mtu ambaye alitendea kazi kanuni za Uhindu na alikuwa mwalimu mkuu kama wengine ambao wameishi katika nyakati nyingine. Hawaamini kwamba Yeye ni mwana pekee wa Mungu.

Wahindu wanaamini katika mzunguko usiokoma wa muda, usio na mwanzo, usio na mwisho, na hakuna matukio yanayobadilisha mambo kwa namna ya kudumu,

Wahindu juu ya kuzaliwa tena na tena au umwilisho. Wanaamini katika kuzaliwa tena kwa nafsi ya msingi ya mtu binafsi katika namna nyingine ya Maisha, mara nyingi.

***Biblia inasema kwamba watu wanakufa mara moja na kwenda katika hukumu mbele za Mungu, ona Waebrania 9:27.***

Wahindu wanaamini juu ya karma. Kulingana na dhana ya karma, mtu anapokea matokeo mazuri au mabaya kwa ajili ya matendo yake katika Maisha haya na yajayo. Karma ni sheria ya asili ya ulimwengu, na si katika msingi uliowekwa na mungu yeyote, na haudhibitiwi na mungu yeyote.

> "Imani ya Kikristo juu ya mwanadamu, thamani isiyo na kikomo ya mwanadamu, na faida yenye thamani kubwa ambayo inatambuliwa kupitia neema ya Mungu iokoayo."
>
> - W.T. Purkiser
> *Exploring Our Christian Faith*

***Wakristo wanatii sheria za Mungu na wana mahusiano ya kibinafsi na Mungu, ona Yohana 14:15. Biblia inatuambia kwamba kristo atawahukumu watu wote kwa viwango vyake vya haki, ona Matendo ya Mitume 17:31, 2 Wakorintho 5:10, Yakobo 4:12.***

Mtu ni mwenye hatia endapo anafanya kitu ambacho ni hatari kwake au kwa wengine. Anaweza kuweka uwiano wa matendo mabaya kwa matendo mema ili kupata matokeo mazuri. Lakini, hakuna msamaha.

Lengo kuu la Uhindu ni kutafuta kuachiliwa kutoka katika mzunguko wa kuzaliwa tena na tena katika hali ya milele inayoitwa nirvana. Baadhi ya Uhindu unafafanua hali hii kama nafsi kuishi katika hali ya umilele, wakati wengine wanaona kuwa ni hali ya kufyozwa ndani ya Brahman, kama tone la maji linavyodondoka baharini. Wahindu wengi wanaamini kwamba mtu hukoma kuishi kama mtu mwenye ufahamu anapofonzwa ndani ya Brahman.

***Lengo la Wakristo ni kuishi milele katika mahusiano ya kibinafsi na Mungu huko mbinguni, ona Ufunuo 21:3.***

► Ni tofauti gani kati ya dhana ya Uhindu ya nirvana na dhana ya ukristo ya mbinguni?

**Mtindo wa Maisha wa Kihindu**

Kutokana na Imani ya Uhindu, wale walioukana ulimwengu hawatakiwi kutengeneza, kuandaa, au kutunza vyakula. Wanapaswa kuomba omba chakula chao kila siku. Baadhi yao huwategemea ndugu zao; wengine huenda nyumba kwa nyumba kuomba omba. Mfano mzuri wa mfuasi wa Uhindu hafanyi kazi ili kujihudumia wenyewe.

***Biblia inasema kwamba mtu hapaswi kutegemea wengine na akakataa kufanya kazi, ona 2 Wathesalonike 3:10.***

Wahindu wengi ni wala mboga mboga. Miongozi mwa wale wanaokula nyama, wengi wao hawali ngo'ombe kwa sababu ng'ombe anataukuzwa. Mara nyingi chakula kinatolewa sadaka kwa sanamu kabla hakijaliwa, hata kama ni nyumbani.

***Biblia inasema kwamba nyama zote zinaweza kuliwa, ona 1 Timotheo 4:3-4.***

Wahindu wana mahekalu yanayojieleza na yenye muundo mzuri, mavazi, na mapambo binafsi yenye umuhimu wa kidini.

Wahindu wanaamini kwamba wanatakiwa kujali kila namna ya uhai. Wanaamini kwamba mtu anapaswa amjali mbwa anayeteseka katika namna ambayo atamjali kijana wake. Wanaamini kwamba hakuna mahusiano yatakayomfanya mtu kuwa na hisia kuhusiana na hitaji la mwingine. Wanaamini kwamba kumjali mtu mwingine kwa sababu ya mahusiano ni dhamira isiyo sahihi. Wanaamini kwamba Brahman hana hisia juu ya kitu chochote, hana huzuni na hana furaha. Mhindu anapaswa kujaribu kufikia hatua hiyo.

Wakati Wahindu wanazungumza kuhusiana kumjali kila mtu sawasawa, wanaonekana kana kwamba wana dhana sawa sawa na Wakristo. Kimsingi, si sawa kabisa. Wakristo wanaamini kwamba wanapaswa kuwapenda wengine sawasawa na wanavyojipenda wenyewe. Wahindu wanaamini kwamba haupaswi kujijali mwenyewe au kuwajali wengine.

Kwa Uhindu, kutafakari kunamaanisha kudhibiti kabisa akili yako. Ili kwamba mawazo yasiweze kuja pasipo ruhusa yako. Ibada zao zimetengenezwa kwa namna ya kuweka wazi akili zao. Ndiyo maana wanatumia sauti za kujirudia rudia na maneno na mazoezi. Kusudi la kutafakari ni kutofikiri kuhusu chochote. Yoga ilianza kama mfumo wa Uhindu wa mazoezi kwa ajili ya kusafidha akili.

Wahindu wanaomba kwa miungu kama njia ya kuweka umakini katika akili zao. Endapo Mhindu atapata umakini kamili, hataihitaji miungu na hatahitaji kuomba. Hawaombi moja kwa moja kwa Brahman.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Uinjilisti

Kwa sababu Wahindu hawaamini Biblia, kutumia andiko ili kukanusha Imani zao hakutabadilisha akili zao. Badala yake, wasilisha injili kwa namna ambayo inagusa mahitaji

yao. Ushuhuda binafsi wa Mkristo wa mahusiano na Mungu utasaidia kumgusa hitaji la Mhindu la kumjua Mungu.

Mungu, muumbaji na mtegemezaji wa ulimwengu, ni nafsi ambayo inafikiri na kuzungumza, tofauti na Brahman wa Uhindu.

Mungu ni mwenye haki na mwenye upendo, hakuna uovu katika asili yake. Anaweza kuaminika, tofauti na miungu ya Kihindu ambayo ina nia za kibinafsi na mgongano katika tabia zao.

Mungu anampenda mwanadamu na alituumba sisi kwa kusudi la kuishi katika mahusiano na Yeye. Ana muundo kwa ajili yetu na ana makusudi kwa ajili ya maisha yetu ili sisi tuishi mbinguni pamoja naye milele. Kila mmoja wetu anaweza kumfahamu Mungu kibinafsi kama Baba.

Watu kibinafsi wanatengwa na Mungu kwa sababu wametenda dhambi dhidi ya mapenzi yake. Kila mmoja atahukumiwa na Mungu kwa dhambi yake. Hii ni tofauti na dhana ya Uhindu ya karma ambayo si nafsi bali ni nguvu inayotenda kazi kama asili.

Yesu alikuja kama Mungu aliyevaa mwili ili kufa kama sadaka ili kwamba dhambi zetu zisamehewe. Kila mtu anaweza kuja katika mahusiano na Mungu katika msamaha kwa msingi wa sadaka ya Yesu.

Kupitia msamaha tunakuja katika mahusiano ya kibinafsi na Mungu ambaye anatupenda sisi na ameahidi kutuasili sisi kama Watoto wake, badala ya kuabudu miungu iliyo mbali na isiyojali ambayo haijaahidi chochote kwetu.

## Ushuhuda

Amit alipokutana na Mkristo, alikwazwa na dhana kwamba kuna njia moja tu ya kufika kwa Mungu. Aliposoma mifano ya Yesu kwenye Biblia, alishangazwa na namna ambavyo inaweza kutendewa kazi katika maisha yake. Alipokuwa anafanya utafiti kuhusiana na usahihi wa Biblia, aliamini kwamba Biblia ilikuwa imetunzwa vizuri kutoka katika maandiko ya halisi ya kwanza. Siku moja aliona mkanda wa video kuhusiana na mateso ya Yesu na alifanya maamuzi ya kuweka Imani yake kwa Kristo. Amit alisema, "Endapo Ukristo ni kama tu moja ya dini nyingi zinazokubalika, basi sadaka niliyoitoa, ikiwemo kupoteza amani ya familia yangu, ni bure. Nilijisikia vizuri katika Imani yangi ya Uhindu na nilifurahia maisha ya maombi; nilijisikia utupu na nilikuwa msumbufu nikiukataa wito wa Mungu kutoka kanisani. Ilikuwa ni kweli na upendo ambao ulinisukuma mimi kumkubali Kristo kama Bwana."

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Isaya 46 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha Andiko kwa ajili ya Uhindu. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

**Zoezi kwa Kila Somo**

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 9
# Ubudha

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Yeo alikulia katika familia ya Kibudha huko Ufilipino. Alikumbuka wakati ambapo haikuwa salama kwenda sokoni kwa sababu Waislamu walikuwa wanawaua Wabudha kwa sababu ya dini yao. Wakati mwingine Yeo alikwenda na mama yake katika hekalu la Kibudha ili kuchoma uvumba. Siku moja dada yake alikuwa anaumwa na alikuwa anakufa. Madaktari walikuwepo lakini hawakuweza kusadia. Mama yake na Yeo aliomba sana bila kukoma ili Buddha amsaidie.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Mwanzo 3 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha Maandiko kinatuambia nini kuhusu Mungu, mwanadamu, dhambi, na Ulimwengu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Ubudha

### Asili ya Ubudha

Ubudha ulianzishwa na Siddhartha Gautama. Hakuna kilichoandikwa kuhusiana na maisha ya Siddhartha Gautama hadi miaka 400 baada ya kifo chake, kwa hiyo habari za maisha yake hazina uhakika.

Gautama alizaliwa mnao mwaka 563 K.K. Alikuwa mwana wa mfalme wa sehemu ndogo ya India. Akiwa kijana aliwatoroka wanaomtunza ili kwenda kuuona ulimwengu. Aliwaona watu katika umaskini na magonjwa, na akahitimisha kwamba kimsingi maisha ni huzuni na mateso.

Gautama alipata uzoefu ambao alisema ulimuangazia yeye kuhusiana na asili ya uhalisia. Neno *Buddha* linamaanisha “aliyeangaziwa.” Gautama mara nyingi anaitwa “Buddha.”

***Biblia inatueleza sisi tusiamini ujumbe kutoka kwa roho ambayo haitambui Yesu Kristo, ona 1 Yohana 4:3. Kuangaziwa ambako Gautama alikupokea kulikuwa ni uongo.***

### Ushawishi wa Sasa

Leo hii kuna makundi mengi ya Ubudha. Hawajaungana katika taasisi ya kiulimwengu.

Maandiko yanayochukuliwa na Wabudha kuwa matakatifu yanaweza kujaza maelfu ya matoleo. Kwa hiyo, kila kundi hujikita katika kadhaa, kuliko kujaribu kusoma yote.

► Ni kwa namna gani ambayo Wakristo wanaiangalia Biblia tofauti na njia ambayo Mbudha anayaangalia maandiko yake?

Idadi ya wanaoukiri Ubudha duniani ambao kwa makusudi kabisa wanafuata mafundisho ya Ubudha ni angalau milioni 350. Zaidi ya watu billion wanaweza kujiita wabudha kwa sababu tu wamekuwa wanafundishwa Ubudha, na hawajajikita katika dini nyingine yeyote tofauti.

Watu wengi wanajiita wao wenyewe Wabudha kwa sababu wanafuata baadhi ya ushauri wa maandiko ya Kibudha. Wanaweza wasielewe mafundisho ya msingi ya Ubudha na wala wasishiriki katika makundi yaliyopangwa.

**Imani kuhusu Uungu na Muda**

Wabudha hawaamini juu ya Mungu Mkuu ambaye ni nafsi. Badala yake, wanaamini katika uhalisia mkuu ambao ni jumla ya kila kitu kinachoishi. Kwa hiyo, Wabudha hutafakari, lakini hawaombi, kwa sababu hawaamini kwamba kuna Mungu anayezungumza na kusikiliza. Wabudha wana maandiko yanayoitwa maombi, lakini hawayaelekezi kwa mtu yeyote. Hakuma miungu ya aina yeyote ambayo ni muhimu katika Ubudha.

"Mungu kweli yupo huko. Yuko huko kama ambavyo yupo hapa na kila mahali, hafungwi katika mti au jiwe, bali huru katika ulimwengu, karibu na kila kitu, pembeni ya kila mtu, na kupitia Yesu Kristo anapatikana kwa kila moyo."

- A.W. Tozer
*The Knowledge of the Holy*

***Ni heshima kubwa kwa Wakristo kuomba kwa ujasiri kwa Mungu anayesikia, ona Mathayo 6:6-8 na 1 Yohana 5:14-15.***

Wabudha wanaamini katika mzunguko usioisha wa muda, usio na mwanzo, usio na mwisho, na hakuna tukio ambalo linaleta mabadiliko ya kudumu.

***Biblia inasema kuna matukio makuu, na kwamba mara zote muda hautaendelea kama ilivyo sasa, ona 2 Petro 3:10.***

**Kuzaliwa tena na Nirvana**

Gautama na watu wengi wa utamaduni wake walikuwa tayari wanaamini juu ya kuzaliwa tena kabla hata ya kuanzisha dini yake. Kuzaliwa tena kunamaanisha kwamba baada ya mtu kufa anazaliwa tena kama mtu mwingine au kiumbe mwingine kama vile mnyama au mdudu. Kwa kuzaliwa tena, mtu anaishi maisha mengi.

Wabudha wanaamini kwamba endapo mtu atafanya matendo mema (karma njema) yakazidi matendo yake mabaya (karma mbaya), anaweza kuzaliwa katika maisha mazuri wakati ujao.

"Katika kurasa zake za kwanza, Biblia imekataa vyote filosofia ya pantheism (mafundisho kwamba Mungu na ulimwengu wako sawasawa) na deism (nadharia kwamba Mungu alianzisha ulimwengu na baada ya hapo akauacha ujiendeshe wenyewe kwa sheria zisizo za kinafsi). Mungu hafananishwi na uumbaji wake. Ni uumbaji wake. Kwa upande mwingine ulimwengu usingeweza kutokea pasipo nguvu ya uumbaji na utunzaji wa Mungu."

- W.T. Purkiser
*God, Man, and Salvation*

***Biblia inasema kwamba matendo yetu hayatufanyi kukubaliwa na Mungu au kulipa kwa ajili ya dhambi zetu, ona Warumi 3:20.***

Kulingana na Gautama, dhamiri ya nafsi ya mtu haizaliwi tena. Ni nyenzo chache tu alizotengenezewa ndizo zinatumika kutengeneza kiumbe mwingine. Hii inamaanisha kwamba kifo katika Maisha ya awali kimsingi ni mwisho wa nafsi hiyo.

***Yesu hutoa uzima wa milele kwa wale ambao wanamuamini, ona Yohana 10:27-28.***

Wakati mwingine watu hupenda dhana ya kuzaliwa tena, lakini kwa sababu maisha ni mateso, Gautama alihisi kwamba kuishi maisha mengi si jambo jema. Aliamini kwamba mtu anapaswa awe na lengo la kuepuka mzunguko usioisha wa kuzaliwa tena na tena.

Mbudha mwenye msimamo hujikita katika njia za Kibudha za Maisha ili kuondoa matamanio yote. Endapo akafanikiwa, hatatamani au kufurahia kitu chochote au mahusiano yeyote.

> "Ninamwamini... Bwana mmoja Yesu Kristo... kupitia Yeye vitu vyote viliumbwa, ambaye kwa ajili yetu sisi wanadamu na kwa ajili ya wokovu wetu alikuja kutoka mbinguni... na akafanyika mwanadamu na akasulubiwa kwa ajili yetu."
>
> - Imani ya Nikea

***Kwa Wakristo, mahusiano ya wanadamu ni muhimu na yanaleta furaha, ona 1 Wathesalonike 3:12.***

Mbudha anaamini kwamba akifa, ataingia katika nirvana badala ya kuzaliwa tena kama kiumbe mwingine. Hili ni lengo kuu la wote waliojikita katika Ubudha. Wakati mwingine watu hudhani kwamba nirvana ni kama dhana ya Wakristo ya mbinguni. Lakini nirvana inamaanisha hali ya kutokuwa chochote, mwisho wa nafsi, kama kupuliza mshumaa. Endapo mtu atafikia nirvana, haishi tena kama mtu anayefikiria.

Katika Ubudha, wa asili, mtu hakuwa na uwezo wa kufikia nirvana mwishoni mwa maisha yake ya sasa ispokuwa alikuwa mtawa Kibudha. Mwanamke hakuwa na uwezo kabisa kufikia nirvana hadi akizaliwa tena kama mwanaume na kuwa mtawa.

### Kweli Nne za Kimaadili za Ubudha

Imani ambazo Gautama alifundisha baada ya kuangaziwa zimefupishwa katika Kweli Nne za Kimaadili za Ubudha.

1. Maisha yamejaa huzuni na mateso na hayana furaha ya kweli.
2. Mateso ni matokeo ya matamanio, kwa sababu hakuna kitu tunachotamani kitadumu.
3. Kujiondoa kutoka katika tamaa zote ni njia ya kuepuka mateso.
4. Kanuni nane za maadili ya Ubudha kwa ajili ya maisha humchukua mtu kuelekea kujiondoa kutokana na matamanio yote na nirvana.

► Je, kuna kitu chochote katika kweli nne ambazo Wakristo wanaweza kukubaliana nazo?

Kulingana na Gautama, mateso yote yanakuja kwa sababu ya matamanio. Kama mtu hatatamani kitu chochote, hatateseka. Ili kujikita kuwa Mbudha, mtu hatakiwi kupendezwa na chochote.

Habari inaelezwa ya mtawa mmoja wa kibudha aliyeitwa Sangamaji. Alikuwa mtawa na akaiacha familia yake ili kutumia muda wake akizunguka na kutafakari. Mke wake alipompata, alimlaza mtoto wake mbele yake, na akamuomba awasaidie. Sangamaji aliketi bila kujibu chochote hadi mke wake akaondoka. Gautama akasema kwamba mwanaume huyu alikuwa amefikia lengo la Ubudha kwa sababu hakuhisi furaha yeyote mke wake alipokuja au huzuni yeyote alipoondoka.

***Wakristo wanaingia katika ndoa kama mahusiano ambayo yanaleta furaha, ona*** Waefeso ***5:28.***

► Ni kwa namna gani dhana ya Ubudha ya maisha kamilifu inatofautiana na dhana ya Ukristo?

**Mtindo wa Maisha wa Ubudha**



Ubudha unasisitiza maisha ya uadilifu. Wabudha wanaamini kwamba tendo linaweza jema au la maadili kama linakufaidisha wewe na wengine, na halimdhuru mwingine. Nia ya mtu inachukuliwa kuwa muhimu zaidi kama matokeo halisi ya matendo yake.

Mazoezi ya kiakili na ya kiroho ambayo Wabudha wanayafanya yametengenezwa ili kumsaidia mtu kutoka katika ubinafsi. Wabudha wanaamini kwamba masumbufu yote yanakuja kutokana na kujijali kulikopitiliza. Wanataka kusahau nafsi na kupenda viumbe wote wenye ufahamu (viumbe wenye akili). Tatizo ni kwamba pasipo uhusiano na Mungu, hakuna msingi wa kujitoa na upendo.[19]

► Kwa nini mtu hawezi kuwa mwenye kujitoa na mwenye upendo pasipo mahusiano na Mungu?

Watu wengi wanaojiita Wabudha wamekulia katika utamaduni wa Ubudha na hawajawahi kuangalia kingine kwa umakini. Nadharia za dini yao ndizo zinaonekana halisi pekee kwao. Taratibu zao za ibada ni sehemu ya maisha yao.

Kwa kawaida, watu wanaojiunga Ubudha kutoka katika dini nyingine wanavutiwa na filosofia yao ya maisha. Hawajiungi kwa sababu wanatafuta nirvana. Wanajiunga kwa sababu Ubudha unaonekana kutoa maisha ambayo yako huru kutokana na masumbufu na

[19] Picha na Honey Kochphon Onshawee kutoka Pixabay, ilichikuliwa tena kutoka https://pixabay.com/photos/buddhists-monks-meditate-thailand-453393/.

mgogoro. Watu wengi wanahisi kwamba katika Ubudha wanapata uhuru kutokana na mgandamizo na kwamba maisha yao yanakuwa katika mpangilio.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Uinjilisti/Kutumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

Kwa sababu Wabudha hawakiri kuwa Wakristo na hawaitambui Biblia kama mamlaka ya mwisho, haitoshi kuwaonesha kwamba Imani yao si sawasawa na Biblia. Tayari wanafahamu kwamba Biblia inasaidia au kuunga mkono dini tofauti na yao.

Ni muhimu na yenye ufanisi kushirikisha injili. Unapozungumza na Mbudha, mwambie unataka kumuelezea misingi ya Imani yako. Shirikisha injili kwa urahisi. Hata kama Mbudha hadai kuamini Biblia, kweli ya Mungu ina nguvu kwa sababu ya kazi ya Roho Mtakatifu.

Unapaswa pia kushirikisha ushuhuda wako. Mwambie namna ambavyo injili imekuleta katika uhusiano na Mungu, imekuletea msamaha na ukombozi kutoka dhambini, na kuwa maisha yako maana.

Zaidi ya misingi ya kuwasilisha injili na ushuhuda binafsi, unaweza kuzungumzia hitaji maalumu la Mbudha kwa kutumia kweli ya injili. Ubudha unang'ang'ana kuelezea mateso na huzuni za maisha. Unashindwa kuelezea uhalisia wa mambo mazuri na furaha iliyopo. Mafundisho ya ubudha yanakana umuhimu wa kitu chochote kinachionekana kuwa ni muhimu katika maisha, yakiwemo mahusiano ya wanadamu. Ni dini pasipo Mungu ambaye ana mahusiano na wanaomwabudu. Haitoi uzima wa milele au umuhimu wa hatma ya mwanadamu.

### Mateso

Mbudha anaamini kwamba mateso hayana maana na si halisi. Haya ni maelezo yasiyojitosheleza.

Ukristo unaeleza hali ya mateso katika ulimwengu. Ulimwengu uliumbwa na Mungu ukiwa kamilifu, lakini mwanadamu alifanya dhambi na akaleta laana juu ya ulimwengu. Hii inaelezea kwa nini kuna uzee, magonjwa, na kifo. Dhambi pia inaonekana katika matendo maovu ya watu yanayoendelea.

### Furaha

Mbudha anaamini kwamba hakuna furaha ya kweli katika maisha, na kwa hivyo hatupaswi kutamani kitu chochote. Hii inakinzana na uzoefu wa furaha na raha ambao watu wanao, hasa katika mahusiano ya kibinafsi.

Ukweli kwamba ulimwengu uliumbwa na Mungu unaelezea kwa nini kuna furaha tele na raha katika maisha, hata kama ulimwengu si kamilifu kama ambavyo Mungu aliukusidia hapo awali.

Kama Wabudha, Wakristo wanaamini kwamba mambo ya duniani si ya kudumu. Tusiishi kana kwamba tutavitunza vile tulivyonavyo milele. Hata hivyo, mkristo anaweza kufurahia maisha kwa sababu anafahamu kwamba ataishi milele na Mungu. Hata kama vitu si vya kudumu, ni halisi, na uchaguzi wetu una matokeo ya milele. Hii inatoa kusudi na umuhimu kwa maisha ya mwanadamu.

**Mahusiano na Wengine**

Kama ukiyaishi kikamilifu, mafundisho ya Ubudha yatakupeleka mbali na mahusiano kwa sababu mahusiano yanachukuliwa kuwa yasiyo na maana. Lakini asili ya mwanadamu ina hitaji la ndani sana la kujikita katika mahusiano.

Mungu ametuumba kwa ajili ya mahusiano na wanadamu wengine. Tunatamani kuthaminiwa na wengine. Tunatamani kujikita kwa wengine. Mahusiano ni muhimu sana kwa sababu tunafahamu kwamba watu wote wameumbwa na Mungu kama viumbe wa milele wakiwa na hatma za milele.

**Mahusiano na Mungu**

Ubudha ni dini pasipo Mungu. Lakini kila mmoja wetu ana hitaji la ndani kabisa la kumuabudu Yeye.

Mungu alitutengeneza sisi ili kuishi katika mahusiano na Yeye. Mtu ahwezi kuridhika na kutosheka hadi awepo katika mahusiano ya kibinafsi na Mungu. Mahusiano na muumba wetu yatakuwa ya milele, na mbinguni ni mahali ambapo tutaishi na Mungu.

**Msamaha wa Dhambi**

Ubudha hauna dhana ya msamaha wa dhambi. Hakuna anayeweza kumuwajibisha mwanadamu kwa kutenda yasiyo sahihi, na hakuna chochote kinachoweza kufanya upatanisho kwa mambo mabaya yaliyofanyika. Kwa sababu ya mambo haya, Wabudha hawana uhakika wa msamaha wa dhambi.

Biblia inatuonesha kwamba kila mmoja ana hatia na anahitaji msamaha wa dhambi. Kwa sababu Yesu alifanya upatanisho kwa ajili yetu, tunauhakika kwamba tunaweza kusamehewa.

Tumia sehemu zifuatazo kutoka katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* ili kumshirikisha Mbudha:

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu

## Ushuhuda

Mama Yeo alikuwa anamuomba Buddha ili amponye binti yake aliyekuwa katika hali ya kufa, lakini ilionekana kwamba hakuna msaada. Ndipo akakumbuka mmishenari wa Kikristo aliyeitwa Wong ambaye amekuwa akihubiri hapo karibu. Alimtuma Yeo ili amlete. Wong alipofika, alisema, "Usimuombe Buddha; muombe Yesu." Wong alianza kuomba, na msichana akaponywa. Mama Yeo akawa Mkristo siku hiyo, na Yeo akawa Mkristo baadae

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Mwanzo 3 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa Mbudha. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 10
# Utao

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

James alikulia katika familia ya kitao huko Malaysia. Familia yake walikuwa na sanamu na madhabahu kwa ajili ya kuabudu mababu. James aliziogoopa sanamu, lakini alizitolea sadaka akiogopa kwamba zitamuadhibu endapo asingefanya. Alisikia Habari za Yesu, lakini alifikiri kwamba Yesu alikuwa Mungu kwa ajili ya watu wa magharibi tu.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Zaburi 16 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha andiko kinasema kuwa Mungu anatawafanyia nini watu wake? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Utao

### Utangulizi kwa Utao



Utao unaweza kuwa umeanza na kitabu kinachoitwa *Tao Te Ching* kilichoandikwa na Mchina anayeitwa Laozi wakati fulani kabla ya 350 B.C. hakuna uhakika endapo Laozi alikuwa mtu au maandiko yalikusanywa kutoka katika waandishi kadhaa. Maandiko ya mtu anayeitwa Zhuangzi pia yameshawishi uwepo wa dini.

Utao pia unaitwa Udao.

Mkusanyiko wa maandiko ya Utao yanajumuisha zaidi ya vitabu 1,000. Mkusanyiko huo unaitwa *Tao Zang*.

Shughuli na dhana za Utao zimeshawishiwa na Confucianism na nyanja za dini na tamaduniu za kale za Uchina. Shughuli na matendo ya Mtao yanatofautiana kutoka sehemu moja kwenda nyingine.[20]

Ni ngumu kukadiria idadi ya Watao kwa sababu watu wengi hujishughulisha kibinafsi na imechanganywa na dini mbalimbali. Inakadiriwa kwamba kuna milioni 400 ya Watao huko Uchina. Utao upo katikati ya jamii ya makundi mbalimbali ya wachina walioko sehemu mbalimbali za ulimwengu, kama vile Singapo na Taiwani. Pia wapo wengi huko Vietnamu na Korea.

[20] Picha na Julian Tong kutoka Unsplash, ilichukuliwa tena kutoka https://unsplash.com/photos/ng7f_jtgbCc.

Kuna nyumba mbali mbali za kitawa za Utao zilizopo, hazijaungana katika taasisi moja. Watao hujishughulisha na taratibu za ibada ambazo zinalenga kuwashawishi miungu na roho. Nyumba nyingi za kitawa za Watao zinawahitaji washirika wao kula mboga mboga tu. Utaratibu wa ibada unahusisha kutoa sadaka za nguruwe, bata, au matunda. Wakati mwinghine karatasi maalumu ikiwa na picha maalumu huchomwa, dhana ni kwamba kitu kilicho kwenye picha huwa kitu halisi katika ulimwengu wa roho, kikiumba kitu kwa ajili ya roho kutumia.

> "Tunamwamini Mungu mmoja Baba mwenyezi, muumba wa mbingu na dunia, nav yote vinavyoonekana na visivyoonekana."
>
> \- Imani ya Nikea

> "Anajitegemea ambaye anahusika na uumbaji, huyu asiye na mipaka ndiye anashikilia na kutunza kupita mipaka katika kila hatua, huyu mkuu ambaye anajali kuhusu ulimwengu wote na shomoro mdogo, huyu wa milele anatoa na anatunza muda na dunia inayopita."
>
> \- Thomas Oden
> *The Living God*

***Biblia inatuambia sisi kutokufanya mambo ambayo watu katika dini nyingine wanafanya ili kuzishawishi roho katika ulimwengu wa roho, ona Kumbukumbu la Torati 18:10-12. Mungu ni nafsi, na Yeye ni Baba yetu, na tunaweza kuzungumza naye, ona Mathayo 6:7-9.***

► Ni kwa jinsi gani Mkristo ajihusishe na ulimwengu wa roho?

Makundi mbalimbali ya Watao wanaamini makundi mbalimbali ya miungu. Yanaomba kwa na kuingiliana na miungu, roho, na mababu.

***Biblia inasema kwamba wale wanaofuata miungu mingine watapata huzuni badala ya mambo wanayotaka, ona Zaburi 16:4.***

Wanapiga ramli na aina mbalimbali za uganga. Baadhi huamini katika kipitio, mtu ambaye kupitia yeye roho zinawasiliana. Huko China na sehemu nyingine ambapo kuna Watao wengi, wanakuwa na gwaride kila mwaka. Washiriki wanafanya maonesho mbalimbali waliwa wamevalia mavazi mbalimbali yanayowakilisha roho mbalimbali au miungu mbalimbali. Washiriki wanachukuliwa kuwa wamepagawa na miungu au roho ambayo anaiwakilisha.

***Baadhi ya dini wanachukulia mtu kupagawa na roho chafu kuwa ni kitu kizuri, lakini Biblia inaonesha kwamba mtu anayetumiwa na roho chafu ni mtumwa na anahitaji ukombozi, ona Matendo ya Mitume 16:16-18.***

Mungu anayetawala ulimwengu anaitwa Yu-huang, Jade Emperor. Kulingana na simulizi alikuwa mtu aliyezaliwa kwa emperor, ambaye alikua na kuwa mungu kama alivyo leo. Anatawala miungu yote na roho zote. Hata kama Yu-huang mungu anayetawala, juu yake kuna mungu mwingine anayehusika na ulimwengu, ambaye ana sifa kuu za kweli. Yuan-shih T'ien-tsun anaitwa Kanuni kuu ya Kwanza, na inaaminika kuwa hana mwanzo wala mwisho, anaishi kabla ya vitu vingine vyote. Anaaminika kuwa anayejitegemea kuishi, asiye

na mipaka, asiyebadilika, asiyeonekana, mwenye maadili, yupo kila mahali, na chanzo cha kweli yote.

► Ni kitu gani kinakosekana katika dhana ya Utao kuhusu Mungu?

*Tao* ni neno la Kitao kwa ajili ya uhalisia ambao unajumuisha na kutunza kila kitu kinachoishi. Neno *Tao* pia linatafsiriwa kama "njia" kwa sababu linarejelea njia ambayo hutunza na kutengeneza mambo tena.

***Biblia inasema kwamba Yesu ndiye aliyeumba na kutunza kila kitu, ona Wakolosai 1:16-17.***

Watao wanaamini kwamba Tao hawezi kuelezewa au kueleweka. Wanasema kwamba Tao si kila kitu ambacho kinaweza kusemwa kuhusu Tao.

***Hatuwezi kuelewa kila kitu kuhusiana na Mungu kwa sababu Mungu hana ukomo, lakini amefunua kweli kuhusu yeye. Yesu alikuja kutuonesha sisi Mungu alivyo, ona Yohana 1:18 na Yohana 14:6-9.***

► Ni kwa namna gani Theolojia ya Kikristo inatofautiana na maelelzo ya Utao kuhusu Tao? Je, tunaweza kumuelewa Mungu?

Watao wanaamini kwamba upinzani ni taswira ya uongo au dhahania au kirahisi nyanja za maisha zinazokamilishana.[21] Lengo la Mtao kujileta mwenyewe katika usawa na nguvu katika ulimwengu. Lengo lake ni kuboresha afya yake na kurefusha maisha yake. Mtao anaamini mtu anaweza kuwa asiyekufa kama anajiweka sawa na nguvu za anga kikamilifu. Watao wanaamini baadhi ya watu amelifikia hili na wanapaswa kuabudiwa kama miungu. Watao wanaamini Yesu alikuwa mtu ambaye ameendelea kiroho na ameonesha njia ya watu kuwa miungu.



*Mchoro wa "Yin na Yang" unaelezea dhana ya Kitao yaukinzani kama vilewema na ubaya ki ukweli ni pande mbili tofauti za uhalisia.*

***Biblia inatuambia kwamba hatutakiwi kuabudu mtu yeyote ispokuwa Mungu; ona Mathayo 4:10 na Ufunuo 22:8-9.***

Kama Wabudha na Wahindu, Mtao anaamini juu ya mzunguko wa muda. Usio na mwanzo, na usio na mwisho, na hakuna tukio litakaloleta mabadiliko ya kudumu. Tofauti na Uhindu na Ubudha, Watao hawaamini juu ya mfumo wa kuzaliwa tena na tena, karma, na nirvana.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

[21] Picha: "yin na yang ya kitamaduni ikiwa na nukta", na Klem, ilichukuliwa tena kutoka kwa https://commons.wikimedia.org/wiki/File:Traditional_yin_and_yang_with_dots.png.

## Uinjilisti

Kwa sababu Watao hawaamini Biblia, kutumia maandiko kukanusha Imani yao hakutabadilisha akili zao. Badala yake, wasilisha injili ya Kibiblia kwa namna ambayo itagusa mahitaji yao. Ushuhuda binafsi wa mkristo wa mahusiano na Mungu utasaidia kugusa hitaji la Mtao la kumfahamu Mungu.

Tunaweza kukubaliana na baadhi ya maadili ya Utao. Wanafundisha kwamba watu wanatakiwa kuwapenda wengine, kuwa wenye huruma, kuacha ubinafsi, kuepuka kuhukumu wengine, na kuacha kufuatilia utajiri kwa nguvu.

Wanaamini kwamba Tao ndiye chanzo cha kila kitu na yupo katika kila kitu. Tunaamini kwamba Mungu ni muumbaji wa vitu vyote na yuko kila mahali kwa wakati mmoja. Utofauti ni kwamba tunaamini kwamba Mungu ni nafsi mwenye akili na kusudi, na tunaweza kuwa na mahusiano Naye.

Wao wanamaini kwamba Tao anajali vitu vyote. Tunaamini kwamba Mungu anahusika katika uumbaji wake na anaujali, lakini anafanya hivyo akiwa na ufahamu, kama Baba ambaye anatupenda.

Watao wanaamini kwamba lazima kuna mungu mwenye sifa kuu ambaye anajua mambo yote, yuko kila mahali, na ana sifa zote. Hii inaendana na Imani ya kikristo katika Mungu, na tunaweza kuwashirikisha kwamba ndiye Mungu aliyemuumba mwanadamu kwa mfano wake kwa ajili ya mahusiano. Elezea kwamba Mungu ambaye hatuwezi kumfikia, ametufikia kupitia Kristo kufanyika mwili. Elezea kwamba dhambi imetutenga na Yeye lakini tunaweza kuja kwake katika mahusiano kwa sababu ya Yesu.

Wakristo wanaamini kwamba, Mungu wa kweli wa milele amezungumza na kutoa Biblia katika maandishi ya ujumbe wake kwa mwanadamu. Jitoe kumshirikisha Mtao injili, ili kwamba aweze kuamua kuamini au la kwamba ni ujumbe kutoka kwa Mungu.

## Makundi mbali mbali yanayochanganya

► Mwanafunzi asome na aelezee sehemu hii. Kama kundi, orodhesheni matawi ya dini hizi ambayo mmeyasikia.

Kuna matawi mengi ya Ubudha, Uhindu na Utao yakiwa na majina tofauti. Kwa mfano, Falun Gong ni dini ambayo ina misingi katika hizi tatu zote, lakini sana Ubudha. Kama Falun Gong, harakati ya dini inaweza kuanza na mwalimu mmoja ambaye anabadilisha baadhi ya mambo na kufundisha njia zake mwenyewe za kuitenda dini. Hii inaweza kutokea kwa urahisi kwa sababu dini hizi hazina matamko yaliyo wazi yanayoeleweka ya Imani.

Wafuasi wa matawi ya Dini za Mashariki wana mambo mengi yanayofanana na hawajichukulii kuwa wao ndio dini pekee ya kweli. Wanachukua mambo mengine kutoka kwa makundi mengine.

Baadhi ya matawi yanasisitiza afya ya mwili au njia ya kuitikia msongo mkubwa wa maisha. Watu wengi hufanya mazoezi ya akili na mwili kwa ajili ya kupata faida za kivitendo na hawafikirii sana kuhusiana na Imani ya dini. Hata hivyo, matendo hayo yana msingi katika theolojia na elimu ya ulimwengu ambayo inakinzana na kweli ya Biblia.

### Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Zaburi 16 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa Mtao. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

### Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 11
# Uislamu

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Daniel alikuwa mshindi wa ndondi za uzito mkubwa. Alipotembelea Uturuki alisikia wito wa kiislamu wa kusali, na alivutiwa sana. Alianza kuusoma Uislamu na akahisi kwamba ilikuwa dini sahihi kwake. Alidai kuwa Mkristo hapo kabla lakini alishawishika kwamba kulikuwa na makosa katika Biblia.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma 1 Yohana 1 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki kinasema nini kuhusiana na mahusiano ya mwamini na Mungu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Uislamu

### Chanzo cha Uislamu

Uislamu ni dini ya pili kwa ukumbwa ulimwenguni, ikiwa na takribani wafuasi milioni 1.9.[22] Entire nations are ruled by the principles of Islam. Neno *Uislamu* linamaanisha "Kujitiisha," likilejerea kujitiisha kwa Allah. Mfuasi wa Uislamu anaitwa Muislamu. Neno *Muislamu* linamaana "anayejitiisha." Waislamu wanajiita "waamini," na wanawaita watu ambao sio Wislamu "Mkafiri" (wasioamini).

Muhammad alikuwa mwanzilishi wa Uislamu. Aliishi mwaka 570-632 B.K.

Muhammad Alidai kupata mafunuo. Watu wengi waliandika kuhusiana na mafunuo yake, na haya yalikusanywa ili kutengeneza Qur'an miaka mingi baada ya kufa kwake. Qur'an imegawanya katika sehemu zinazoitwa *Sura*.

► Ni kwa namna gani chanzo cha Qur'an ni tofauti na chanzo cha Biblia?

Dini ya Muhammad ilikuwa tofauti na dini nyingine nyingi zilizokuwa zinamzunguka kwa sababu ilikuwa iliyoamini mungu mmoja na ilikuwa kinyume cha ibada ya sanamu. Alifahamu kuhusiana na Uyudaizimu na Ukristo, lakini alizikataa zote.

Muhammad alitokea katika familia maskini, lakini alimuoa mjane Tajiri, alipokufa, alioa wanawake wengine 12 zaidi. Kulingana na Qur'an, wanaume wanaruhusiwa kuoa hadi wake wanne.

---

[22] "Religion: Islam," Joshua Project, https://joshuaproject.net/religions/6, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

Muhammad alipopata wafuasi wa kutosha, aliuteka mji wa Medina, kwa sasa upo nchini Saudi Arabia. Baada ya vita kadhaa, aliudhibiti mji wa Mecca, na akahamia kule. Yeye na wafuasi wake wakavamia na kuyashinda maeneo kadhaa yaliyowazunguka. Hatimaye walizishinda nchi kadhaa na wakawalazimisha watu kuwa Waislamu.

Waislamu wengi leo si wakorofi. Wanajaribu kuishi kwa amani na majirani zao ambao si Waislamu. Hata hivyo, kuna agizo la ukorofi Qur'an. Qur'an inawaagiza Waislamu kuwashambulia na kuwaua maabudu sanamu.[23] Qur'an inasema kwamba watu ambao wanafanya vita kinyume na Uislamu wanapaswa wauawe au mikono na miguu yao ikatwe.[24] Waislamu wa itikadi kali wanayachukua maagizo hayo kwa umakini mkubwa. Muhammad aliharibu vijiji vya kiyahudi, aliwaua wanaume na kuziuza familia zao katika utumwa.

► Ni kwa namna gani Uislamu ulienea tofauti na Ukristo?

**Imani za Uislamu**

Imani ya Uislamu inayorudiwa rudiwa sana inaitwa *shahada* is: "Hakuna Mungu ispokuwa Allah, na Muhammad ni mtume wake."

Waislamu wanaamini kwamba Allah ndiye mungu pekee, muumba wa ulimwengu. Wanaamini kwamba ndiye aliyetoa mafunuo ya kibiblia kwa watu kama vile Nuhu, Abrahamu, na Musa.

Waislamu hawaamini katika Utatu Mtakatifu wa Mungu au kwamba Mungu kufanyika mwili inawezekana.

> "Namwamini Mungu Baba Mwenyezi, Muumba mbingu na nchi. Na Yesu Kristo Mwana wake wa pekee, Bwana wetu. Aliyechukuliwa mimba kwa uwezo wa Roho Mtakatifu, Akazaliwa na Bikira Mariamu."
>
> - Imani ya Mitume

► Ni kwa namna gani mtazamo wa Muislamu kwa Muhammad ni tofauti na mtazamo wa Mkristo kwa Kristo?

Wasilamu wanaamini kwamba Yesu alikuwa nabii kutoka kwa Mungu na alitenda miujiza, alikuwa Masihi, na hakuwa na dhambi. Hawaamini kwamba alikufa msalabani , bali alichukuliwa na Allah wakati Wayahudi wanataka kumuua.[25] Hawaamini alikuwa mwana wa Mungu au ni Mungu aliyevaa mwili.[26] Hawaamini ni Mwokozi wa ulimwengu.

> "Ninashawishika kikamilifu leo kwamba Maandiko ni ya Mungu na kwamba kama mwangaza wa jua. Na ushawishi huu (kama kilazawadi njema) inatoka kwa Baba wa nuru."
>
> - John Wesley
> (barua mnamo 1747)

Waislamu wanaamini kwamba Biblia ilitoka kwa Mungu, lakini wanaamini kwamba kama kuna mgongano kati ya Biblia na kitabu chao kitakatifu Qur'an, Qur'an ndio msemaji wa mwisho kwa sababu

[23] Sura 9:5
[24] Sura 5:33
[25] Sura 4:157-158
[26] Sura 9:30-31, 18:4-5


ndio ufunuo wa mwisho. Wanaamini kwamba ufunuo wa mwisho unaweza kukinzana na ule wa kwanza.[27]

***Biblia inasema kwamba Neno la Mungu halitapita kamwe bali linasimama daima milele, ona Isaya 40:8 na 1 Petro 1:25.***

Wasilamu wanaamini kwamba wokovu unapatikana kwa kutimiza matakwa fulani yanayoitwa Nguzo tano kuu za Uislamu. nguzo tano kuu za Uislamu ni:

1. *Shahada*: Kuitaja kwa uaminifu Imani ya Kiislamu
2. *Salat*: Kufanya taratibu za ibada mara tano kila siku
3. *Zakat*: kutoa sadaka kwa maskini
4. *Sawm*: kufunga wakati wa mwezi wa Ramadan
5. *Hajj*: kwenda kuhiji Mecca mara moja katika maisha

**Mafundisho Magumu ya Uislamu**



Ili kuona aina ya maisha ambayo Wasilamu wanaamini, tunaweza kuangalia nchi ambazo zinaongozwa na sheria za Kiislamu. Sheria za Kiislamu zinaitwa *Sharia*. Nchi nyingi za Kiarabu zinafuata *Sharia* kwa kiwango kadhaa. Sheria za Kiislamu haziruhusu uhuru wa kuzungumza, uuhuru wa kuabudu, uhuru wa mikusanyiko, uhuru wa vyombo vya Habari kama ulimwengu wa magharibi unavyoelewa na kutenda kuhusiana na uhuru kama huo.[28]

Katika baadhi jamii za Kiislamu mtu anaweza kuuawa kwa sababu ya kuokoka au kuwa Mkristo au juhudi za kufanya uinjilisti. Hata hivyo, mtu anaweza kuuawa kwa sababu ya kundi fulani la watu na sio kwa sababu ni kitendo cha kiofisi cha nchi.

Kulingana na Sharia, mwanaume anaweza kumpa talaka mwanamke mara moja kwa sababu yeyote. Mwanamke hawezi kutoa talaka pasipo makubaliano na mume wake. Wanaume wanaruhusiwa kuwapiga wake zao, kulingana na Qur'an.[29] Mwanaume anaweza kuoa hadi wake wanne.[30] Mwanamke anaweza kuuawa na ndugu zake kana hafuati matakwa ya Kiislamu. Katika baadhi ya nchi wanawake hawaruhusiwi kuendesha magari, kwenda shule, au kuonekana hadharani pasipo kufunika nyuso zao. Mwanamke anaweza kupigwa hadharani kama atavunja sheria.

> "Habari njema ni kwamba Mungu kupitia Yesu Kristo alifanya kile ambacho sheria haikufanya: kumtuma mwanaye kama sadaka ya dhambi. Yesu alilipia ghadhabu ya dhambi kwa kifo chake cha kujitoa sadaka."
>
> \- Thomas Oden
> *The Word of Life*

[27] Sura 2:106, 13:39
[28] Picha na Juan Camilo Guarin kutoka Unsplash, imechukuliwa tena kutoka https://unsplash.com/photos/njEXjDmYn8w.
[29] Sura 4:34
[30] Sura 4:3

***Wakristo wanaitwa kuwa wapole kwa wake zao, ona 1 Petro 3:7. Mwanaume anapaswa kumpenda mke wake akama anavyojipenda mwenyewe, ona Waefeso 5:28-29.***

Waislamu wanaamini kwamba mema na mabaya yanakuja tu kutoka katika mapenzi ya Allah. Allah anaweza kubadilisha lile lililo jema kama atachagua, kwa sababu mapenzi yake ndilo analolijali kuliko tabia ya kutobadilika.

***Biblia inatuambia sisi kwamba Mungu ni mwena na ni chanzo cha kila kitu chema. Mungu habadiliki, ona Yakobo 1:17.***

Qur'an haisemi kwamba watu waliumbwa kwa mfano wa Allah. Allah anasemekana kuwa mbali sana na hawezi kufahamika na yuko tofauti sana.

***Wanadamu wameumbwa kwa sura na mfano wa Mungu. Kwa hivyo, tunaweza kuelewa baadhi ya vitu kuhusiana na asili ya Mungu na tunaweza kuwa na mahusiano na Yeye, ona Mwanzo 1:27.***

Waislamu hawategemei kuwa na mahusiano binafsi na Allah. Allah anaitwa "mwenye upendo wote," lakini vinginevyo haisemwi katika Qur'an kwamba anawapenda watu. Qur'an mara nyingi inataja kwamba Allah husamehe na mwenye rehema kwa wale wanaokuwa waamini wa Uislamu. Watu wanapaswa kutubu na kuomba kwamba waepushwe na hukumu wakiwa na matumaini kwamba Allah ni mwenye rehema, lakini hakuna uzoefu wa wokovu au uthibitisho wa msamaha.

***Biblia inatuhaidi sisi kwamba Mungu humsamehe mtu ambaye atakiri na kuamini, ona 1 Yohana 1:9.***

► Ni kwa namna gani mahusiano ya Wakristo na Mungu ni tofauti na mahusiano ya Waislamu na Allah?

Faida za Uislamu mara nyingi ni kwa wanaume, na Qur'an hushughulikia jambo katika mtazamo wa wanaume. Wanawake ni miliki ya wanaume. Paradiso ya Kiislamu baada ya kifo ni kwa ajili ya wanaume, wanawake wakitolewa kule kwa ajili ya starehe.[31]

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Uinjilisti

Haitoshi tu kuthibitisha mafundisho ya Kikristo kutoka kwenye Biblia, kwa sababu Waislamu wanaamini kwamba Qur'an ni mbadala wa Biblia kama mamlaka ya mwisho

Tunaweza kukubaliana na baadhi ya mafundisho ya muhimu ya Kiimani ya Kiislamu. Wakristo hukubaliana kuna Mungu aliyeumba Ulimwengu. Wakristo wanakubali kwamba kuna hukumu ya mwisho, na kwamba kila mtu atapelekwa ama jehanamu ama mbinguni.

[31] Sura 55:56

Kweli nyingine muhimu zinapaswa zioneshwe katika Biblia. Waislamu wanaamini kwamba Biblia imetoka kwa Mungu lakini inazidiwa na Qur'an. Hata hivyo, unaweza ukajenga hoja kwamba kuna kweli nyingine ni za msingi kiasi kwamba hazibadiliki. Pia, kweli za kihistoria hazibadiliki.

Mungu aliwaumba wanadamu kwa mfano wake (Mwanzo 1:27). Anawapenda na anataka kuwa katika mahusiano na wao.

Wakristo wanakubaliana na Uislamu kwamba Yesu ni Masihi na hakuwa na dhambi. Onesha kwamba alihaidi kutoa uzima wa milele kwa wale wanaomwamini (Yohana 10:28), aliahidi kuwafufua wafu kwa sauti yake (Yohana 5:28-29), na alisema ya kwamba hakuna awezaye kuja kwa Baba ispokuwa kwa Yeye (Yohana 14:6).

Onesha kutoka katika Maandiko kwamba alikuwa zaidi ya mtu asiyekuwa na dhambi; Ona *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* juu ya

(5) Yesu ni Mungu.

Asingeweza kuwa mtu mwema na nabii wa Mungu kama madai yake kuhusiana na Yeye yasingelikuwa kweli. Uislamu unafundisha kwamba Yesu alikuwa nabii wa Mungu, lakini ama alitakiwa kuwa kama alivyodai kuwa na kuweza kutoa uzima wa milele, au alikuwa mtu mwovu na mbinafsi aliyewafanya watu waweke tumaini kwake.

Yesu alikuja kuonesha upendo wa Mungu. Alionesha kwamba Mungu anampenda kila mtu, wakiwemo wanawake na watu wa tabaka la chini. Watu hawajatengwa na Mungu kwa sababu ya jinsia au tabaka la kijamii. Watu wanatengwa na Mungu kwa sababu ya dhambi zao, na Mungu ametoa msamaha. Mungu anamkaribisha mwenye dhambi ili asamehewe na kuingia katika mahusiano na Yeye.

## Ushuhuda

Jalal aliishi huko Saudia Arabia. Akiwa mvulana alikuwa mwaminifu kwa dini ya Kiislamu. Alikariri sehemu kubwa ya Qur'an na alisaidia katika msikiti. Alipokuwa na miaka 16, alitaka kujiunga na vita takatifu ili apigane kwa ajili ya Uislamu, lakini wazazi wake walisema alikuwa mdogo sana. Baadae alipata kazi na akawa na shughuli nyingi na akaanza kukupuuza dini. Aliingia katika shida na alitaka kuomba ilia pate msaada, lakini aliogopa kwamba Allah alikuwa amemkasirikia kwa sababu ya kuipuuza dini. Alimuomba Yesu ili apate msaada, na tatizo likatatuliwa siku mbili baadae. Alipata ndoto na alimuona Yesu akiwaonesha watu njia ya kwenda mbinguni. Aliweka Imani yake katika Kristo kwa ajili ya wokovu. Jalal anasema, "ninasikia upendo ndani ya moyo wangu, na nina furaha kumfahamu Yesu. Nilipokuwa Muislamu, sikuweza kufikiri kwamba Wakristo walikuwa sawa. Baada ya hapo, nimegundua ni kwa kiasi gani Mungu ananipenda, na nikawa Mkristo. Ndio, ananipenda, anakupenda, anaupenda ulimwengu wote. Yesu Kristo anatupenda sisi, na bado anatupenda. Na usisahau siku za mwisho hakuna anayeweza kukuokoa, ni Yesu Kristo tu."

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma 1 Yohana 1 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa mfuasi wa Uislamu. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 12
# Uyudaizimu

## Kukutana kwa mara ya kwanza

Hans alikuwa Mjerumani ambaye alihamia Marekani. Alipokuwa chuo alitengeneza marafiki waliokuwa Wayahudi. Aliifahamu historia ya Wayahudi na alifahamu kuwa mamilioni yao yalikuwa yameuawa na Wajerumani chini ya Hitler. Aliona aibu ya kuwa Mjerumani, na alijiuliza kama angejiunga na Uyudaizimu kulipa kwa sehemu ambacho nchi yake imekifanya.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Isaya 52:13–53:12 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambayo inafupisha kifungu hiki cha andiko. Kama hukujua kuhusu Yesu, je ungeweza kuona ni nini kifungu hiki kinasema kuhusu mtu anayeitwa "mtumishi"? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Uyudaizimu

Uyudaizimu unakaribiana sana na Ukristo kuliko kuliko dini nyingine yoyote ambayo haijiiti kuwa ya Kikristo. Uyudaizimu unadai kumwabudu Mungu wa Israeli ya zamani, Mungu wa Agano la Kale, ambaye ndiye Mungu yule yule anayeabudiwa katika Ukristo. Maandiko ya Uyudaizimu ni Agano la kale katika Biblia ya Kikristo.

***Wafuasi wa Uyudaizimu wanaamini Agano la kale, lakini hawaelewi kweli muhimu sana katika Agano la kale kuhusu Masihi, angalia Yohana 5:39-40, 2 Wakorintho 3:14-16.***

Uyudaizimu wa sasa umetokana na dini na historia ya Israeli kama ilivyoelezewa katika Agano la kale. Matendo na Imani zimechukuliwa katika karne nyingi na hazifanani kabisa na zile za kwanza.

Kuna takribani wafuasi milioni 14 wa Uyudaizimu. karibu nusu yao wanaishi katika taifa la Israeli.

Uyudaizimu ni dini ya msingi ya taifa la Israeli, na wafuasi wengi wa Uyudaizimu kwa asili ni Wayahudi, ama wanaishi Israeli au mahali pengine. Ukisema mtu ni Myahudi kwa kawaida unatambulisha dini na asili yake, na mara nyingine utaifa wake.

> "Ni asili ya pendo la Mungu kuchagua. Halichagui ili kuwatenga wengine ila ili kutoa njia ambayo upendo wa Mungu utajulikana kwa watu wote. Upendo wa Mungu ulifunuliwa hasa kwa Israeli ili kwamba uoneshwe kwa wote."
> - W.T. Purkiser
> *God, Man, and Salvation*

Hata hivyo, tafsiri ni ngumu. Wafuasi wengi wa Uyudaizimu ni wa asili ya Kiyahudi, lakini watu wamebadilikia katika Uyudaizimu kutoka kwenye makundi mengine ya asili. Uyudaizimu ni dini ya kitaifa, lakini 25% ya watu katika Israeli siyo Wayahudi, katika dini au asili. Wayahudi wengi hawaishi Israeli, na baadhi ambao wanaishi Isareli hawafanyi dini yoyote kwa kumaanisha. Mtu ambaye kwa asili ni ni Myahudi, ama katika Israeli au mahali popote, anaweza kuwa amebadilika kwenda kwenye dini tofauti, au hata kuamini kuwa hakuna Mungu.

► Muelezee Myahudi ni nani, kwanza na tafsiri ya asili, kisha na tafsiri ya kidini.

## Sifa maalumu za Uyudaizimu

### Maandiko ya Kiebrania

*Torah* ni neno la Kiebrania ambalo linamaanisha mafundisho, mwelekeo, au sheria. Ni neno linatumika mahususi sana kurejelea vitabu vitano vya kwanza vya Agano la Kale. Mara nyingine linatumika kwa upana zaidi kurejelea Biblia ya Kiyahudi, ambayo ni Agano la Kale katika Biblia za kikristo za Kiprotestanti. Istilahi Torati imetumika kwa upana zaidi ili kujumuisha maelezo ya vifungu vya Kiebrania vilivyoandikwa na walimu wa kale wa Kiyahudi

Wayahudi wanaheshimu sana vifungu vilivyovuviwa na Mungu. Katika nyakati zilizopita Torati (inarejerelea vitabu vitano) iliandikwa kwa namna ya umakini sana ambayo ilizuia makosa. Vitabu vilivyokuwa na Torati vilitunzwa kwa heshima kubwa

*Talmud* ni mkusanyiko wa maandiko ya walimu wa kale wa Kiyahudi. Yalitolewa katika namna ya kitabu, ni zaidi ya kurasa 6,000. Uyudaizimu unategemea Talmud katika mamlaka kwa ajili ya mila na taratibu zao.

### Kutahiri

Mwanzo 17:9-14 Ni kumbukumbu ya amri ya Mungu kwa Ibrahimu kwamba wanaume wote katika nyumba yake watatahiriwa kutahiri ni alama ya agano kati ya Mungu na Israeli. Wana wa Israeli waliwaita watu wa mataifa mengine kama "wasiotahiriwa"—watu ambao hawakuwa na sheria ya Mungu wala agano. Katika nyakati za sasa, watu wengi ambao siyo Wayahudi wanatahiri kama mchakato wa kitabibu, lakini bado Wayahudi wanachukulia kuwa ni kitendo cha kidini.

### Sabato

Sabato ni siku ya saba ya wiki. Sabato inakumbusha siku ambayo Mungu alipumzika kutoka katika kazi yake baada ya siku sita za uumbaji (Mwanzo 2:2-3). Mungu alisema kuwa watu wapumzike siku ya Sabato (Kutoka 20:8-11). Wayahudi walitengeneza makatazo mengi kwa ajili ya sabato ili kuifata kanuni ya kupumzika kutoka kwenye kazi. Wayahudi wanaofata makatazo hawafanyi kabisa biashara yoyote au kazi yoyote kama inawezekana kuzuilika. Wanajaribu kufanya matumizi ya kisasa kwenye makatazo ya zamani ya Sabato. Kwa mfano, Wayahudi wa zamani hawakupaswa kuwasha moto katika nyumba zao siku ya

Sabato (Kutoka 35:3), ingawa wangeweza kuuacha uendelee kama uliwashwa hapo awali. Baadhi ya Wayahudi wa sasa hawawashi taa za umeme au joto siku ya Sabato, lakini wanatumia taa na joto ambalo lilikuwa limewashwa hapo awali

## Uyudaizimu na Injili

Taifa la Israeli kiujumla lilimkataa Yesu kama Masihi. Wayahudi waliomwamini Yesu walikuwa washirika wa kwanza wa kanisa la Kikristo, kisha kuenea kwa injili kuliwaleta Mataifa katika kanisa.

***Mungu anatamani kuwa Wayahudi wote waokolewe, ona Warumi 9:31, Warumi 10:1, na Warumi 11:1.***

Leo kuna mashirika kama vile Wayahudi kwa Yesu ambao wanajaribu kuutunza urithi wa Kiyahudi wakati wanapokuwa Wakristo. Wanaitwa "Wayahudi wanaomkubali Yesu kama Masihi" kwa sababu wanamkubali Yesu kama Masihi wakati wakiendelea kujitambulisha kama Wayahudi. Wao sio sehemu ya dini ya Uyudaizimu.

Uyudaizimu ni dini ya Wayahudi ambao walijaribu kuitunza dini ya Agano la Kale wakati wakimkataa Yesu kama ukamilisho wa matumaini ya Agano la Kale. Kuna makundi makuu matatu katika Uyudaizimu wa kisas: Uyudaizimu wa Kiorthodox, Uyudaizimu wa matengenezo, na Uyudaizimu wenye itikadi kali.

Zaidi ya karne, Uyudaizimu umeendelea kutengeneza tamaduni zake, wakati wakiendelea kutunza tamaduni nyingi kutoka katika nyakati za kale. Wayahudi wengi wanafuata tamaduni za mavazi ambayo yanawafanya watambulike kama Wayahudi. Wanafuata pia makatazo ya chakula ya Agano la kale kama kujizuia kula nyama ya nguruwe

***Wakristo wako huru mbali kutoka kwenye matakwa ya Agano la Kale ya siku maalumu na chakula kwa sababu vitu hivyo vilikuwa alama ya Kristo, na sasa ameshavitimiliza vyote, angalia Wakolosai 2:16-17.***

KatikaUyudaizimu, wokovu hautokei kama uzoefu wa badiliko la mtu binafsi. Wayahudi wanaamini wanaweza kuishi katika uhusiano uliobarikiwa na agano na Mungu kwa kufuata amri zake. Wokovu unamaanisha kuokolewa katika hali ya uonevu au hali ambazo zinawazuia kumtumikia Mungu kama wanavyopaswa. Wokovu ni suala la kitaifa au kundi zaidi kuliko suala la mtu binafsi.

► Ni nini dhana ya wokovu katika Uyudaizimu?

Kulingana na Ukristo wa kibiblia, wokovu unamaanisha ukombozi binafsi wa mtu kutoka kwenye dhambi. Yeyote aliyeokolewa ameokolewa kwa neema kupitia imani, ama ni Myahudi au Mtu wa mataifa. Kila mtu ametenda dhambi na anahitaji msamaha. Wokovu haupatikani kwa kuzingatia vipengele vya sheria ya Agano la kale, bali kwa kuitafuta neema kupitia imani. Hakuna mtu anayepata haki kwa kuitunza sheria, kwa sababu kila mtu ameshatenda dhambi na kuivunja sheria (Warumi 3:20-23).

Ukristo ni muendelezo na ukamilifu wa dini ya Israeli kama ilivyofunuliwa katika Agano la Kale. Mungu ni Mungu wa wote Wayahudi na Watu wa mataifa, na ana mpango wa wokovu kwa wote (Warumi 3:29-30).



Manabii wa Israeli walitabiri kuja kwa Yesu. Kiini cha Imani ya Agano la Kale ilikuwa uhusiano na Mungu, uliwezekana kwa msamaha na neema yake. Kwa hiyo, Wakristo wanadai kuwa na maandiko ya Agano la Kale kama urithi wao.[32] Wakristo wanafuata mfano wa wale ambao walikuwa na uhusiano sahihi na Mungu tangu awali katika mwanzo wa mwanadamu. Kwa maana hiyo, Myahudi halisi ni yule ambaye alipokea kazi ya neema ya Mungu katika moyo wake (Warumi 2:28-29). Baraka ya Ibrahimu inapatikana kwa Mataifa (Wagalatia 3:14).

► Kwa nini ni kweli kusema kwamba Ukristo sio dini mpya?

Hakuna shirika moja kwa wafuasi wote wa Uyudaizimu, hakuna usemi mmoja wa imani ambao wote wanaushikilia, na hakuna mamlaka ya mwisho ya fundisho ambalo wote wanalitambua. Baadhi ya mashirika yao yana misimamo mikali sana, yenye mtazamo wa juu sana ya maandiko, na yanajaribu kushilia tamaduni na imani za kale. Mashirika mengi ya Wayahudi wa Kiliberali wamejifunza imani na tamaduni zao kuwafanya waendane na mila za kisasa, kuchagua ni nini wanataka kutunza kutoka kwenye tamaduni na maandiko.

Uyudaizimu hauamini kuwa Mungu ni utatu au kwamba Mungu kuuvaa mwili kumetokea. Wayahudi wanaamini kwamba Yesu alikuwa mwalimu mwenye utata ambaye hakuwa Masihi wala Mungu.

***Agano la Kale lilitabiri kuwa Masihi atakuwa Mungu mwenye nguvu, angalia Isaya 9:6. Agano Jipya linasema kwamba Yesu ni Mungu Mwana na Masihi, angalia Warumi 1:1-4.***

Matazamio kwamba Masihi atakuja ni kiini kwa Uyudaizimu. Hawaamini kuwa Masihi ameshakuja. Wanaamini kuwa Masihi hatakuwa Mungu aliyefanyika mwili, isipokuwa mtu maalumu aliyepakwa mafuta, atakayeleta amani katika ulimwengu.

Wayahudi wenye misimamo mikali wanaamini kuwa Masihi atakuwa mtu halisi. Wayahudi huru huenda wanazingatia zaidi kuwa Masihi ni lugha ya picha ya mjumbe wa amani, ambaye anaweza kuwa kundi au shirika fulani.

► Fafanua dhana ya Masihi ya Uyudaizimu.

Biblia inatuambia kuwa muda utafika ambapo Israeli itamkubali Kristo (ona Warumi 11:23-26.) Mtume Paulo alisema sasa injili inaenea kati ya mataifa, na Wayahudi wengi wamepofushwa kwa habari ya injili. Lakini anaendelea kusema, "Israeli wote wataokoka"

[32] Picha na nellyaltenburger kutoka Pixabay, ilitafutwa tena https://pixabay.com/photos/torah-scroll-israel-jewish-4299038/.

(Warumi 11:26). Hiyo haimaanishi kuwa kila Myahudi ataokolewa, lakini kama taifa wamemkataa Yesu, na kama taifa watatubu na kumkubali. Hata sasa, Wayahudi wengi wanabadilishwa.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

**Uinjilisti**

Baadhi ya wayahudi wanabaguliwa dhidi ya Ukristo kwa sababu wakati mwingine Wayahudi wamekuwa wakiteswa sana na waliodai kuwa Wakristo katika nyakati zilizopita. Tunaweza kujaribu kuwasaidia kutambua baadhi ya kweli kuhusu kuteswa. Kwanza, Yesu kamwe hakuhimiza mateso, na waliodai kuwa Wakristo ambao wanawachukia wengine hawafuati mfano wake. Mateso yako kisiasa vilevile kidini, na yanahimizwa na sababu ambazo zinapinga kanuni za Ukristo. Namna bora ya Myahudi kushawishika kuwa Wakristo siyo adui zake ni kwa Wakristo kuonesha upendo wa Kristo.

> "Katika Warumi 9:4-5 Paul essentially says that kimsingi Paulo anasema
> ' Kristo alikuwa katika hali ya mwanadamu Myahudi lakini kiukweli Mungu.'"
>
> - imetolewa kutoka
>
> Willard Taylor
> *God, Man, and Salvation*

Dini ya Myahudi inahusianishwa sana na familia yake kubwa, namna yake ya maisha, na urithi wa kale. Myahudi anaweza kufikiri kuwa angepoteza kila kitu cha maana kama atabadilika na kuwa kwenye dini nyingine. Mkristo anapaswa kuonesha kuwa Yesu ni ukamilifu wa asili wa dini ya Kiyahudi. Ni Masihi waliyemtarajia. Alitoa wokovu uliofafanuliwa katika Agano la Kale.

Ukweli kwamba Yesu ni Masihi umefafanuliwa kwa ukamilisho wake wa unabii wa Agano la Kale. Mifano ni utabiri kuwa masihi atazaliwa katika Bethlehemu (Mika 5:2) na kwamba angekuwa wa kabila la Yuda (Mwanzo 49:10). Ni muhimu hata kuonesha kutoka Isaya 52:13-53:12 kwamba aliukamilisha wokovu ambao ulitarajiwa kwa Masihi. Yesu bado hajaukamilisha unabii wake wa Kimasihi wa amani ya ulimwengu, lakini inaeleweka kuwa wokovu kutoka dhambini ni lazima uje kwanza kwa sababu vita inatoka katika mioyo ya watu wenye dhambi.

Ni muhimu kushirikisha Injili na kusisitiza kuwa mtu aliyeokoka anaingia katika uhusiano binafsi na Mungu. Wayahudi wanamwamini Mungu lakini hawana uhusiano binafsi na Yeye.

Inawezekana kuielezea Injili kwa kutumia Agano la Kale. Watu wote wamemtenda Mungu dhambi (Zaburi 143:2). Dhambi inawatenga watu na Mungu (Isaya 59:2). Masihi aliteseka na alikufa kama sadaka kwa ajili ya dhambi zetu (Isaya 53:5). Mungu anaahidi kusamehe na kumsafisha ambaye anatubu na kuamini (Isaya 1:16-18).

Zaburi 51 ni maombi ya toba na imani. Daudi aliomba msamaha na kusafishwa. Haya ni maombi yanayohamasishwa na Roho wa Mungu, ambayo yanatuambia kuwa Mungu anatoa msamaha namna hii. Kama mtu anaamini kwamba Mungu amemtoa Yesu kama Sadaka kwa ajili ya dhambi, anaweza kuomba maombi haya katika imani na kuipokea neema ya Mungu.

## Ushuhuda

Daudi ni mwanaume wa Kiyahudi ambaye familia yake ilitokea Ujerumani. Mababu na bibi zake wote walifariki katika magereza ya kambi za Nazi. Anasema kuwa Wayahudi walihisi kwamba walikuwa wakiuawa na ulimwengu wa Kikristo kwa sababu makanisa ya Ujerumani na ulimwengu uliobaki uliruhusu. Wazazi wake walimwambia kuwa kamwe asiuangalie msalaba kwa sababu uliwakilisha kifo. Kila siku basi la shule yake likipita kanisa lenye msalaba, ana alijaribu kutokuliangalia. Siku moja rafiki wa Kiyahudi alijaribu kumpa Agano Jipya, lakini alikataa, akisema kuwa hiyo haikuwa kwa ajili ya Wayahudi. Baadaye rafiki mwingine alimuonesha mistari katika Agano la Kale na Agano Jipya ambayo hakuwahi kuiona hapo kabla. Daudi alikuwa na maswali mengi kuhusu kwa nini ulimwengu uko hivi, na alianza kuona majibu katika Biblia. Akaamini kuwa Yesu ni Masihi.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Isaya 52:13–53:12 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha maandiko kwa mfuasi wa Uyudaizimu. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa kila somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha Injili kwa mtu kutoka kwenye kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wana darasa wenzako kuhusu mazungumzo ambayo mmekuwanayo. Andika ripoti yako iliyoandikwa ya kurasa 2 na urejeshe kwa kiongozi wako wa darasa. Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 13
# Dini ya New Age

## Kukutana kwa mara ya kwanza


Ethan alikuwa katika dini ya Romani Katoliki, lakini aliacha kuenda kanisani alipokuwa mtu mzima. Aliishi kwa starehe kwa miaka mingi, lakini alianza kuhisi kuwa anahitaji kujua kusudi la maisha yake haraka. Rafiki yake alimfundisha kutumia dawa za kulevya, na Ethan alihisi kuwa amepata taswira mpya ya ulimwengu na yeye mwenyewe. Alianza pia kusikia sauti zikimpatia muelekeo.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Zaburi 19 pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki kinatuonesha nini kuhusu matokeo ya kweli ya Mungu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Dini ya New Age

### Utangulizi wa dini ya New Age



*Stonehenge, kumbukumbu ya jiwe la kale huko Uingereza, ni eneo la shughuli za dini mbalimbali.*

Dini ya New Age ina makundi, mashirika na watu mbalimbali. Wafuasi wa dini ya New Age hawajaungana chini ya jina fulani au kauli ya Imani. Baadhi yao huonekana kuwa watu wa kidini, na wengine huonekana kuwa kundi la kisayansi badala ya kidini. Si wote husema kuwa ni sehemu ya dini ya New Age, lakini wote hushiriki sifa fulani.[33]

Wafuasi wa New Age huamini katika uwezo wa binadamu kutatua matatizo yote. Wanaamini kuwa mtu anaweza kuwa kiumbe chenye nguvu mbali zaidi ya inavyozingatiwa kuwa kawaida. Huamini kuwa majibu yote yapo ndani yetu. Huamini kuwa lengo la elimu si kutuambia nini ni kweli ila kutuonesha namna ya kufungua uwezo wetu binafsi.

***Biblia inasema moyo huwa mdanganyifu na mwovu hadi utakapobadilishwa na Mungu. Mtu hawezi kupata majibu ya maisha. Matatizo yamo ndani, ona Yeremia 17:9.***

► Ni mafundisho yapi ya Kikristo dini ya New Age inayapuuza?

[33] Picha na Dyana Wing So kutoka Unsplash, ilichukuliwa tena kutoka https://unsplash.com/photos/NxvP54MX4no.

Kufungua uwezo wa kibinadamu, wafuasi wa New Age hutafuta hekima za zamani katika dini ya kipagani na vitendo vya kichawi. Hufanya unajimu, mawasiliano ya kipepo na uaguzi wa kila namna Wafuasi wa New Age huingiliana na ulimwengu usioonekana kwa kutumia namna yeyote ya uchawi. Hujaribu kuwasiliana na roho na watu walioishi zamani. Wanafanya matendo ya kuwasiliana na roho kupitia upitishaji wa roho, ambapo roho ya mtu aliyeishi zamani huvaa mwili wa mtu anayeishi na kuchukua sauti yake kwa muda

***Watu humkataa Mungu na tafuta vyanzo vingine vya msaada katika ulimwengu usioonekana kwa sababu hawataki kutubu dhambi. Mtu anayehitaji muongozo na nguvu lazima amtafute Mungu, tazama Isaya 8:19.***

Hawaamini kuwa dini yoyote ina ukweli wote. Huamini kuwa dini zote kimsingi ziko sawa, lakini zina Imani na mazoea tofauti ambayo yanasaidia. Hata kama Imani fulani zinapingana, huamini kuwa zote ni za kweli, hufikiri kuwa wote huweza kuwa kweli katika namna isiyo ya busara. Hukataa madai yoyote kuwa fundisho ni kweli kabisa. Hawaamini kuwa fundisho lolote laweza kuwa kweli kwa maana kwamba mafundisho yanayokinzana yaweza kuwa uongo. Wafuasi wa New Age huweza vumilia kundi lolote la dini isipokuwa wale ambao hudai kuwa na kweli ambayo kila mtu ni lazima aamini. Hukataa Ukristo kwa sababu unadai kuwa sahihi na husema kuwa dini nyingine si sahihi.

> "Wakati mwingine inasemekana kwamba tunaishi chini ya utamaduni tofauti na kile ambacho ni sawa au si sawa kwa sasa kimebadilika kwa sababu ya muda kubadilika.... katikati ya [machafuko] ya mabadiliko ya mwanadamu unasimama mwamba wa kweli ambao ni neno la Mungu na viwango vyake havibadiliki."
>
> \- Leslie Wilcox
> *Profiles in Wesleyan Theology*, *Volume 3*

***Biblia inanena wazi hukumu juu ya wale wasiotenganisha maovu na wema na kukataa kiwango cha wema na ubaya, ona Isaya 5:20.***

► Ni dini gani nyingine ambazo wafuasi wa New Age wasingependa?

Wafuasi wa New Age hukubali ulimwengu usioonekana bila kanuni yoyote ya kutenganisha kati ya nguvu nzuri na nguvu mbaya. Huamini kuwa ushirikiano wowote wa kiroho ni mzuri.

***Kuna roho mbaya zinazohusika katika ulimwengu, na zimekwisha hukumiwa adhabu ya milele. Watu wanaozifuata watashiriki hukumu yao ona Mathayo 25:41.***

Wafuasi wa New Age hawajitenganishi na dini nyingine. Hufikiri kuwa baadhi ya dini hushiriki Imani zao nyingi, haswa dini za mashariki kama Wabudha, Wahindu na Watao. Pia wanapenda dini za asili, ambazo zinaingiliana na roho katika asili (ona Somo namba 14).

Wafuasi wa New Age hukataa uhalisia wa mauti. Hufikiri kuwa kifo ni pale mtu anapoenda katika hatua nyingine ya uwepo. Baadhi husema kuwa maisha baada ya kifo ni kama sawa na maisha ya asili. Wengi wao huamini katika kuzaliwa upya na kanuni ya Karma, kama ilivyo kwa Wahindu. Badala ya kuona kama kuzaliwa upya ni kitu kibaya, kama Wahindu na

Wabudha wanavyofanya, Wafuasi wa New Age hufikiri ni njema kuishi mara nyingi. Baadhi yao hufikiri kuwa wanajua kuwa walikuwa akina nani katika maisha yaliyopita

Dhana ya Mungu kwa wafuasi wa New Age ni ya kishabiki. Hii humaanisha kuwa wafuasi wa New Age huamini ukweli wote ni kiini kimoja, na kuwa kila kitu kwa pamoja ni Mungu. Kila kitu na kila mtu ni sehemu ya Mungu. Hawaamini kuwa Mungu ni mtu anayefikiri au kuongea, na hukataa kuwa Mungu ni muumbaji.

► Mfuasi wa New Age anaomba?

Wafuasi wa New Age huamini kuwa Yesu alikuwa mtu aliyejua jinsi ya kutumia nguvu zake za pekee na kujaribu kuwafundisha wengine kufanya hivyo pia. Huamini kuwa Yesu hakujali kuhusu viwango vya maadili na hakuhukumu maovu ya mtu yeyote.

Wafuasi wa New Age hawaamini katika ukweli kuhusu dhambi, kwa sababu hawaamini katika Mungu alieweka viwango na waamuzi. Huamini kuwa uovu katika ulimwengu ni uhitaji wa maarifa na marekebisho ili kila kitu kiwe katika maelewano. Wafuasi wa New Age huhalalisha kila aina ya upotovu wa dhambi.

***Mungu huwakaribisha watu kutafuta suluhu ya kweli –msamaha na usafi, tazama Isaya 1:18.***

Wafuasi wa New Agers hukataa dhana ya biblia ya Wokovu. Hawaamini kuwa dhambi ni halisi lakini huamini kuwa suluhu ya matatizo ya binadamu ni maendeleo ya ufahamu wa kiroho na nguvu za kiroho.

Wafuasi wa New Age huamini kuwa utu ni kuingia katika zama mpya ambapo watu wanaoelewa kanuni za zama mpya watabadili jamii yote. Huamini kuwa kutakuwa na Amani na ulinzi kiuchumi kwa kila mtu.

> "Shetani hukufanya kujiabudu sanamu mwenyewe; kukufanya mwenye hekima katika macho yako mwenyewe kuliko Mungu mwenyewe na maneno ya Mungu. Ili kufanya hivi, hawezi tokea katika umbo lake. Hiyo ingekatisha mpango wake. Badala yake, anatumia ujuzi wake kukufanya ukatae uwepo wake mpaka pale anapokuwa nawe katika mahala pake."
>
> - John Wesley
> "A Caution against Bigotry"

***Biblia inatuonya tusitarajie amani na ulinzi katika jamii ambayo haijakabidhiwa kwa Mungu. Tazama, 1 Wathesalonike 5:3.***

► Wafuasi wa New Age wanaamini nini mbali na dhana ya wokovu?

### Kutambua wawakilishi wa Zama mpya

Kuna vitu vingi vinavyosaidia kutambua kundi, shirika, au mwandishi kama Zama mpya. Baadhi ya mifano ni:

- Ulaji mboga kwa sababu za kidini au ki filosofia
- Njia za kiafya za kifumbo zisizoweza kuelezeka kisayansi.
- Marejeleo ya Karma
- Matumizi ya masharti kuhusu kuishi katika umoja na asili ama ulimwengu.

- Kutafakari kama namna ya uelewa usio na mantiki
- Matumizi ya masharti kuhusu uwezo wa binadamu usio na ukomo
- Aina za ajabu za nguvu na nishati ya kisaikolojia na ajabu
- Mawasiliano na watu waliokufa ama roho
- Matumizi ya vitu mbalimbali kwa ajili ya uaguzi
- Unajimu
- Uchawi na ushirikina
- Ushiriki wa kidini na asili
- Maslahi katika piramidi na fuwele
- Maslahi katika UFOs na viumbe visivyotoka katika dunia
- Imani katika uongozi wa kiroho na viumbe vya juu
- Dhana na mazoea yaliyotokana na dini za Mashariki

► Ni mifano ipi ya vitendo vya New Age umekwisha sikia ama kuona?

**Mwitikio wa Wakristo**

Hakuna jipya kuhusu dini ya New Age religion. Isaya 47:10-14 imeelekezwa kwa taifa mahususi ambalo linatenda kila aina ya uchawi, na husikika kuwa New Age. Watu walitafuta hekima ya kipekee wakati wakitenda uovu. Wakijaribu kuwa miungu. Waliingiza mbinu nyingi za kutengeneza nguvu za kiroho.

> "Ninakiri ubatizo mmoja kwa msamaha wa dhambi; na ninatazamia ufufuo wa wafu; na maisha ya ulimwengu ujao."
>
> - Imani ya Nikea

Biblia inakataza kila aina ya uchawi na ushirikina, si kwa sababu si halisi, lakini kwa sababu ni uovu na unapingana na nguvu za Mungu (Mambo ya Walawi 19:26, 31, Mambo ya Walawi 20:6, Kumbukumbu la Torati 18:9-12). Mungu aliamuru taifa la Israeli kuwaua wachawi (Kutoka 22:18, Mambo ya Walawi 20:27). Wkristo leo hawana jukumu la kumuua yeyote, lakini amri inaonesha hukumu thabiti ya Mungu juu ya dhambi hiyo. Katika agano jipya, watu walipobadilishwa kuwa Wakristo, waliharibu vitabu vyao vya uchawi (Matendo ya Mitume 19:19).

Watu humkataa Mungu lakini bado hutafuta nguzu za kiroho. Nguvu za Mungu ni kubwa kwa wale wanaomuamini, na hutumia nguvu zake kwa wale wanaomuamini, lakini haachi nguvu zake chini ya udhibiti wa watu. Mtu anayetafuta nguvu na maarifa kupitia mbinu za kichawi anajaribu kutafuta huku akimkataa Mungu. Muingiliano na roho na utafutaji wa nguvu humpelekea mtu katika uovu wa kina.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Uinjilisti

Ni kipaumbele kushiriki injili pamoja na mfuasi wa New Age. Usikamatwe katika mabishano ambayo yatakuzuia kushiriki injili. Anaweza fikiri kuwa ana mazoea na makanisa, lakini anaweza asielewe kiuhalisia injili ni nini.

Yesu alidhihirisha nguvu kubwa kuponya, kutabiri na kutambua kweli. Alikuwa mkuu kuliko kiongozi yeyote wa New Age. Si mfano wa mtu aliejiendeleza mwenyewe na kutumia nguvu za kiroho kutoka katika asili. Yesu aliwasilishwa kwa Baba na aliamini katika ukweli mtupu. Hakukubaliana na wale wasioamini ukweli wa mamlaka ya Mungu, dhambi, na hukumu.

Wakristo huamini katika zama mpya zinazokuja na ufalme wa Mungu. Itakuwa mwisho wa mateso, na zitaleta Amani na mafanikio. Wale tu walio katika uhusiano sahihi na Mungu wanaweza ingia katika zama hizo mpya.

## Ushuhuda

Ethan alijaribu kufuata sauti alizosikia. Zilimwambia kuwa yeye ni Kristo, mwana wa Mungu, lakini alikataa udanganyifu huu. Mara kadhaa alihisi nguvu na maarifa yasiyo ya kawaida. Baadhi ya rafiki zake walimwambia hakuna ugomvi kati ya kumwamini Yesu na kuamini katika Budha au kitu kingine. Alianza kuhisi kuwa kitu kilichompa nguvu kilijaribu kumpagaa. Alikutana na kundi la Wakristo ambao walikuwa marafiki zake. Alianza kuelewa kuwa asingeamini sauti zote alizokuwa akisikia. Mara nyingine Mungu alikuwa akizungumza naye, lakini mara kadhaa roho chafu zilikuwa zikijaribu kumpeleka katika uelekeo usio sahihi. Alijifunza kujaribu mawazo yake kwa ukweli thabithi. Aligundua kuwa uhusiano halisi na Kristo ulikuwa unaridhisha zaidi ya uzoefu aliowahi kuwa nao.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Zaburi 19 tena. Kila mwanafunzi anapaswa kuandika kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha maandiko kwa mfuasi wa New Age. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa kila somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 14
# Dini za Asili

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Miri alikuwa mtoto mdogo katika Kijiji huko Papua New Guinea. Alikuwa na wanasesere wachache wa kuchezea lakini kuna nyakati alichezea fuvu la babu yake. Fuvu lilikuwa limetunzwa ndani ya nyumba kama njia ya kuwaheshimu mababu na pia ili kuzifukuza roho mbaya.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Zaburi 147 pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha andiko kinasema nini kuhusiana na Mungu kuhusika katika uumbaji? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Dini za Asili

Dini ya asili ni mfumo wa Imani ya kidini au mtazamo dunia ambao ni halisi katika tamaduni za asili, na ni msingi wa vitendo vya kidini katika jamii nyingi za asili. Imani nyingi na matendo ya dini za asili yanaweza pia kupatikana miongozi mwa waabudu wa dini nyine kubwa ulimwenguni ikiwemo Uhindu, Ubudha, Uvoodoo, na Uromani katoliki. Watu wengi katika dini ya New Age wanajifunza dini za asili ili kupata njia za kuingiliana na ulimwengu wa roho.

> "Mungu hakuumbwa, ni muhimu, mmoja, asiye na mipaka, mkuu sana, wa milele, maisha yote kwa wote wanaoishi."
>
> - Thomas Oden
> *The Living God*

Dini ya Asili wakati mwingine imekuwa inaitwa kuabudu mizimu. *Kuabudu Mizimu* ni neno linalosisitiza Imani kwamba mambo ya asili yana roho. Hii inajumuisha Wanyama, miti, milima, na mito. Muabudu Mizimu anaamini kwamba ni lazima wazitambue na kuingiiliana na roho hizo ili kufanikiwa kupata chakula, kujenga nyumba, na kubakia mwenye afya.

***Waabudu Mizimu wanaamini katika roho ambazo zinakaa katika maeneo fulani fulani, lakini Mungu ana nguvu juu ya kila eneo, ona 1 Wafalme 20:28.***

Waabudu Mizimu pia wanaamini juu ya roho kwamba si lazima zivae mwili wa nyama au kukaa mahali. Wanaweza pia kuamini kwamba roho za mababu zao zinahusika katika ulimwengu na katika maisha yao.

Waabudu Mizimu wanaweza wasiite Imani zao dini. Uabudu Mizimu ni halisi kwao. Uabudu Mizimu kwa ujumla hauna Maandiko yenye mamlaka na hawana mafundisho yaliyoandikwa.

► Ni mfanano gani unaouona kati ya dini ya asili na dini zingine ambazo tumekwisha jifunza?


> "Ni kwa nguvu kuu za Mungu kwamba anafanya utoaji na miujiza kuwa nyumbani kikamilifu katika ulimwengu wa kibiblia. Mungu hawezi kutengwa na uumbaji wake."
>
> - W.T. Purkiser
> *God, Man, and Salvation*

Katika dini za Asili, wanadamu hawatofautiani na ulimwengu, bali ni sehemu yake, wakiwa hawana nafasi maalumu.

***Mungu aliweka thamani maalumu kwa wanadamu na akawajali kwa namna maalumu, ona Mathayo 10:31.***

Wale wanaoshughulika na dini za asili wana maneno, vitu, au matendo maalumu ili kuingiliana na roho. Taratibu hizi ni tofauti kutoka jamii moja hadi nyingine. Taratibu hizo zinawasaidia wao kuepuka kuzikasirisha roho, na pengine ili kupata mwitikio kutoka kwao. Mtu anaweza kubeba kitu ambacho kinaonekana kina nguvu. Mara nyingi, mwabudu mizimu hawezi kuelezea ni kwanini taratibu fulani inafanywa.

***Mungu anataka sisi kuondoa kitu chochote ambacho kinatumika kwa ajili ya kutegemea msaada kutoka kwa roho. Kama tuna vitu hivyo, hatumwamini Mungu kikamilifu, ona Matendo ya Mitume 19:19.***



Waabudu Mizimu wanaweza kuamini kwamba kuna njia za mtu kupata nguvu kutoka katika kitu au mtu mwingine. Wanaamini mtu anapaswa kuwa makini ili asiathiriwe na nguvu mbaya kutoka kwa kitu au mahali.[34]

Matendo mengi yanayoitwa ushirikina yanatoka kwenye dhana ya muabudu mizimu. Ushirikinna ni dhana kwamba mtu anapaswa afuate matendo fulani kwa sababu vitu, matendo, au mahali ulani pana nguvu za kiroho. Wakristo sio washirikina, hata kama wanafahamu kwamba nguvu zisizo za kawaida ni halisi, kwa sababu wanaamini nguvu kuu ya Mungu.

► Kwa nini Biblia inatukataza sisi kutumia vitu ambavyo ni sehemu ya ushirikina?

Waabudu Mizimu wanaamini kwamba ulimwengu umejaa hatari za kiroho, na kwamba wanapaswa kuwa makini wasizikasirishe roho za asili au za mababu zao. Maisha yao yanaongozwa na hofu kila wakati. Wakati mwingine watu wanafikiri kwamba jamii za kale zina furaha na hazina mashaka hadi pale ambapo wamisionari walipokuja na kuanzisha mambo ya dini, lakini si kweli. Watu wa jamii za kale ambao hawana injili wanaishi katika utumwa wa hofu ya roho. Injili inakuja kama ujumbe wa ajabu wa ukombozi. Wanajifunza kwamba wanaweza kumtumikia Mungu ambaye anawependa na hawahitaji kuogopa roho.

[34] Picha na Bruce Warrington kutoka Unsplash, ilichukuliwa tena kutoka https://unsplash.com/photos/8Or5Z9-sH0Q.

***Biblia inatuambia mara nyingi kwamba hatupaswi kuogopa kwa sababu tunamwamini Mungu, ona Isaya 41:10.***

Watu wanaofuata dini za Asili wanaweza kuwa na wataalamu wa dini ambao wanachukuliwa kuwa wabobezi katika kushughulika na mambo ya roho. Kila utamaduni una majina kwa ajili ya wabobezi hao.

Waabudu Mizimu wanaweza kuamini juu ya Mungu mkuu aliyeumba, lakini hawamuombi kwa sababu wanafikiria kwamba haiwezekani kuhusiana Naye. Wanafikiri kwamba wanatakiwa kushughulika na roho zinazowazunguka kwa ajili ya matokeo ya Maisha yao.

> "Namwamini Roho Mtakatifu: Bwana ma mtoa uzima aliyetoka kwa Baba na Mwana."
>
> - Kanuni ya Imani ya Nikea

Jaribio la kuungana au kushirikiana na roho mara nyingi zimepelekea Waabudu Mizimu kushirikiana au kuungana na mapepo.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno **mlalo na lililokolezwa.**

## Uinjilisti

Waabudu Mizimu wengi yatari wameshamwamini Mungu mkuu, lakini hawaamini kwamba wanaweza kumfikia au kwamba ana makusudi kwa ajili yao. Injili inatuambia kwamba Mungu anawapenda na ameonesha upendo wake kwa kumtuma Yesu.

Waabudu Mizimu wengi hufikiri kwamba wamemkosea kiumbe wa kiroho: Mungu, ndugu zao ambao ni miungu, au yeyote yule. Injili inaeleza kwamba Mungu yupo tayari kusamehe dhambi zetu ili kwamba tuje na kuwa na ushirika na Yeye.

Waabudu Mizimu husihi katika hofu ya roho. Tunaweza kuwathibitishia wao kwamba wakimfahamu Mungu, wanakuwa chini ya ulinzi wake na wanaweza kushughulika na Mungu kuliko kushughulika na roho.

## Ushuhuda

Hato alikuwa chifu wa kikabila huko Papua New Guinea. Aliishi akiogopa roho na mababu. Wanakijiji mara zote walikuwa na vita baina yao. Mmisionari alikuja na kuishi katika Kijiji chake. Hato aliona namna ambavyo Mmisionari alimwamini Mungu wakati wa majanga wakati ambapo kijana wa mmisionari alikuwa katika hatari. Hato alifanya maamuzi ya kumtumikia Mungu kuliko roho.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Zaburi 147 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa muabudu mizimu. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

**Zoezi kwa Kila Somo**

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 15
# Voodoo

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Sara alitembelea duka la Voodoo ili kuuliza maswali. Mtu huyo alisema kwamba Voodoo haikinzani na Ukatoliki na kwamba mtu anaweza kuwa Mkatoliki na akafanya Voodoo pia. Alisema kwamba roho zinawasaidia watu, lakini watu wanatakiwa kuzilipa roho kwa kuziruhusu roho hizo ziwapagae au ziwavae.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Zaburi 145 pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha Maandiko kinasema nini kuhusiana na nguvu na wema wa Mungu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Voodoo

### Utangulizi kuhusu Voodoo

Voodoo inatokana na Dini za Asili za Afrika lakini Imani na matendo kutoka dini hizo yamechanganywa na mambo tofauti kutoka vyanzo vingine. Wengi wanajishughulisha na mambo siku za leo wanapendelea kutumia neno *Vodun*.

Kulingana na Voodoo, kuna Mungu, lakini watu hawawezi kumfikia kwa ajili ya masaada. Badala yake, watu wanaweza kuingiliana na roho ambazo inahusika katika ulimwengu.

> "Yesu alipaa mbinguni na kuketi mkono wa kuume wa Baba, Mungu mwenyezi, kutoka huko atakuja kuwahukumu walio hai na wafu. Katika kuja kwake watu wote watafufuliwa katika miili yao na kutoa hesabu kwa matendo yao. Na wale waliotenda mema wataingia katika uzima wa milele; na wale waliotenda maovu wataingia katika moto wa milele."
>
> - Imani ya Kiathanasi

***Biblia iantuambia kwamba Mungu yu karibu sana na kila mmoja wetu, na kwamba tunaweza kumpata, ona Matendo ya Mitume 17:27.***

► Ni dini gani nyingine zinafanya kama hivi?

Wale wanaojishughulisha na Voodoo kimsingi wanamuabudu Shetani na roho chafu. Wengi wanaweka wazi kwamba wanamtumikia.

Mara nyingi shughuli za Voodoo hazitambuliwi na watu wa nje kwa sababu mara nyingi zinatumia taratibu mbalimbali za kiibada, picha, na majina kutoka Kanisa la Romani Katoliki. Waabudu Voodoo pia wanatumia misalaba na alama nyingine za Kikristo. Takwimu za

Voodoo ni ngumu kuzipata kwa sababu wengi wanaojihusisha na Voodoo wanajihusiha pia na dini nyingine ikiwemo Ukristo.

***Ni ngumu kumtumikia Mungu na roho nyingine pia, ona 1 Wakorintho 10:20-22.***

Wakati mwingine watu wanaojiita Wakristo lakini ambao hawajaongoka kweli hawaoni mgongano uliopo kati ya Voodoo na Ukristo. Mtu anayehudhuria kanisani anaweza pia kwenda kwa mganga wa Voodoo ili apate msaada kwa tatizo fulani. Mfanyabiashara anaweza kuomba uchawi ili umsaidie kuuza bidhaa zaidi. Mzazi anaweza kwenda kutafuta msaada kwa ajili ya mtoto mgonjwa.


> "Tunapaswa kukumbuka kwamba Mungu anakaa na kufanya kazi ndani ya watoto wa nuru, kwa hiyo shetani hukaa na kufanya kazi ndani ya Watoto wa giza. Roho Mtakatifu anapokaa ndani ya nafsi ya mtu mwema, vivyo hivyo roho chafu hukaa ndani ya nafsi ya mtu mwovu. Kwa hiyo, mitume walimwita 'mungu wa dunia hii;' kutokana na nguvu isiyodhibitika aliyonayo juu ya watu wa ulimwengu."
>
> - John Wesley
> "A Caution against Bigotry"

► Ni kwa nini inawezekana muabudu Voodoo akawa pia Mkristo?

Mwabudu Voodoo huingiliana na roho kwa kutumia madhabahu, sadaka, kucheza, na sherehe za kidini. Pia wanawaomba mababu.

Roho (*loa*) zimegawanywa katika nchi tano, na familia nyingi za watu wenye majina ya ukoo yanayofanana. Roho fulani au familia ya roho fulani zinahusika na Nyanja fulani ya Maisha, kama kilimo, jeshi la ulinzi, au mapenzi. Hii inafanana na jinsi Romani Katoliki imegawanha watakatifu katika nyanja mbalimbali za Maisha.

Makuhani wa kike na wa kiume katika dini wanaongoza ibada na matukio na wanaweza kuajiriwa kufanya uchawi au kuzuia na kulinda na uchawi. Wanaweza kuwa na kundi ambalo linaongoza katika ibada mara kwa mara na kutoa huduma ya kiroho. Kuna washirikina wengine wanaitwa bokor ambao wanaweza kuwa au wasiwe makuhani, na ambao wanahusika sana na uchawi. Kwa mfano, *bokor* anaweza kuajiriwa kuleta laana juu ya mtu mwingine.[35]



*Ofisi ya Mganga wa Kienyeji*

***Mtu aliyeitwa Simoni alikuwa mchawi nwenye nguvu, lakini nguvu za Mungu zilikuwa zaidi, ona Matendo ya Mitume 8:9-13.***

Dini ya Voodoo haina utawala wala mamlaka maalumu. Kila kuhani mwanaume au mwanamke ana desturi yake. Kila mwabudu Voodoo yupo katika familia ya Voodoo.

---

[35] Picha na Stephen Gibson, imechukuliwa tena kutoka https://www.flickr.com/photos/sgc-library/52352524591, umiliki wa umma.

***Kama Mkristo, tupo katika familia ya kiroho, Pamoja na kaka na dada ambao wanashiriki uzima pamoja na sisi na kusaidiana katika mambo ya kawaida, ona Yakobo 2:15-16 na Wagalatia 6:10.***

Mara nyingi ibada za Voodoo hufanyika siku ya Ijumaa au Jumamosi usiku. Ibada ya Voodoo inajumuisha kusoma mistari kwa heshima ya roho mbalimbali ambazo zinahusiana na familia, nyimbo nyingi, na maombi. Wanaoabudu hutumia ngoma, matari, na filimbi katika ibada zao ambazo zinaweza kuchukua usiku mzima. Wakati wa ibada ya Voodoo, roho huwavaa waabudu mbalimbali, zinaongea na kutenda kupitia wao. kupagawa na roho ni lengo muhimu katika ibada ya Voodoo. Inaaminika kwamba baraka maalumu sana huja kwa familia za wale ambao wamepagawa kwa namna hii. Wakati mwingine roho hutoa ushauri au laana.

***Roho Mtakatifu hutoa maongozi kwa kanisa na anaweza kuaminiwa kwa sababu ni Mungu, ona Matendo ya Mitume 13:2, Matendo ya Mitume 15:28 na Wagalatia 3:5.***

► Kwa nini Wakristo hawapaswi kuatafuta msaada kutoka kwa maroho?

Katika sherehe maalumu za Voodoo zipo sadaka za kuku, nguruwe na kunywa na kunyunyiza damu. Kuhani wa kike anaweza kung'ata kichwa cha kuku kutoka kwa kuku. Waabuduo wanaweza kucheze wakiuzunguka moto au kucheza kuzunguka mti. Wanaimba na kuomba kwamba roho ziwapagae. Wanaweka chakula ardhini kwa ajili ya roho. Wanachora michoro ardhini ambayo inatakiwa kudhibiti nguvu. Wanatumia nyoka katika sherehe zao za kidini. Wakati mwingine huvaa mavazi meupe. Wakati mwingine hupaka rangi nyuso zao, kwa kutumia rangi mbalimbali, na hasa hasa nyeupe.

Wakati mwingine nguvu isiyo ya kawaida huoneshwa. Baadhi hudai kwamba wameponywa kwa kutumia roho hizo. Hujaribu huzikimbiza na kuziondoa roho ambazo husababisha magonjwa. Wengine huweza kung'ata mbao inayowaka moto na kushika mkaa wa moto unaowaka katika midomo yao.

Wakati mwingine mwanasesere mdogo anaweza kutumiwa ili kumuwakilisha mtu anayelaaniwa. Pini au visu vinaweza kuchomwa kwenye mwanasere. Watu wamekufa kutokana na laana, lakini wakristo wa kweli wameshuhudia kwamba laana za Voodoo hazikuweza kuwadhuru.

Katika nyumba binafsi ya anayeabudu, anaweza kuwa na madhabahu kwa ajili ya maroho na mababu. Madhabahu zinaweza kuwa na picha na sanamu ya maroho, na mambo ambayo wanayapenda kama vile maua, mishumaa, manukato, au chakula. Mishumaa yenye rangi nyeupe na birauri ya maji inaweza kuwa sadaka rahisi.

Baadhi ya wale wanaojishughulisha na Voodoo huvaa vitu ambavyo vinasadikika kuwalinda kutokana na roho chafu. Pia huwavalisha vitu hivyo Watoto wao.

Wanaamini kwamba baada ya kifo nafsi huvaa baadhi ya Nyanja za asili kama miti.

Baadhi ya wanaoabudu Voodoo wamepagawa na mapepo wakati wote. Wengine huwa katika hali ya kutokuwa na akili sawasawa, wagonvi, na hujidhuru wenyewe.

***Mtu alipagawa na mapepo huwa na hofu na akili ambayo haiko sawa, na anajidhuru yeye mwenyewe, Marko 5:2-5.***

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

**Uinjilisti**

Waoabudu Voodoo hawana mahusiano na Mungu na hawana uhakika wa wokovu. Inamaana kwamba wanauhitaji wa kiroho ambao unaweza kufikiwa kwa Injili. Mkristo anaweza kushirikisha injili na ushuhuda wake wa wokovu na inamaanisha nini kwake kuishi katika mahusiano na Mungu.

Waoabudu Voodoo wanaishi katika hofu. Hawamtumikii Mungu ambaye anawapenda. Wanategemea yote mabaya na mema kutoka kwa maroho. Wanapaswa kumlipa kuhani wa Voodoo kwa ajili ya huduma ya kiroho anayoifanya kwa ajili yao. Katika baadhi ya nchi watu wanatumikishwa na viongozi wa Voodoo.

Mtu anayechagua kuzitumikia roho anafanya hivyo kwa sababu anafikiri anahitaji msaada na ulinzi kutoka kwao. Matokeo ni yale yale wanapofuatilia dhambi yeyote; mazuri ambayo mtu anajaribu kuyatafuta yanatoweka, na dhambi inaharibu kila kitu katika Maisha yake, yakiwemo mahusiano ya kifamilia.

Mtu anayekataa injili anataka kuendelea na dhambi na kuyatawala Maisha yake kuliko kumpa Mungu utawala. Hata hivyo, mtu aliye katika mahusiano na roho chafu hupoteza utawala juu yake mwenyewe na yuko katika utumwa.

Injili ni ujumbe wa ukombozi kutoka nguvu za giza. Ni toleo la msamaha. Ni toleo la uhusiano na Mungu ambaye anatupenda na anatujali sisi.

**Ushuhuda**

Jacques alikuwa mganga wa Voodoo huko Haiti. Aliwaua watu wengi kwa laana. Aliishi na wake kadhaa. Siku moja mmisionari alimwambia kwamba siku moja roho anazozitumikia zitakuja kumuharibu. Baadae Jacques alimuomba mmisionari aje na kumuombea. Jacques alitubu na akaharibu vifaa vyake vyote vya Voodoo.

**Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2**

► Sasa soma Zaburi 145 tena. Kila mwanafunzi anatakiwa kuandika kifungu cha maneno akielezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa wafuasi wa Voodoo. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 16
# Kuelewa Usabato

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza


Lydia alishangaa kuona watu wengi mtaani wanaenda kanisani siku ya Jumamosi. Aliwauliza majirani zake kuhusiana na hili, na wakamwambia kwamba Jumamosi ndio siku sahihi ya kuabudu. Walimuelezea kwamba Jumamosi hawafanyi biashara au hawanunui au hawafanyi yale ya kujifurahisha sana. Lydia alifikiri kwamba lazima walikuwa na dini tofauti na makanisa mengine, lakini walionekana kuamini mambo yale yale kuhusu Mung una wokovu.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma 1 Timotheo 1 kwa pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha maandiko kinasema nini kuhusiana na kufundisha mafundisho? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Usabato

### Chanzo cha Usabato


*William Miller*

Mnamo miaka ya 1830, William Miller,[36] muhubiri wa Kibaptisti, alianza kuhubiri kwamba Yesu angerudi upesi. Wafuasi wake waliitwa Wamiller kwa miaka mingi. Katika mwaka 1844, Wamiller walitabiri kurudi kwa Kristo mnamo Octoba 22, 1844. Maelfu ya watu walishawishika. Wengi wa Wamiller waliacha harakati baada ya Yesu kutotokea. Hiram Edson alidai kupokea maono kwamba tarehe hiyo Yesu alianza huduma mpya katika madhabahu ya mbinguni. Wale waliobakia na harakati waliitwa kanisa la Sabato.

Kuna makanisa mengine yanayosisitiza kwamba Jumamosi ndio siku sahihi ya ibada ya Kikristo. Kuna wengine pia kabla ya taasisi hii ambayo ilifundisha fundisho hilo, lakini Wasabato ndilo kundi kubwa Zaidi na lenye ushawishi.

[36] Picha: "William Miller", by J. H. Bufford Lithography Company, ilitafutwa tena kutoka kwa National Portrait Gallery, Smithsonian Institution https://npg.si.edu/object/npg_NPG.80.107.

**Ushawishi wa Sasa**

Katika Desemba 2020, Wasabato walidai kuwa na zaidi ya makanisa 92,000 na Zaidi ya washirika milioni 21. Walifanya kazi katika nchi 212 na kuhudumu katika lugha 535. Walikuwa na hospitali 229 na shule 9,400.[37]

**Mafundisho ya Wasabato**

Wasabato wanaamini katika mafundisho ya masingi kuhusu Mungu kama vile Utatu, Uungu wa Yesu Kristo, na Roho Mtakatifu. Pia wanaamini katika mamlaka ya mwisho ya Biblia, na Wokovu kwa njia ya Imani.

Wasabato wanasema wanaamini kwamba mtu haokolewi kwa matendo mema, lakini kwamba Wakristo wa kweli wataishi katika maisha ya utii kwa Mungu baada ya kuokolewa. Wanaamini kwamba sheria ya Mungu inawaonesha Wakristo namna ya kuishi, na kwamba Wakristo wanapaswa kuishi katika ushindi dhidi ya dhambi. Wanaamini kwamba mtu atapoteza wokovu wake endapo hataendelea kuishi kwa ajili ya Mungu.

***Wasabato wako sawa kwamba dhambi huvunja uhusiano wetu na Mungu. Yesu alisema kwamba tunabakia katika mahusiano ya upendo Pamoja naye kwa kushika amri zake, ona Yohana 15:10.***

Taasisi kuu ya Wasabato hawaamini katika wokovu kwa matendo. Hata hivyo, kuna makundi binafsi ya Wasabato ambao wamesisitiza sheria sana kiasi kwamba wanasema kwamba sheria ndio njia ya wokovu. Endapo mtu anatarajia kukubaliwa na Mungu kwa sababu ya matendo yake, haweki Imani yake katika neema iliyotolewa na Kristo (Waefeso 2:8-9).

► Nini ni mtazamo sahihi wa matendo? Ni kwa namna gani tunaelezea kwamba tunaokolewa kwa neema hata kama ni muhimu kuishi katika utii kwa Mungu?

Wasabato wanaamini kwamba mwanadamu hana asili ya kutokufa. Wakati wa kufa wanadamu huenda katika hali ya kutokuwa na ufahamu hadi watakapofufuliwa. Wakati wa ufufuo, wale waliokolewa watapokea uzima wa milele. Wale ambao hajaokolewa watafufuliwa kwa ajili ya hukumu na kisha kuharibiwa katika ziwa la moto. Wanaamini kwamba Shetani na mapepo wengine pia wataharibiwa kabisa. Hakuna hukumu ya milele.

***Yesu alisema kutakuwa na hukumu ya mwisho, ona Mathayo 25:46, Ufunuo 20:10, 15.***

Wasabato wanaamini kwamba Wakristo wanatakiwa kufuata na kutii baadhi ya sheria za vyakula za Agano la Kale. Wanaamini kwamba sheria za vyakula zilikuwa ni kwa ajili ya afya. Wanaamini kwamba Wasabato huishi Maisha marefu kuliko watu wengine.

---

[37] "Seventh-Day Adventist World Church Statistics 2021." Seventh-day Adventist Church, Februari 14, 2022. https://www.adventist.org/statistics/, ilitafutwa Aprili 11, 2023.

***Nyama zote zinaruhusiwa kwa Wakristo, kulingana na 1 Timotheo 4:4.***

Wasabato hujulikana sana kwa ajili ya fundisho lao la Sabato. Wanaamini kwamba Jumamosi, siku ya saba ya wiki, ndio siku sahihi kwa ajili ya Wakristo kupumzika na kuabudu. Wanaamini kwamba makanisa yanayoabudu siku ya Jumapili yanafuata mila za kipagani.

### Mtazamo wao Kuhusu Makanisa Mengine

Wasabato wanaamini kwamba wao ni "masalia," waaminifu wale wanaoshika sheria za Mungu katika ulimwengu huu wenye Ukristo usio thabiti. Wanaamini kwamba Babeli katika unabii unarejelea taasisi za kikristo zilizokengeuka na ushirika wao na mifumo ya ulimwengu.

Wanaamini kwamba wapo Wakristo wanaoshika sheria za Mungu katika madhehebu mengine ya Kkiristo kulingana na uelewa wao, lakini hawaelewi matakwa yote anayohitaji. Katika siku za mwisho kabla ya kuja Bwana, kila mmoja atapitia ghasia na atatakiwa kupokea mwanga na kutembea katika huo au kuharibiwa katika hukumu ya Mungu. Wanaoabudu Jumapili ambao hawatakubali ukweli hatimaye watapokea "chapa ya huyo mnyama."

Wasabato wanatambua kwamba watu mbalimbali katika historia ya kanisa walikuwa Wakristo wa kweli na walitumiwa na Mungu kama viongozi wa Uamsho. Wanasoma pia na kunukuu kutoka kwa wanatheolojia na wasomi wa Biblia ambao sio Wasabato.

► Ni kwa namna gani utaelezea mtazamo wa Wasabato kwa makanisa mengine?

### Umuhimu wa Unabii

Wasabato wanaamini kwamba unabii ni kipawa kwa ajili ya kanisa, na unahitajika kwa ajili ya maongozi. Nabii muhimu sana alikwa Ellen White. Alianza kutabiri mnamo mwaka 1844. Aliandika Zaidi ya maono 2,000. Maono yake na maandishi mengine yanatengeneza vitabu 80. Wasabato wanawatia moyo washirika wake kusoma maandiko yake mara kwa mara.

Wasabato wanaamini kwamba Biblia ndio mamlaka ya mwisho, na kwamba unabii wote lazima upimwe na Maandiko. Ellen White mwenyewe alisema vitabu vyake vinavyoitwa *Shuhuda* havitahitajika endapo watu hawatafuata maandiko kwa ukaribu vya kutosha. Alisema kwamba maandishi yake hayajakusudiwa kufunua chochote ambacho hakioneshwi katika Biblia.[38]

> "[Msimamo mkali uliopitiliza] kwa ujumla unaweza kufafanuliwa kama: uwehu/uchizi wa kidini unaoinuka kutoka kwa ushawishi potofu au hamasa toka kwa Mungu; angalau, inatokana na kutarajia au kutumaini kitu kutoka kwa Mungu ambacho haukupaswa kukitarajia kutoka kwake."
>
> - Imechukuliwa kutoka John Wesley "The Nature of Enthusiasm"

[38] Ellen White, *Testimonies*, Volume 5, 664-665

Wasabato bado wanachapisha na kugawa vitabu vya Ellen White kama maelezeo sahihi ya mafundisho wao. Wanamnukuu mara kwa mara katika machapisho yao. Hawadai kwamba maandishi yake ni mamlaka ya mwisho ukilinganisha na Biblia.

Maandishi mengi ya Ellen White yanaelezea mawazo ambayo hayapo katika Biblia, na yanatoa mafafanuzi ya maandiko ambayo yanategemea mafunuo mapya kuliko tafsiri ya kawaida. Kuna hatari kwamba Wasabato wanatoa mamlaka ya juu sana kwa maandishi kuliko Biblia, na hawaiachi Biblia kuwa na mamlaka ya mwisho.

► Yapi ni matumizi sahihi ya maandishi ya wachungaji na waalimu?

Mkazo wa Wasabato ni juu ya unabii unaonekana katika jina la kanisa lao, ambalo linarejelea ujio wa Bwana. Wanasisitiza tafsiri ya kina ya unabii wa siku za mwisho wa Kibiblia, vikiwemo vifungu vingi vya maandiko vilivyojificha. Wasabato wanasisitiza jukumu la maono na miujiza katika huduma ya sasa.

**Suala la Siku ya Saba**

Wasabato huanza Sabato yao Ijumaa wakati wa jua kuzama na inaishia Jumamosi wakati wa jua kuzama, kama Wayahudi wanavyofanya.

Wasabato wanaamini kwamba kuabudu Jumapili badala ya Jumamosi ni chapa ya huyo mnyama inayoelezewa katika kitabu cha Ufunuo.

***Chapa ya huyo mnyama katika kitabu cha Ufunuo haionekani kumaanisha chochote kama kuabudu katika siku fulani mahususi, ona Ufunuo 13:16-17.***

Wanaamini muda utakuja ambapo ulimwengu utadai kuabudu Jumapili na utajaribu kuwatesa wale watakao kuwa waaminifu katika kutunza Jumamosi kama Sabato. Wanaamini kwamba sasa hivi kuna wakristo wa kweli katika makanisa yanayoabudu Jumapili, lakini katika wakati fulani mbeleni watabadilika na kwenda kwenye kweli ya Sabato ya Jumamosi au kupoteza nafsi zao kwa kukataa ukweli. Wanaamini kwamba ghasia itakapokuja Wakristo wote wa Kweli watakuwa waaminifu kwa Sabato ya Jumamosi hata kama itamaanisha kifo, na kila mmoja ambaye anashika Jumapili kama siku ya Bwana si Mkristo.

Hakuna kitu chochote katika kitabu cha Ufunuo kinachoonesha kwamba ni suala kuu. Badala yake, suala kuu ni kuabudu mtu ambaye si Mungu.

Zingatia kinachomaanishwa na Imani ya Wasabato. Vipi kama wapo sawa, karibu makanisa yote ya Kikristo yamekuwa si sahihi tangu karne ya kwanza. Hakuna hata mmoja wa mamilioni ya Wakristo wa kimungu, wa kiroho waliotambua kwamba walikuwa wanafuata "chapa ya huyo mnyama," na kwa kweli Mungu hakuwahi kuwaonesha wao hili. Hili si fundisho dogo ambalo limepotea, lakini kulingana na Wasabato, katika siku za mwisho mtu atapoteza nafsi yake kama hakuwa sahihi.

Jumapili ni siku ya kuabudu kwa Wakristo wengi katika kila nchi duniani. Mamilioni ya Wakristo ulimwenguni kote hukutanika kumwabudu Mungu na kusikiliza Neno lake. Wanashuhudia upendo wake na neema na wanajikita katika kumtumikia Yeye. Mamilioni wanapata mateso makali kwa ajili ya Imani yao kwa Mungu. Ni kweli kwamba tunaamini wanafuata mafundisho ya Kishetani na kwamba siku moja watapoteza nafsi zao kama hawatashawishika kwamba Jumamosi ndio siku ya kuabudu?

► Fikiri kuhusu mifano ya kimungu ambao wamekuwa baraka katika Maisha yako. Je, inawezekana kuamini kwamba watapotea ispokuwa wamebadili akili zao kuhusiana na suala hili?

Wasabato wanadai kwamba Kuabudu Jumapili kulianza na baraza la Nikea mnamo 325 B.K. ukweli ni kwamba maamuzi ya baraza hayakutengeneza mafundisho mapya. Waliweka misingi kwa mafundisho ambayo walikuwa wanayaamini yalikuwa yametoka kwa mitume.

Wakristo walianza kuitunza siku ya Jumapili kama siku ya Bwana mapema sana kiasi kwamba hatuwezi kupata tarehe ya kuanza. *Didache* iliandikwa mwanzoni mwa karne ya pili ya kanisa lakini iliwakilisha utamaduni na mafundisho ya kanisa la karne ya kwanza. Ni ufupisho wa mafundisho ya mitume. Ilikuwa inatumiwa na makanisa kila mahali. *Didache* inasema kwamba Wakristo walikutana siku ya Bwana kwa ajili ya ushirika. Maandiko haya hayajaribu kufundisha fundisho lolote jipya, lakini yalirejea mafundisho yaliyokuwepo, ambayo ilimaanisha kwamba kitendo hiki tayari kilikuwa cha kawaida, na kwamba wakristo wengi tayari walikuwa wanalifahamu kama fundisho la mitume.

> "Katika siku ya Bwana, kusanyikeni na mmege mkate, toeni shukrani, lakini kwanza tubuni dhambi zetu ili kwamba sadaka yenu iwe safi."
>
> \- *Didache*
> (kutoka kanisa la karne ya pili)

Waraka wa Barnabas uliandikwa karibu na mwishoni mwa mwa karne ya kwanza. Yenyewe si maandiko, lakini ilitumika kama kitabu cha mafundisho ya kiroho katika makanisa. Uliita Jumapili "siku ya nane," siku ambayo Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Unasema kwamba Wakristo waliisherehekea siku ya nane.

Hatuoni popote katika Biblia ambapo inaelezea kwamba Sabato ilibadilishwa kwenda Jumapili. Badala yake tunaona agizo kwamba mtu asihukumiwe kwa sababu kushika ya Sabato (Wakolosai 2:16-17, Warumi 14:5-6). Pia tunaona kwamba Wakristo wa Agano Jipya walitakiwa kutoa sadaka siku ya Jumapili (1 Wakorintho 16:1-2), walikwenda kwa ajili ya ibada Jumapili (Matendo ya Mitume 20:7), na walikuwa wanaiita Jumapili Siku ya Bwana (Ufunuo 1:10).

Sabato ya Kiyahudi si takwa la msingi kwa Wakristo, lakini kanuni ya kupumzika ni kanuni ya uumbaji ya wakati wote. Kwa hivyo, Wakristo wanatakiwa kuepuka kazi au biashara Jumapili na badala yake wanatakiwa kupumzika na kumuabudu Mungu.

**Ufupisho wa Suala la Siku ya Sabato**

1. Hakuna chochote kinachoonesha kwenye kitabu cha Ufunuo kwamba "chapa ya huyo mnyama" inarejelea jambo la siku ipi ni siku ya kuabudu.
2. Haiwezekani kuamini kwamba Wakristo wote wa karibu nyakati zote mahali popote duniani wamekuwa si sahihi kuhusiana na fundisho ambalo linaweza kuwasababishia wao kupoteza nafsi zao.
3. Biblia inatuambia sisi tusiwahukumu wengine kuhusiana na kushika sabato.@AI
5. Wakristo wa Agano Jipya walikutana jumapili na waliiita siku ya Bwana.

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

## Uinjilisti/Kutumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

Hatupaswi kusema kwamba mtu sio Mkristo kwa sababu yeye ni Msabato. Inawezekana kwamba mtu ambaye anaamini mafundisho yote ya Kisabato kuwa ameokoka. Tatizo katika ushirika na baadhi ya Wasabato si kitu tunachokikataa bali ni kwamba wao ndio wanatukataa.

Tunakubaliana na Wasabato kwamba Maisha ya Mkristo ni katika kumtii Mungu. Hatukubaliani na makanisa ambayo yanafundisha kwamba kwa sababu tumeokolewa kwa neema si muhimu kuishi Maisha ya ushindi dhidi ya dhambi.

Baadhi ya Wasabato wanaonekana kuamini kwamba mtu huokolewa kwa matendo na si kwa neema. Baadhi wanaonekana kuamini kwamba mtu asipofuata matakwa ya Agano la Kale hajaokoka, hata kama anafuata Biblia kwa uaminifu kama anavyoielewa. Wasabato hao hawaelewi Injili ya Kimaandiko. Kwa wale Wasabato, tumia dondoo zifuatazo kutoka katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*:

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu

Unaweza kuitikia suala la Sabato kwa sehemu katika somo hili kuhusiana na "Suala la Siku ya Sabato."

Endapo Msabato kiukweli anaamini kwamba mafundisho ya Biblia yanajitosheleza kwa ajili ya wokovu pasipo mafunuo yeyote, hiyo ni vizuri. Endapo Msabato anaonekana kufikiri kwamba mafunuo mengine, kama yale ya Ellen White, ni muhimu, unapaswa umuoneshe yeye rejea ya Maandiko katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*, katika sehemu ya 1

(1) Biblia inajitosheleza kwa mafundisho.

## Ushuhuda

Benjamin alikuwa mshirika wa Usabato kwa miaka 12. Alijifunza mafundisho yao na akasoma maandiko ya Ellen White. Haja yake kubwa ilikuwa kuona ni kwa namna gani mtu anapata wokovu na kutakaswa. Alisema kwamba mafundisho ya wasabato yanasema kwamba tunaokolewa kwa kushika amri. Alisoma Wagalatia 5:4, ambayo inasema kwamba kama tunajaribu kuhesabiwa haki kwa matendo ya sheria hatuna Kristo. Alisema kwamba Wasabato pia wanaonekana kusema kwamba Injili itabadilika nyakati za mwisho, na watu ambao hawatakuwa wanashika sabato ya kweli hawawezi kuokolewa, hata kama hapo mwanzo kuna watu waaminifu waliokolewa pasipo kushika sabato. Benjamin bado anaamini kwamba ni lazima tumtii Mungu, lakini aliacha Usabato kwa sababu aliamini wana injili ya matendo.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma 1 Timotheo 1 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa mfuasi wa Usabato. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

## Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 17
# Kuelewa Romani Ukatoliki

## Kukutana kwa mara ya kwanza

Kipindi cha utoto wake, Hannah alimuomba Mungu amuongoze kwenye kanisa ambapo angejisikia kukubalika. Kama kijana mdogo alitembelea kanisa Katoliki kwa ajili ya ibada. Desturi nyingi za Romani Katoliki zilionekana ngeni kwake. Alipenda ukweli kuwa walifanya desturi sawa za kuabudu ulimwenguni kote. Alianza kuhisi kuwa ni muujiza wa ajabu kuwa ibada inakuwa mwili na damu ya Yesu kila wakati, ili kwamba watu wawe na ushirika na Yesu.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Tito 2 pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Ni nini kifungu kinasema kuhusu kuishi Kikristo? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Romani Katoliki

### Asili ya Romani Ukatoliki

Kiongozi wa ulimwengu wa Romani Ukatoliki anaitwa papa. Makao makuu ya kanisa la Romani katoliki ni Rumi.

Istilahi *Katoliki* inamaanisha "ya kulimwengu" au "kamili." kanisa la Romani Katoliki linadai kuwa kanisa kamili la Mungu na kwamba makanisa yote siyo ya kweli.

> "Kanisa ni la kitume, kwa kuwa linaendelea kuongozwa na mamlaka ya kitume inayoishi katika maandiko ya mitume, na kwamba Mamlaka hiyo imekuwa ndiyo kipimo"
>
> - William Pope
> *Compendium of Christian Theology III*

Ukatoliki unadai kuwa ndiyo kanisa la asili lililoanzishwa na Kristo. Wakatoliki wanadai kuwa papa wa kwanza alikuwa Petro, na kwamba mara zote kumekuwa na mrithi wa Petro kama papa wa kanisa la Katoliki. Wanaamini kwamba kundi lao la viongozi linaloitwa "makadinali" ni warithi wa mitume na wana mamlaka sawa na mitume wa asili.

Romani Ukatoliki ni sawa na Uothodox wa Mashariki katika imani na sherehe za kidini.

### Ushawishi

Kanisa la Romani Katoliki ni shirika moja ulimwenguni kote. Hadi 2021, kuna zaidi ya washirika bilioni 1.37 ya Katoliki. Idadi ya watu ya mataifa mengi wengi wao ni Waromani. Katika nchi hizo, Katoliki ni sehemu ya tamaduni zao. kuna mamilioni ya watu wanaojiita kuwa Wakatoliki lakini wanashiriki kwa msimu tu katika shughuli za kidini.

Kanisa  Katoliki ni tajiri na sana na lina nguvu sana kisiasa. Katika karne za mwanzo, mara nyingi kanisa lilitumia majeshi kuyalazimisha mataifa kunyenyekea kwa kanisa. Katika nchi zinazotawaliwa na Ukatoliki, watu wengi waliteswa na kuuawa kwa sababu hawakukubaliana na mafundisho ya Katoliki.

► Swali hili linatambulisha sehemu inayofuata. Umeona nini kwenye vitendo vya kidini vya Romani Ukatoliki?

**Imani za Romani Ukatoliki**

Namna ya kuabudu ya Ukatoliki ni rasmi sana. Wakatoliki wana mahekalu mengi makubwa ulimwenguni kote ambayo yanafahamika kwa usanifu mkubwa. Mahekalu yamepambwa kwa picha na sanamu za watakatifu kutoka kwenye historia. kwa kawaida makuhani wana mavazi maalumu. Shughuli za ibada zinafanywa kwa sehemu kubwa na makuhani, kwa ushiriki mdogo kutoka kwenye kusanyiko

> "Kristo aliteseka badala yetu kutimiza sharti la msingi ya utakatifu wa Mungu, ili kukiondoa kiambaza cha msamaha na upatanisho wa wakosaji. Kile ambacho utakatifu wa Mungu ulikihitaji, upendo wa Mungu ulikitoa msalabani."
>
> - Thomas Oden
> *The Word of Life*

Watu wa tamaduni nyingi walikuwa katoliki wakati wakiendelea kutunza matendo ya kidini ya dini zao za zamani. Zamani miungu ya kipagani mara nyingine ilipewa majina ya watakatifu wa Kikatoliki. Sherehe za Kikatoliki zilichanganywa na sherehe za dini ya kuabudu sanamu au dini ya asili.

Imani za kanisa Katoliki zinakubaliana na mafundisho ya msingi ya Kikristo kama vile Utatu Mtakatifu, Uungu, kufa, kuzikwa, na kufufuka kwa mwili wa Kristo, na Uungu wa Roho Mtakatifu

Kanisa Katoliki linadai kuwa kanisa lina mamlaka ya kuelezea Biblia inamaanisha nini, hata kama tafsiri ya kanisa inaonekana kuwa tofauti na kile ambacho Biblia inasema. Wakatoliki wanajumuisha pia maandiko mengine, yanayojulikana kama Apokrifa, katika Biblia yao (kama maandiko) ambayo hayajawekwa katika Biblia na makanisa mengine.

► Je ni nini mtazamo sahihi wa mamlaka ya kanisa katika uhusiano wa Biblia?

Wakatoliki wanaamini kuwa papa ni mwakilishi wa Kristo duniani. Wanaamini kuwa anapofanya maamuzi ya kiofisi kuhusu dini, hawezi kufanya makosa. Mamlaka hii inatoka katika desturi zao na siyo katika Biblia. Mapapa wengi katika kipindi kilichopita wamekuwa watu waovu, wenye hatia na hata wauaji.

Wote Uothodox wa Mashariki na Romani Ukatoliki unachagua watu wa kihistoria ili kuwatambua kama watakatifu. Watakatifu walio wengi wana nyadhifa katika kanisa sawa sana zile za miungu. Watu wanaomba kwao msaada. Watakatifu fulani wanapaswa kupendelea vipengele fulani vya maisha au katika kazi fulani, hivyo wavuvi, wakulima, na

walimu wana watakatifu maalumu, wanaoitwa watakatifu wasimamizi, ambao wanawaomba. Katika baadhi ya maeneo, watakatifu walichukua nafasi ya miungu ya kipagani. Watu wanamchukulia Mungu na hata Yesu kuwa mbali na hajihusishi nao, kwahiyo wanaomba kwa watakatifu badala yake.

***Katika Waebrania 4:16, Mungu anatukaribisha kwenda kwake kwa ujasiri katika maombi. Sisi wenyewe hatuna haki, lakini Yesu ametupa fursa ya kuingia katika uwepo wa Mungu kwa fidia, Waefeso 2:13.***

Waromani Katoliki wanashutumiwa kwa kuabudu sanamu kwa sababu wanaomba kwa watakatifu kwa kutumia picha na sanamu zao.

***Kutengeneza picha kwa ajili ya maombi na ibada ni kuabudu sanamu. Biblia inakataza kuabudu sanamu, angalia Kutoka 20:4-5 na 1 Yohana 5:21. Wakati mwenye dhambi anapotubu na kuwa katika uhusiano na Mungu anakataa sanamu, angalia 1 Wathesalonike 1:9. Kamwe Biblia haisemi kwamba Mkristo anapaswa kuomba kwa yeyote isipokuwa kwa Mungu au kutumia picha kwa ajili ya ibada.***

Vitu ambavyo vilitumika na watakatifu vinatunzwa kanisani kwa ajili ya heshima. Wakati mwingine mabaki ya mwili kama meno au mifupa vinatunzwa kanisani. Watu huja kupiga magoti na kuomba kwa watakatifu wanaowakilishwa na mifupa.

Makuhani wa Katoliki hawaruhusiwi kuoa.

Mariamu (mama wa Yesu) anaheshimiwa sana. Fundisho la **kupata mimba bila dhambi ya asili** linafundisha kuwa Mariamu alizaliwa bila asili ya dhambi na hakuwahi kutenda dhambi. Wakatoliki wengi wanaomba kwa Mariamu zaidi kuliko kwa Mungu. Wanahisi kuwa Yesu Yesu atamsikiliza Mariamu na atashawishiwa naye. Mariamu amekuwa mpatanishi kati ya mwamini na Kristo.

***Kwa mujibu wa 1 Timotheo 2:5, Yesu ndiye mpatanishi pekee kati ya Mungu na mtu. Yesu ana huruma zote, na hatuhitaji yeyote amshawishi ili atujali, angalia Yohana 11:35.***

► Je ni mtazamo upi sahihi wa Kikristo kuhusu Mariamu?

Wote Ukatoliki na Uothodox wa Mashariki unafundisha fundisho la **kubadilika kwa asili ya mkate na divai**. Hii ni imani kwamba wakati wa ushirika, mkate na divai vinabadilika kuwa mwili na

> "Mprotestanti wa kweli anaamini katika Mungu, ana ujasiri kamili katika rehema yake, anamuogopa kwa heshima ya mwanae, na anampenda kwa roho yake yote. Anamwabudu Mungu katika roho na kweli, katika yote anamshukuru; anamwitia Yeye kwa moyo vilevile kwa midomo yake, katika nyakati zote na mahali pote; analiheshimu jina lake na neno lake, na anamtumikia kwa dhati siku zote za maisha yake."
>
> "Najitenga na wanaotukana ovyo, wavunja Sabato, walevi; wanzinzi wote, waongo, wadanganyifu, wenye dhuruma, kwa ufupi, wote wanaoishi katika dhambi ya wazi. Hawa siyo Waprotestanti; siyo Wakristo kabisa."
>
> - John Wesley
> " Barua kwa Romani Katoliki"

damu halisi ya Yesu. Kwahiyo, waumini wanaweza kuvipokea kwa ajili ya wokovu. Kwahiyo wanaamini kuwa mkate na divai ni vitakatifu.

Waromani Katoliki wanaamini kwamba wokovu hautegemei tu upatanisho wa Kristo bali kwa kuwa sehemu ya kanisa Katoliki kupokea ushirika, na kutenda matendo mema.

Wakatoliki hawahubiri ujumbe wa injili kuwa mwenye dhambi anaweza kutubu dhambi zake, kuweka imani yake kwa Kristo, na kupokea uhakika wa wokovu. Badala yake, ni lazima mtu afuate kwa uaminifu maelekezo ya kuhani na tumaini la wokovu.

Wakatoliki wengi wanaendelea kuishi katika dhambi ya wazi. Wanatarajia kuwa wataendelea kubaki Wakatoliki mpaka kufa, kisha wanakaa toharani, kisha wanakwenda mbinguni.

***Biblia Inasema kwamba ushahidi wa mtu kuwa ni Mkristo ni kuwa anaishi maisha matakatifu, angalia* 1 Yohana *3:7-8.***

**Toharani na Hati ya Msamaha**

Waromani Katoliki wanaami kuwa baada ya kifo mtu anapaswa kutumikia adhabu ya dhambi kabla ya kuingia mbinguni. Hili linaitwa fundisho la toharani. Wanaamini kuwa dhambi ni lazima iwe na adhabu hata kama imesamehewa. Kwahiyo, hata Mkatoliki mwaminifu anategemea kukaa toharani kwa dhambi alizozifanya. Wenye dhambi wasiojali wanategemea kukaa toharani baada ya kifo, kisha wataruhusiwa kuingia mbinguni. Wanaamini kuwa moto wa toharani unasababisha maumivu makubwa kuliko maumivu yoyote waliowahi kuyapitia katika maisha.

***Yesu aliteseka ili tusiadhibiwe kwa ajili ya dhambi, angalia Isaya 53:5. Wakatoliki wanakataa kuwa sadaka ya Kristo ilitosha kwa sisi kusamehewa na siyo kutoadhibiwa kwa dhambi.***

Wanaamini kuwa Wakristo wanapaswa kuwaombea watu waliokufa na kutoa sadaka kanisani kwa ajili yao, hivyo Mungu atawasamehe dhambi zao mara na kuwatoa toharani.

***Hakuna mahali popote ambapo Biblia inatwambia kuwa tuwaombee wafu. Badala yake, inamaanisha kuwa hakuna kinachoweza kufanyika kwa wenye dhambi ambao wamekufa bila wokovu, angalia Luka 16:23-26.***

Wakatoliki wanaamini kuwa kanisa lina malimbikizi ya haki za ziada kutoka kwa Kristo na watakatifu. Papa anaweza kuwapa watu haki hii kwa kuwasaidia kupata msamaha. Haki hii wanaweza kupewa walio hai au waliokufa ambao wako toharani.

***Wazo kuwa haki kutoka kwa watakatifu inaongezeka kwenye haki kutoka kwa Kristo kuwasaidia watenda dhambi ni fundisho la hatari sana. Matendo ya wanadamu hayaleti haki yoyote kwa ajili ya msamaha, angalia Waefeso 2:8-9. Mwamini anasamehewa kabisa kwa msingi wa neema, na siyo kwa matendo ya mtu yeyote, angalia Warumi 4:5-8.***

► Ni kwa namna gani fundisho la toharani linaathiri mtindo wa maisha ya wale wpte wanaoliamini?

Fundisho la kipekee la Ukatoliki halitegemei andiko. Fundisho lao limejikita hasa kwenye desturi za kanisa

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno **mlalo na lililokolezwa.**

## Uinjilisti/Kutumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

Waromani Katoliki wanaamini msingi wa kweli za Kikristo za Utatu Mtakatifu na uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu.

Kuna Wakatoliki wengi ambao wameweka imani yao katika Kristo kwa ajili ya wokovu, lakini ujumbe wa injili hauko wazi katika Ukatoliki. Wakatoliki wengi hawajapata toba, msamaha, na uhakika wa wokovu, na hawaishi katika uhusiano na Mungu. Kwahiyo, ni muhimu kwa Mkristo kushirikisha injili. Mambo ya msingi ya Injili ambayo yanakataliwa katika Ukatoliki yanaweza kuthibitishwa kwa sehemu zifuatazo kutoka kwenye *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*:

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(10) Mungu Pekee ndiye anayepaswa Kuabudiwa.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani.

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

Kwa sababu Waromani Katoliki wameongeza tamaduni ambazo wanazichukulia kuwa za muhimu katika Ukristo, Mkristo anapaswa kuwaonesha maandiko yaliyonukuliwa katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* katika sehemu

(1) Biblia inajitosheleza kwa mafundisho.

## Ushuhuda

Bartholomayo alifanyika kuwa kuhani wa Romani Katoliki baada ya miaka kadhaa ya kusoma. Alitumikia kama kuhani wa parishi katika California na baadaye alitumikia kama padre wa jeshi la maji. Mama yake alikuja kuwa Mkristo wa kiinjilisti. Aliona badiliko la ajabu kwake na alikuwa na mzungumzo mengi pamoja naye kuhusu kubadilishwa kwake. Alimsihi kutegemea Biblia kama mamlaka ya mwisho ya imani yake. Alianza kugundua kuwa mafundisho mengi ya muhimu ya Ukatoliki yako tofauti na Biblia. Aliondoka katika kanisa la Romani Katoliki. Hatimaye alielewa kuwa wokovu unatokana na kazi ya Kristo na siyo kwa kazi zetu au kwa sakramenti za kanisa.

### Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma tena Tito 2. Kila mwanafunzi anapaswa kuandika kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe ambao kifungu hiki kinao kwa ajili ya Romani Katoliki. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

### Zoezi kwa kila somo

Kumbuka kutafuta nafasi ya kufikisha Injili kwa mtu kutoka kundi hili la kidini. Jiandae kuwashiriksha wanadarasa wako kuhusu mazungumzo ambayo mmekuwa nayo. Andika ripoti yako yenye kurasa 2 zilizoandikwa na uikusanye kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 18
# Kuelewa Uorthodox wa Mashariki

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

Kwa Kadiri Jonathan alipokuwa anaufahamu Uorthodoxy wa Mashariki, alivutiwa na namna ambavyo wamekuwa wakivumilia mateso kutoka kwa Waislamu na Wakomunisti katika nchi nyingi. Mashujaa wao sio wachungaji wa makanisa makubwa au viongozi wa muziki. Mashujaa wao ni wafia Imani. Jonathan alifikiri kwamba endapo mateso yanatakuwa makubwa kila mahali, waamini wa Uorthodoxy wa Mashariki ndio watakakao vumilia.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma 1 Wathesalonike 1 kwa Pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Nini kilitokea wakati watu hawa walipokuwa Wakristo? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Uorthodoxy wa Mashariki

### Utangulizi kwa Uorthodoxy wa Mashariki

Neno *Orthodox* linatokana na neno la Kiyunani linalomaanisha "ibada sahihi." Kanisa la Orthodoxy wa Mashariki wanaamini kwamba ndilo kanisa la kweli wakiwa na mafundisho na matendo ambayo yanatoa mwanga wa kumuabudu Mungu kwa usahihi.

Uorthodoxy wa Mashariki na Roman Catholicism uligawanyika rasmi mwaka 1054 B.K. kila moja likiadai kwamba ndilo kanisa sahihi la Mungu duniani lilianzishwa na Yesu Kristo na Mitume. Kila moja likidai kuwa ndilo kanisa sahihi duniani na lenye mafundisho sahihi, yenye msingi katika tamaduni mwanzo za Kikristo. Wanaamini mafundisho mengi yanayofanana. Ibada zao zitaonekana zinafanana kwa mtu ambaye hawafahamu wote.

Uorthodoxy wa Mashariki una taasisi 15 zinazojiongoza. Zimegawanywa kijiografia. Katika baadhi ya nchi kanisa limetumia jina la nchi kutengeneza jina la kanisa kama vile Kanisa la Kiorthodox la Urusi au Kanisa la Kiorthodox la Serbian. Mengine kati ya 15 yanajumuisha Kanisa la Kiorthodox la Ugiriki, Kanisa la Kiorthodox la Antiokia, Kanisa la Kiorthodox la Romania, na Kanisa la Cyprus.

Kila taasisi ya Kanisa inaongozwa na Patriaki au Askofu mkuu. Patriaki wa Kostantinopo anachukuliwa kuwa kiongozi mkuu wa viongozi 15. Mji wa kale wa Kostantinopo ni Istanbul ya sasa, Uturuki. Patriaki wa Kostantinopo hana mamlaka juu ya makanisa mengine, lakini wote wanamheshimu yeye kama wa juu sana.

Idadi inayokadiriwa ya waamini wa Uorthodoxy wa Mashariki ni kati ya Milioni 225 hadi Milioni 300. Taasisi ya pili ya Kikristo kwa Ukubwa duniani, baada ya Uromani Katoliki.

Katika nchi nyingi za Mashariki mwa Ulaya, watu wengi wanajichukulia wao kuwa ni wa Uorthodoxy wa Mashariki. Na kuna idadi kubwa ya waamini wa Uorthodoxy wa Mashariki katika nchi mbalimbali za Mashariki ya Kati.

► Ni makanisa gani ya Uorthodoxy wa Mashariki unayafahamu?

**Imani za Uorthodoxy wa Mashariki**

Makanisa ya Uorthodoxy wa Mashariki yanaamini mafundisho ya msingi ya Ukristo kuhusiana na Mungu, kama vile Utatu na uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu.

> "Sasa kama kanisa la Yesu Kristo limejengwa juu ya misingi ya Mitume na manabii, Yesu Kristo akiwa jiwe kuu la pembeni, matakwa ya mafundisho ya kanisa la Kikristo lazima yatoke katika maandiko matakatifu."
>
> \- Adam Clarke
> *Christian Theology*

Uorthodoxy wa Mashariki unategemea sana tamaduni za kanisa. Ili kuthibitisha fundisho, viongozi wao watanukuu kwa viongozi wa awali kuliko kunukuu kutoka katika Biblia. Wanafundisha kwamba Biblia ni mamlaka ya mwisho kwa mafundisho yao, lakini ni lazima Biblia itafsiriwe na kanisa.

Uorthodox umetengeneza mfumo mgumu wa Imani na desturi za kidini ambazo zina msingi katika tamaduni. Kanisa linadai kwamba lina mamlaka ya kufundisha kile ambacho ni muhimu kwa ajili ya wokovu, hata kama ni zaidi ya kile kinachofundishwa katika Biblia. Wafuasi wa Uorthodoxy wa Mashariki wanaamini kwamba tamaduni zao hazikinzani na Biblia.



Muundo wa kuabudu ya makanisa Kiorthodox ni wa kisasa. Wana makanisa makubwa duniani kote ambayo yanajulikana kwa ustadi wa usanifu wa majengo. Makathedro yamepambwa kwa picha na sanamu za watakatifu kutoka katika historia. Wakuhani wanavaa kanzu maalumu. Shughuli za ibada mara nyingi zinafanywa na makuhani, kukiwa na ushiriki mdogo wa kusanyiko.[39]

Watu wa utamaduni mbalimbali wamekuwa Waorthodox wakati wanatunza desturi za kidini za dini zao za awali. Hapo awali sanamu za kipagani zilipewa majina ya watakatifu wa Kikristo. Shughuli za kiibada za kanisa zilichanganywa na shughuli za kiibada za dini za kipagani au dini za asili, au hata ushirikina.

[39] Picha na Freddy Torres kutoka Pixabay, ilitafutwa tena https://pixabay.com/photos/architecture-church-kiev-religion-2166264/.

Wafuasi wengi wa Uorthodox wanamchukulia Mungu, na hata Yesu, kwamba yuko mbali na hajihusishi kuhusu wao, kwa hiyo badala yake wanawaomba watakatifu.

***Roho Mtakatifu hutusaidia kuomba kwa namna ambayo inakubalika na Mungu, ona Warumi 8:26-27. Tunapaswa kuwa na ujasiri kwamba Mungu husikia na kujibu maombi yetu. Mtu anayeomba anapaswa kuwa na ujasiri kwamba Mungu anajibu maombi, au kwamba mtu huyo hana Imani ambayo inampendeza Mungu, ona Waebrania 11:6.***

Picha na sanamu za watakatifu zinatolewa na kanisani ili kwamba watu waziombe. Vitu vilivyotumiwa na watakatifu vimetunzwa katika kanisa kwa ajili ya heshima. Wakati mwingine mabaki ya miili kama vile meno au mifupa yametunzwa kanisani. Watu huja na kupiga magoti na kuwaomba watakatifu wanaowakiliswa na mifupa.

► Ibada ya sanamu ni nini? Je, baadhi ya desturi za Uorthodoxy wa Mashariki ni ibada ya sanamu?

Mariamu uheshimiwa sana katika Uorthodoxy wa Mashariki. Wafuasi wengi wa Uorthodox wanamuomba Mariamu sana kuliko Mungu. Wanahisi kwamba Yesu atamsikiliza Mariamu na kushawishiwa na yeye. Mariamu amekuwa mpatanishi kati ya anayeabudu na Kristo. Tofauti na Ukatoliki, Uorthodoxy wa Mashariki hauamini kwamba Mariamu alizaliwa na asili ya mwanadamu ambayo ni tofauti na wengine wote na kila wakati yuko mbali za dhambi.

***Kumuomba Yesu ni alama ya Ukristo kila mahali, ona 1 Wakorintho 1:2. Wakristo pia humuomba Mungu baba, ona 1 Petro 1:17. Biblia pia huzungumza kuhusu mawasiliano na Roho Mtakatifu, ona 2 Wakorintho 13:14. Biblia kamwe haijawahi kutuambia tuombe kwa Mariamu au mtu mwingine yeyote ispokuwa Mungu.***

Yote Ukatoliki na Uorthodoxy wa Mashariki unafundisha **kubadilika kwa asili ya mkate na divai**, Imani kwamba wakati wa ushirika wa meza ya Bwana, mkate na divai vinabadilishwa na kuwa mwili na damu halisi ya Yesu, ili kwamba anayeabudu aweze kuvipokea kwa ajili ya wokovu.

***Wakati Yesu anawaonesha wanafunzi wake namna ya kufanya ushirika mtakatifu, bado alikuwa hai na alikuwepo, ona 1 Wakorintho 11:23-25. Kwa hivyo, aliposema, "Huu ndio mwili wangu" alimaanisha mkate ulikuwa alama ya mwili wake. Leo, ushirika wa meza ya Bwana unapaswa kuchukuliwa kama vile vile kama Yesu aliposema.***

Tofauti na Uromani Katoliki, wale walio katika kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki hawaamini juu ya toharani. Pia hawaamini juu ya watu ambao wana mamlaka ya Kristo juu ya kanisa lote ulimwenguni. Wanamkataa papa wa Romani Katoliki na hawana kiongozi wao wenyewe ambaye ana mamlaka kama hayo.

Mkuhani wa Uorthodox wanaruhusiwa kuoa, lakini yule tu ambaye hajaoa ndio anaruhusiwa kuwa askofu.

Uorthodoxy wa Mashariki unafundisha mafundisho ya ***theosis*** kama mchakato wa wokovu. Katika *theosis* mwamini anabadilishwa pole pole na kuwa kama Mungu, anakuwa na asili ile ile ya utakatifu kamilifu. Hili hukamilishwa kwa neema na kazi ya Roho Mtakatifu. Mchakato haukamiliki hadi baada ya kifo. Wale walioko katika makanisa ya Uorthodoxy wa Mashariki wanasema kwamba katika kupokea utakatifu huu kamilifu, tunakuwa miungu, lakini haimaanishi kwamba tunakuwa hatuna mipaka kama Mungu.

***Biblia inasema kwamba kila mwamini anashiriki asili ya Mungu, ona 2 Petro 1:3-4. Hatupaswi kusubiri hadi baada ya kifo ili kuwa na asili yake.***

Wanamini kwamba Kristo aliishinda dhambi kwa ajili yetu, lakini kila Mkristo anapaswa apokee nguvu ya Roho Mtakatifu ili kuelendelea katika ushindi binafsi wa dhambi na uchafu.

Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha kwamba Mkristo anahesabiwa haki katika Kristo, ambayo inamaanisha kwamba mwamini anasamehewa dhambi ambazo tayari amekwisha kuzifanya na kimsingi ni mwenye haki katika maisha anayoishi. Hii haimaanishi kwamba mtu atahesabiwa hana hatia wakati anaendelea na maisha ya dhambi, na haimaanishi kwamba endapo mtu atarejea katika maisha yake ya zamani bado amehesabiwa haki. Mwamini anategemea nguvu ya Roho Mtakatifu kuishi kwa haki kila siku. Hii ni theolojia nzuri endapo mtu atakumbuka kwamba Mungu humkubali yeye kwa sababu ya Yesu na si kwa sababu matendo yake ni mazuri.

> "Upatanisho unajumuisha dhambi zote, za asili na za kawaida, zilizopita na zijazo, kubwa au ndogo, wakati huu au milele."
>
> - Thomas Oden
> *The Word of Life*

Wafuasi wengi wa Uorthodoxy wa Mashariki wanaamini injili na uzoefu wa neema ya Mungu. Hata hivyo, kanisa kimsingi haihubiri ujumbe wa injili kwamba mwenye dhambi anapaswa atubu dhambi zake na kuweka Imani yake kwa Kristo ili kupokea uthibitisho wa haraka wa wokovu. Kwa hiyo, mamilioni ya washirika wa Uorthodox, wengi huendelea kuishi kwa wazi katika dhambi huku wakiendelea kufanya desturi za kidini. Wengi wao hawaelewi namna ya kuokoka.

► Nini ni baadhi ya mambo mazuri kuhusiana na theolojia ya Uorthodoxy wa Mashariki?

► Sasa rudi nyuma na soma kila andiko na neno ***mlalo na lililokolezwa***.

### Uinjilisti/Kutumia *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*

Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha kweli za msingi za Ukristo za Utatu na uungu wa Kristo na Roho Mtakatifu.

Kuna baadhi ya waabudu wa Kiorthodox ambao wameweka Imani yao kwa Kristo kwa ajili ya wokovu, lakini ujumbe wa injili hauko wazi katika fundisho la kanisa. Wengi wao hawajapata uzoefu wa toba, msamaha, na uthibitisho wa wokovu, na wengi wao hawaishi katika mahusiano na Mungu. Kwa hivyo, ni muhimu kwa Mkristo kushirikisha injili. Misingi

muhimu ya Injili ambayo inakataliwa na Uorthodox inaweza kuthibitisha na sehemu zifuatazo katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho*:

(9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

(10) Mungu Pekee ndiye anayepaswa Kuabudiwa.

(11) Tunapokea wokovu kwa Imani.

(12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

Kwa sababu Uorthodoxy wa Mashariki umeongeza tamaduni ambazo zinachukuliwa kuwa za muhimu kwa Ukristo, Mkristo anapaswa kuwaonesha wao maandiko yaliyonukuliwa katika *Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho* katika sehemu

(1) Biblia inajitosheleza kwa mafundisho.

**Ushuhuda**

John alilelewa katika familia ya Kiorthodox huko Romania. Babu yake na bibi yake walikuwa viongozi katika kanisa. Alibatizwa na kuoa kanisani lakini hakuudhuria ibara mara kwa mara. Makuhani hawakuongea naye kuhusiana na dhambi zake. John hakuwa na Biblia, na makuhani hawakuwahi kumwambia kusoma Biblia. Akiwa kijana alijiunga na chama cha kikomunisti. Alitumwa na Wakomunisti kutazama ibada za Kibaptisti. Alitumwa kuwauliza kwa nini wao ni Wabaptisti na sio Waorthodox. Katika ibada, alitambua hakuwahi kutubu dhambi zake. Alifanya maamuzi ya kutubu na kuwa mwamini mwaminifu wa Yesu. Alilazimishwa na familia yake na chama cha Wakomunisti kuachana na Imani yake. Alitiwa moyo kwa kutumia muda kusoma Biblia. Baada ya familia yake kuona mabadiliko latika maisha yake, wengi wao waliamini pia. John alisema kwamba utofauti mkubwa kati ya Uorthodox wa Mashariki na Ukristo wa Kiinjilisti ni kwamba Wainjilisti husisitiza kuzaliwa upya.

**Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2**

► Sasa soma 1 Wathesalonike 1 tena. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki kwa mfuasi wa Uorthodoxy wa Mashariki. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

**Usomaji wa Hiari: Kanisa la Oriental Orthodox**

Kanisa la Oriental Orthodox ni tofauti na kanisa la Uorthodox wa Mashariki.

Uoriental orthodox una taasisi makanisa sita: Koptiki, Ethiopia, Eritrea, Malankara Siria, Siriaki, na mitume la Armenian. Kila taasisi inaongozwa na Patriaki. Kila taasisi inatawaliwa kwa uhuru pasipo kuingiliwa na wengine. Patriaki wa kanisa la Koptiki ndiye papa wa makanisa yote ya Oriental Orthodox, lakini hana mamlaka juu ya wengine, ispokuwa katika kuongoza vikao vya wawakilishi kutoka taasisi sita.

Katika nchi za Armenia, Ethiopia, na Eritrea, Wakristo wa Oriental Orthodox ni kundi kubwa la kidini. Katika nchi nyingine za Kiislamu ambapo Wakristo ni asilimia ndogo ya mkusanyiko wa watu, kama vile Misri, Sudan, Siria, na Lebanoni, Wakristo wa Oriental Orthodox ni asilimia kubwa ya Wakristo. Wameteswa sana kwa karne nyingi katika nchi za Kiislamu.

Oriental Orthodoxy imekuwa tofauti na makanisa mengine ya Kikristo kwa sababu ya kutokukubaliana kimafundisho katika mwaka 451 B.K.

Walitengana kutokana na kutokukubaliana Kitheolojia juu ya asili ya Kristo. Kwa wakati huo kulikuwa na kanisa moja kuu lililowakilisha Ukristo. Kanisa lilikuwa halijagawanyika na kuwa kanisa la Kiorthodox la Mashariki na Kanisa la Romani Katoliki. Makanisa machache yalijigawa kutoka kanisa kuu wakati huu.

Baraza la Chalcedon, lilikusudiwa kuwakilisha Ukristo wote, lilifanya maamuzi kwamba ilikuwa ni sahihi kukubali kwamba Yesu alikuwa na asili mbili, asili ya uanadamu na uungu. Baadhi ya makanisa yalikataa maamuzi haya kwa sababu ilionekana kusema kwamba Yesu alikuwa watu wawili katika mmoja. Waliamini kwamba asili yake ilitokana na asili ya uanadamu na uungu, lakini ni asili moja. Waliamini wanashikilia Imani halisi ya Kikristo. Masuala mengine yaliyohusika, yakiwemo masuala ya kisiasa, lakini masuala ya Kitheolojia ndio yaliyokuwa muhimu.

Ndani ya miaka michache baada ya baraza, maaskofu ambao hawakukubaliana na maamuzi ya baraza walifukuzwa kutoka kanisani. Makanisa ya Oriental Orthodox yalitengenezwa baada ya hapo.

## Zoezi kwa Kila Somo

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Somo la 19
# Kuelewa Theolojia ya Mafanikio

## Kukutana kwa Mara ya Kwanza

James alikuwa anaangalia ibada ya kanisa katika televisheni. Kanisa lilikuwa linazungumzia kutoa kwa ajili ya mradi maalumu. Muhubiri kanisani aliomba kwa ajili ya baraka kwa yeyote ambaye atatoa fedha kwa ajili ya mradi. Muhubiri alihaidi kwamba yeyote atakayetoa atapokea kutoka kwa Mungu mara mia zaidi ya kile walichokitoa. James alifikiri kama angechangia kwa njia ya mtandao au la.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 1

► Soma Mathayo 6:25-34 kwa Pamoja kwa sauti. Kila mwanafunzi anapaswa aandike kifungu cha maneno ambacho kinafupisha kifungu hiki cha andiko. Kifungu hiki cha andiko kinafundisha nini kuhusiana na Mungu kutoa kwa ajili ya mahitaji yetu? Kila mwanafunzi anapaswa aandike orodha ya maelezo. Kama kundi, jadilini kile mlichoandika.

## Baraka za Mungu kwa Wanadamu

Mungu hubariki uumbaji wake (Mwanzo 1:22, 28). Mungu aliwaumba wanadamu wa kwanza na akawaweka katika mazingira kamilifu ili kuwapa kila kitu walivhokihitaji (Mwanzo 2:8-9). Kabla ya mwanadamu wa kwanza kufanya dhambi, kazi ilikuwa ya kupendeza, na hakukuwa na mateso ya kimwili au kuteseka au kuzeeka au kifo (Mwanzo 3:17-19). Muundo wa Mungu wa Maisha kwa ajili ya mwanadamu wakati wa uumbaji unatuonesha sisi kwamba anataka kutupatia sisi kila tunachotitaji.

Yesu alipokuwa hapa duniani, alionesha upendo wa Mungu. Kwa kuponya magonjwa na kuwalisha wenye njaa, alionesha kwamba Mungu anajali kuhusiana na mahitaji yetu ya kimwili, katika kaburi la Lazaro, Yesu alionesha huruma ya Mungu alipoomboleza Pamoja na familia (Yohana 11:35) kisha akamfufua Lazaro kutoka kwa wafu.

Mtume Yohana aliandika kwamba anatamani waamini wafanikiwe na kuwa na afya (3 Yohana 1:2).

Katika kifungu cha Maandiko ulichosoma mwanzoni mwa somo hili, Yesu alisema kwamba kama vile Mungu anavyotoa kwa ajili ya mashomoro na kuyavika maua kwa uzuri atatoa pia kwa ajili ya Watoto wake (Mathayo 6:25-34). Alisema kwamba Watoto wa Mungu hawapaswi kusumbukia mahitaji yao. Mwamini anapaswa afanye ufalme wa Mungu kuwa kipaumbele chake kikuu kuliko mahitaji yake binafsi.

► Mwanafunzi asome 1 Timotheo 6:6-10 kwa ajili ya kundi.

Mungu anataka Watoto wake waridhike badala ya kutafuta utajiri. Kifungu hiki kinatuonya tusipende fedha, kwa sababu kupenda fedha ni shina la mabaya yote. Mtume Paulo aliandika kwamba turidhike endapo mahitaji yetu ya msingi yanafikiwa. Alisema kwamba wale wanaotamani kuwa matajiri huangukia katika majaribu na tamaa mbaya. Yeye anayetafuta fedha nyingi huangukia katika huzuni nyingi.

## Dhana ya Kibiblia ya Mateso

Mateso ni matokeo ya dhambi, ingawaje mateso ya mtu hayapimwi moja kwa moja kwake kama matokeo ya dhambi yake. Mateso hayajagawanya kwa haki katika maisha haya. Tunateseka, si tu kwa sababu ya dhambi yetu wenyewe, lakini kwa sababu ya dhambi za wengine.

Mungu aliumba ulimwengu kamilifu na kamwe hakukusudia kwamba magonjwa, kuzeeka, na kifo kuwepo. Hatimaye anarejesha ulimwengu uliokamilika. Upatanisho uliofanywa na Kristo hatimaye unatoa kwa ajili ya urejesho kamilifu wa uumbaji wote.

Sio faida zote za upatanisho zinapokelewa kikamilifu kwa sasa. Mungu ana mpangilio wa vipaumbele ambavyo anavifuata. Kwa sababu mateso ni matokeo ya dhambi, dhambi lazima ishughulikiwe kwanza. Kama Mungu angeondoa mateso kwa haraka, watu wasingeona madhara ya dhambi. Mateso yanaonesha ubaya au uovu wa dhambi na hitaji ya toba.

Kwa kuwaumba wanadmu kama viumbe huru, Mungu alionesha vipaumbele vyake. Mungu anachukia dhambi, lakini huzingatia kwamba ni muhimu kwa watu kuwa huru kufanya uchaguzi. Mungu anataka watu wafanye mema kwa sababu wamechagua kufanya, si kwa sababu wanalazimishwa. Mungu anataka kuwaokoa watu kwa ushirikiano na chaguzi zao, kwa hiyo anawashawishi katika utashi wao huku akiruhusu mateso ili kuonesha matokeo ya dhambi. Kwa kadiri watu wanavyoona wema wa Mungu katika mateso duniani, wanaona kwamba wanapaswa watubu dhambi zao na kumtii Mungu.

Mungu anashughulika na tatizo la dhambi kwanza, na hilo linachukua muda kwa sababu amewapa watu uhuru wa kuchagua. Dhambi ya ulimwengu haiwezi kuondolewa hivi punde kwa sababu watu wanapaswa waamue kibinafsi. Wale wanaotubu hatimaye wataingia katika ulimwengu mpya wa Mungu, mahali ambapo hapatakuwa na mateso. Wale ambao hawako tayari kuzicha dhambi zao hawataokolewa kutoka katika mateso.

Nguvu ya Mungu haina mipaka, lakini ina utaratibu wa vipaumbele. Kuokoa watu kama wakiwa tayari, kama waamini waliotubu, lazima shughulike na dhambi kwanza kuliko mateso. Wakati mwingine Mungu anaponya, lakini uponyaji kamilifu kwa watu wote hauwezi kuhakikishwa wakati huu wa sasa. Hii ndio sababu tunaendelea kuzeeka na kuharibika kimwili. Lazima tungoje kwa Imani hadi ukombozi mkuu wa mwili wetu (Warumi 8:23).

## Misingi ya Kibiblia ya Mafanikio

► Ni kwa njia gani baadhi ambazo Mungu hutoa kwa ajili ya mahitaji ya watu wake?

Wakati mwingine Mungu hutoa kwa njia isiyo ya kawaida, ya muujiza. Kwa mfano, alidodosha chakula maalumu kutoka angani kwa ajili ya watu wa Israeli (Kutoka 16:14-15). Yesu kwa muujiza alizidisha mikate na samaki kwa ajili ya makutano katika awamu mbili (Marko 6:34-44, Marko 8:1-9). Hata hivyo, Mungu ameweka njia za kawaida la kuleta baraka kwa watu.

1. **Mungu hubariki kazi.** Kazi ilikuwa sehemu ya maisha makamilifu ambayo Mungu aliyakusudia kwa ajili ya watu (Mwanzo 2:15). Maandiko yanasema kwamba tunapata faida kutokana na kazi (Mithali 14:23). Mtu anapaswa afanye kazi ili kupata rasilimali za kushiriki na wengine (Waefeso 4:28). Biblia mara nyingi imekuwa inamkosoa mvivu (Mithali 6:9, Mithali 10:26, Mithali 20:4). Kanisa halipaswi kumsaidia mtu asiye tayari kufanya kazi (2 Wathesalonike 3:10). Mtu ambaye anaweza kufanya kazi asitegemee Mungu kukutana na mahitaji yake pasipo kufanya kazi.

2. **Mungu hubariki biashara**. Maelezeo ya Biblia ya mwanamke mwenye busara yamejumuisha maelezo ya kina kwamba anafanya biashara kwa faida (Mithali 31:16, 24). Mungu anapendezwa na biashara yenye uaminifu na anachukuia kutokuwa mwaminifu (Mithali 11:1). Mungu hapendezwi na biashara isiyo sawa kwa watu ambao wako katika mazingira magumu (Mithali 22:16, Amosi 8:4-8).

3. **Mungu hubariki mali**. Nabii Mika alisema kwamba baraka za Mungu juu ya taifa zinajumuisha mali binafsi za watu (Mika 4:4). Mara nyingi Mungu ameahidi kubariki ardhi na mashamba na wanyama wanaomilikiwa na watu wake (Kumbukumbu la Torati 28:4). Ni vizuri mtu kuendeleza mali ili kwamba zimletee faida.

4. **Mungu hubariki familia ya kanisa.** Mungu ana mipango kwa kanisa kutunza watu wake kama washirika wa familia. Waamini wanapaswa wawasaidie wale ambao wako katika familia ya Imani (Wagalatia 6:10, 1 Timotheo 5:3). Kanisa ni mojawapo ya njia ambazo Mungu hukutana na mahitaji wa waamini.

5. **Mungu hubariki kutoa kwa kujitoa**. Mtume Paulo aliliahidi kanisa kwamba Mungu anatimiliza mahitaji yao kwa sababu wametoa kwa kujitoa ili kwamba yeye aweze kuwahudumia wengine (Wafilipi 4:14-19). Yesu alisema kwamba sadaka ndogo ya mama mjane ilihesabiwa kama kubwa sana kwa sababu alitoa kwa kujitoa (Marko 12:43-44). Kila mtu katika kanisa anatakiwa kuchangia katika huduma za kanisa na kuangalia njia za kuwasaidia wengine katika familia ya kiroho.

6. **Mungu hubariki utoaji endelevu.** Mfumo wa Agano la Kale wa fungu la kumi (kikumi) na matoleo unaonesha kwamba mwamini anapaswa atoe 10% ya mapato yake *na* matoleo ya ziada. Mungu ameahidi baraka za kiuchumi kwa watu wanaotoa fungu la kumi (Malaki 3:10).

7. **Mungu hubariki kutunza wachungaji.** Mungu alikusudia wachungaji watunzwe na huduma zao (1 Wakorintho 9:14). Waamini wanapaswa kutoa ili kuwatunza wachungaji wao (Wagalatia 6:6). Mchungaji anapaswa kufanya kazi inapohitajika

(Matendo ya Mitume 20:34). Mchungaji anatakiwa kusukumwa au kuhamasishwa na upendo na si na fedha (1 Petro 5:2). Waalimu wengi wa mafundisho ya uongo wanahamaishwa na kusukumwa na fedha. (Tito 1:11, 2 Petro 2:3). Si sahihi kununua au kuuza baraka za Mungu kwa ajili ya fedha (Matendo ya Mitume 8:20).

## Waalimu wa Mafanikio ya Uongo

Biblia inatuonya juu ya wahubiri ambao wana ujumbe wa uongo ambao unavutia watu (2 Timotheo 4:1-4). Waalimu wa Mafanikio ya Uongo hushiriki tabia kadhaa zinazofanana:

1. Huwavuta waamini katika malengo ya kidunia badala ya kuwaitwa ili watubu.
2. Hawatoi mtazamo halisi wa Kikristo juu ya mateso ya wanadamu.
3. Wana mtazamo wa kiburi ambao hauheshimu makanisa mengine, wakristo wazee, na hata Mungu.
4. Wanatoa ahadi ambazo Mungu hajazitoa, hupelekea watu kuvunjika moyo na kupoteza imani.

> "Lakini yeyote atakayesema katika Roho, 'Toa fedha,' au kitu chochote kile kama hiki, usimsikilize. Bali kama akiuambia toa kwa ajili ya wengine ambao wapo katika mahitaji, asiwepo wa kumuhukumu."
>
> - *Didache*
> (kutoka kanisa la karne ya pili)

Wakati mwingine waalimu wa Mafanikio ya uongo huvuta usikivu kwa mafundisho yasiyo ya kawaida na kipaji cha kuhubiri. Hudai kuonesha miujiza na mafunuo ambayo makanisa mengine hayana. Wanataka kuheshimiwa kama watu maarufu wa kidini.

Husisitiza mafunuo mapya, na mengi ya mafundisho yao hayapatikani katika Biblia. Hudai kujifunza mafunuo haya katika mazungumzo yao na Mungu.

Hujulikana kwa mafundisho yao kuhusiana na imani, wakisisitiza kwamba kila mtu anaweza kuwa na afya na utajiri kama watajifunza namna ya kutumia Imani. Wanaahidi kwamba kila mtu anaweza kuponywa. Wanasema ni mpango wa Mungu kwa kila Mkristo kuwa tajiri.

Wanadai kwamba miujiza mingi hutokea katika huduma zao, lakini hakuna ushahidi mzuri kwamba miujiza mingi ni halisi. Wanadai kutoa mwongozo ili kwamba kila mwamini aweze kuwa tajiri, lakini ni viongozi tu ndio wanaokuwa matajiri—kutokana na utoaji wafuasi wao.

Umati mkubwa wa watu wanaowafuata watu hawa si matajiri, wala hawana uzoefu wa afya kamilifu. Badala yake, ni watu wanaoishi kwa matumaini, wanaongozwa na Habari za mafanikio ambazo hazijathibitishwa.

Makanisa mengi mapya ya mafundisho ya Mafanikio ya uongo yameanza katika nchi mbalimbali ulimwenguni kote. Baadhi yao huwaigiza waalimu wa Kimarekani katika televisheni. Baadhi yao hutumia vitabu na video kutoka kwa wahubiri wa Kimarekani wa Mafanikio ya uongo. Baadhi ya waalimu wa Mafanikio ya uongo wameanzisha makanisa

katika nchi nyingine na wamechukua matoleo kwa ajili yao badala ya kutumia fedha kubariki makusanyiko ya wenyeji.

## Theolojia ya Mafanikio ya Uongo

Waalimu wa Mafanikio ya uongo wametengeneza theolojia ya uongo ili kusaidia mawazo yao.

Waalimu wa Mafanikio ya uongo wanasema kwamba Imani ni nguvu fulani isiyo ya kinafsi na kiini cha ulimwengu. Wanaamini kwamba Imani ni nguvu ambayo watu wanaweza kutumia kama ambavyo Mungu anaitumia.

Waalimu wa Mafanikio ya uongo wanafikiri kwamba wanaweza kutumia Imani pasipo kumtegemea Mungu na pasipo kujaribu kufahamu mapenzi ya Mungu. Kinyume chake, Yesu alituambia kuomba ili mapenzi ya Baba yafanyike (Mathayo 6:10). Biblia inatuambia kwamba Imani inatuongoza kumuamini Mungu na kutafuta thawabu ambayo anatoa (Waebrania 11:6).

Waalimu wa Mafanikio ya uongo wanafundisha kwamba Mungu hamiliki dunia au haitawali. Wanafundisha kwamba Mungu alimpa mwanadamu mamlaka juu ya dunia, na mwanadamu akampatia shetani. Wanasema kwamba Mungu hawezi kufanya chochote duniani hadi watu wampatie ruhusa. Kinyume chake, Biblia inasema kwamba dunia na kila kitu ni mali ya Mungu (Zaburi 24:1). Biblia inasema kwamba Mungu ndiye mwamuzi wa dunia yote na hutenda katika dunia (1 Samweli 2:10).

Mafundisho yao kuhusiana na imani yana msingi juu ya mafundisho kuhusu Mungu ambayo ni tofauti na Ukristo wa kihistoria. Kwa mfano, wanafundisha kwamba Mungu Baba ni mtu mwenye mwili. Wanaamini kwamba watu ni nakala ya kifizikia ya Mungu. Wanaamini kwamba kwa sababu watu ni nakala za Mungu, wanapaswa kuweza kufanya kile ambacho Mungu anafanya.

> "Mojawapo ya dhambi ambazo mtu anaweza kutengeneza, na ngumu kuliko zote ambayo Mungu anaichukia sana kama kuabudu sanamu, kwa sababu kuabudu sanamu ni dharau na kutukana tabia yake.... mungu aliyezaliwa kutoka katika kivuli cha moyo ulioanguka kiuhalisia hawezi kuwa mfano wa Mungu wa Kweli. 'ndivyo ulivyofanya,' anasema Bwana kwa mtu mwovu katika Zaburi 50:21, 'ukadhani ya kuwa mimi ni kama wewe.'"
>
> - Imechukuliwa kutoka A.W. Tozer

Biblia inasema kwamba Mungu ni Roho (Yohana 4:24) na si mwanadamu (Hesabu 23:19). Yesu ni mwana pekee wa Mungu ambaye amefanikisha wokovu wetu (Yohana 3:16). Lakini waalimu wa Mafanikio ya uongo wanasema kwamba Mungu ni mwanadamu kama sisi na kwamba Yesu hana tofauti na sisi.

Kenneth Copeland alisema kuhusu Adamu,

> Adamu alikuwa nakala, alifanana kabisa na [Mungu]. Kama ungemsimamisha Adamu pembeni ya Mungu, wanafanana kabisa. Kama ungemsimamisha Yesu na Adamu upande upande, wangefanana na kusikika wanafanana kabisa.[40]
>
> Kidogo alikuwa kama Mungu. Hakuwa angalau kama Mungu. Hakuwa chini ya Mungu…..Adamu ni sawa sana na Mungu kama ambavyo ungempata, kama ambavyo ni sawa na Yesu.[41]

Kenneth Hagin alisema, "Kila mtu ambaye amezaliwa mara ya pili ni mungu aliyefanyika mwili, na Ukristo ni muujiza. Mwamini ni mungu aliyefanyika mwili kama alivyokuwa Yesu wa Nazareti"[42]

Benny Hinn alisema, "Usiniambie kwamba una Yesu. Wewe ni kila kitu kama alivyokuwa na kila kitu kama alivyo na vile atakavyokuwa."[43]

Morris Cerullo alisema, "Na tukisimama hapa, ndugu, humuangalii Morris Cerullo, umamuangalia Mungu. Unamuangalia Yesu."[44]

Mungu anasema,

> … mimi ni Mungu, wala hapana aliye kama mimi; nitangazaye mwisho tangu mwanzo, na tangu zamani za kale mambo yasiyotendeka bado; nikisema, Shauri langu litasimama, nami nitatenda mapenzi yangu yote, (Isaya 46:9-10).

Biblia inasema, "Nchi na vyote viijazavyo ni mali ya BWANA, Dunia na wote wakaao ndani yake" (Zaburi 24:1).

Lakini waalimu wa mafanikio ya Uongo wanasema kwamba Mungu kwa sasa hana mamlaka katika dunia.

Kenneth Copeland alisema,

> Yeye [Mungu] lazima awe na mwanadamu ambaye ni kama yule wa kwanza [Adamu]. Ni lazima mwanadamu. Ni lazima wawe wanadamu wote. Hawezi kuwa Mungu na kuja hapa na dhoruba pamoja na sifa na heshima ambayo ni tofauti na hali ya kawaida ya watu. Hawezi kufanya hivyo. Si kisheria.[45]

---

[40] Kenneth Copeland, "The Authority of the Believer IV" (Fort Worth, TX: Kenneth Copeland Ministries, 1987), kanda ya sauti #01-0304, upande wa 1.
[41] Kenneth Copeland, "Following the Faith of Abraham," (Fort Worth, TX: Kenneth Copeland Ministries, 1985), kanda ya sauti upande wa 1.
[42] Kenneth Hagin, "The Incarnation," *The Word of Faith* # 13, 12 (Desemba, 1980), 14.
[43] Benny Hinn, "Our Position in Christ #2 - The Word Made Flesh," (Orlando, FL: Orlando Christian Center, 1991), kanda ya sauti #A031190-2, side 2.
[44] Morris Cerullo, "The Endtime Manifestation of the Sons of God," kanda ya sauti 1.
[45] Kenneth Copeland, "The Incarnation," (Fort Worth, TX: Kenneth Copeland Ministries, 1985), kanda ya sauti #01-0402, upande wa 1.

> Hakutumia kitu chochote ambacho hakipatikani kwa mwanadamu ili kukamilisha kazi yake.[46]

Copeland pia alisema, "Yeye [Mungu] hawezi kwenda tena katika mavumbi ya ardhi na kumtengeneza mwanadamu mwingine. Hamiliki mavumbi ya ardhi tena."

Frederick Price alisema,

> Sasa hii ni Habari ya kushtua! Lakini Mungu anapaswa apatiwe ruhusa ya kutenda katika ulimwengu kwa niaba ya mwanadamu…..Ndio! Wewe ndiye unatawala! Nani ambaye kwa sasa hatawali? Mungu... Mungu alipompa Adamu utawala, hii ilimaanisha kwamba Mungu hana tena utawala. Kwa hiyo Mungu hawezi kufanya kitu chochote duniani hadi tumempatia ruhusa. Na namna tunavyomwacha au kumpatia ruhusa ni kupitia maombi.[47]

> "Ni ajabu kiasi gani kwamba watu wanaokiri Ukristo wanaweza kufikiri kwa roho zao za kidunia, ushirika wa kidunia, na Maisha yao yanayoongozwa na misemo ya kidunia, wanapata upendeleo kutoka kwa Mungu au wafike mbinguni!"
>
> \- Adam Clarke

Theolojia ya waalimu wa Mafanikio ya uongo inakinzana na Biblia na Imani ya msingi ya Ukristo iliyoanzishwa tangu mwanzo.

## Masahihisho ya Kibiblia

Paulo aliandika kwa waamini wa Korintho ili kusahihisha kutoelewa ambako kulikuwepo kuhusiana na maisha ya Kikristo (ona 1 Wakorintho 4:8-13). Wengi wao walikuwa maskini kabla hawajawa Wakristo. Walifikiri kwamba kwa sababu wamekuwa Watoto wa Mungu, na wana Imani na karama za kiroho, wanaweza kuanza kuwa matajiri na wenye vyeo/hali ya juu ulimwenguni. Paulo aliwaambia wao kwamba hata mitume walikuwa masikini na walikuwa na cheo/hali ya chini ulimwenguni. Ingawaje walikuwa na Imani kubwa na karama za kiroho, wakati mwingine walikuwa na njaa, hawakuwa na malazi, na walifanya kazi ili kujihudumia wenyewe. Imani haihakikishi utajiri.

Katika kifungu kingine, Paulo anaelezea kwamba uumbaji wote bado unateseka kwa matokeo ya laana ya dhambi (ona Warumi 8:22-23). Viumbe hivyo vyote vinateseka na kuhangaika ili kuishi. Alisema kwamba hata Wakristo bado wanateseka na wanasubiria wakati ambao miili yao itakombolewa. Ingawaje tunaokolewa kutoka dhambini, bado hatujapata uzoefu wa uponyaji kamili ambao umetolewa na upatanisho. Bado tunaumwa, tunazeeka, na tunakufa kwa sababu hatupo mbinguni bado. Wakati mwingine Mungu anaponya, lakini hatuhakikishii kwamba hatutaishi huru kutoka kwa matatizo yote ya kimwili.

[46] Copeland, "The Incarnation."
[47] Frederick Price, "Prayer: Do You Know What Prayer Is... and How to Pray?" *The Word Study Bible* (Tulsa, OK: Harrison House, 1990), 1178.

Mtume Yakobo anawakemea watu ambao wanapenda mambo ya dunia na kuomba mambo ambayo yanaridhisha matamanio yao (Yakobo 4:3). Mtume Paulo alikuwa na huzuni kuhusu Dema ambaye aliiacha huduma kwa sababu alipenda mambo ya dunia (2 Timotheo 4:10). Kwa vyovyote vile, Yakobo na Paulo wote walielewa kwamba Imani sio uhakika wa utajiri.

Waebrania 11 inanandika maisha ya mashujaa wengi wa Imani. Walikamilisha mambo makubwa kwa sababu waliamini ahadi za Mungu na walimtii Mungu. Walivumilia nyakati ngumu kwa sababu ya uaminifu wao kwa Mungu. Wengi wao hawakuwa na malazi na walikosa chakula na mavazi (Waebrania 11:37-38). Hawakuteseka na mambo haya kwa sababu hawakuwa na imani, lakini walikuwa na imani. Walikuwa tayari kupoteza kila kitu katika ulimwengu huu kwa ajili ya mahusiano yao na Mungu.

► Nini ni baadhi ya Ushahidi wa kibiblia kwamba Imani haitoi uhakika wa utajiri?

Injili ya kibiblia ni ujumbe wa matumaini wa mtu ambaye anafahamu kwamba ana hatia ya dhambi na anahitaji msamaha na amani na Mungu. Mahusiano na Mungu kwa msamaha na kukabidhi mapenzi yetu. Maisha ya Mkristo ni katika kutii, unyenyekevu, na kujikabidhi katika mapenzi ya Mungu kila siku. Mungu anatukaribisha sisi ili kuleta mahitaji yetu kwake katika maombi, lakini tunapaswa kukubali mapenzi yake katika kila hali. Mungu anahaidi kwamba kila kitu kiko chini ya udhibiti wake kwa ajili mema yetu (Warumi 8:28-29), lakini hajahaidi kuondoa mateso yote kwa haraka (Warumi 8:16-18, 1 Petro 1:6).

Sala ya Bwana ni mfano wa mtazamo wa Mkristo. Hii inakinzana na mtazamo wa waalimu wa Mafanikio ya uongo ambao hudai nguvu na heshima kwa ajili yao wenyewe. Katika maombi haya tunaona kwamba kipaumbele ni ufalme na utukufu wa Mungu, na kila kitu kinatakiwa kukabidhiwa katika mapenzi yake (ona Mathayo 6:9-13).

► Ni kwa namna gani mtazamo wa Mkristo kuhusiana na uponyaji na fedha unapaswa kuwa tofauti na mtazamo unaooneshwa na waalimu wa mafanikio ya Uongo?

## Ushuhuda

Kanisa huko Santo Domingo lilihitaji kupanua kanisa lao. Walimuomba Mungu ili awasaidie kwa ajili hiyo. Pia waliomba taasisi za kimisionari ili kusaidia. Watu wa kanisa walitoa fedha zao kwa kujitoa. Pia walitoa muda wao na kufanya kazi katika mradi wa upanuzi wa jengo. Mungu alibariki kujitoa kwao na sadaka zao, na jengo likakamilika.

## Kujifunza Andiko – Sehemu ya 2

► Sasa soma Mathayo 6:25-34 tena. Kila mwanafunzi aandike kifungu cha maneno kinachoelezea ujumbe wa kifungu hiki cha andiko kwa mfuasi wa mafanikio ya uonfo. Wanafunzi kadhaa wanaweza kushirikisha kile walichokiandika.

**Zoezi kwa Kila Somo**

Kumbuka kutafuta fursa ya kuwasilisha injili kwa mtu mmoja kutoka katika kundi hili la kidini. Jiandae kushirikisha wanadarasa wenzako kuhusiana na majadiliano mliyokuwa nayo. Andika ripoti ya kurasa 2 na uirudishe kwa kiongozi wako wa darasa.

# Kijitabu cha Mkononi cha Fundisho

Kijitabu hiki kinatoa msaada wa kibiblia kwa baadhi ya mafundisho ambayo mara nyingi yanakanwa/yanakataliwa na dini potofu. Kijitabu hiki hakijatengenezwa ili kujumuisha mafundisho yote ya Kikristo, na si mafundisho yote muhimu yameshughulikiwa hapa.

## (1) Biblia Inajitosheleza kwa Mafundisho.

### Kwa nini ni Muhimu

Baadhi ya dini zinadai kwamba kuwa Mkristo kunategemea ufunuo mpya kwa ajili ya mafundisho yao muhimu. Wanadai kwamba Biblia haijabeba vitu vyote vya msingi kwa ajili ya fundisho. Lakini Biblia inajisemea kwamba ujumbe wake unajitosheleza, kwa hivyo endapo mtu ataifuata kikamilifu, ataokoka.

### Uthibitisho wa Kimaandiko

"Lakini ni vyepesi zaidi mbingu na nchi vitoweke, kuliko itanguke nukta moja ya torati" (Luka 16:17). Alama hii iliandikwa juu ya baadhi ya herufi za kiebrania haikuwa na maana ispokuwa ilikuwa ya kupendezesha tu. Ukweli wa mstari huu ni kwamba neno la Mungu linatunza.

"Mmezaliwa mara ya pili... kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele…. Majani hukauka na ua lake huanguka; Bali Neno la Bwana hudumu hata milele. Na neno hilo ni neno lile jema lililohubiriwa kwenu" (1 Petro 1:23-25). Neno la Mungu halishindwi, na linawasilisha injili. Kwa hivyo, injili haitapatikana katika mafundisho ambayo ni nje na Maandiko, au yaliyo kinyume na maandiko.

"Mbingu na nchi zitapita; lakini maneno yangu hayatapita kamwe" (Marko 13:31). Yesu alisema kwamba maneno yake hayatapotea.

"Tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu" (2 Timotheo 3:15).

"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu... ili mtu wa Mungu awe kamili" (2 Timotheo 3:16-17). Kuna ya kutosheleza katika Biblia ili kumfanya mtu awe sawasawa na vile ambavyo Mungu anataka awe.

## (2) Kuna Mungu Mmoja tu.

### Kwa nini ni Muhimu

Kama Muumbaji na Baba, Mungu anastahili kuabudiwa. Anatuhitaji sisi tumpatie uaminifu wetu ambao haujagawanyika kwenda kwa kiumbe yeyote. Anasema kwamba Yeye ni Mungu mwenye wivu (Kutoka 34:14, Kumbukumbu la Torati 4:24, Kumbukumbu la Torati 5:9, Kumbukumbu la Torati 6:15). Mungu hukasirika wakati ambapo wengine wanapewa ibada

ambayo ni Yeye tu anastahili (Kumbukumbu la Torati 32:16, 21). Wakati dini inafundisha kwamba kuna mungu zaidi ya mmoja, au kwamba mwanadamu anaweza akawa mungu, matokeo ni kuchukua kutoka kwa Mungu baadhi ya utukufu ambao ni wake pekee.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

"Kabla yangu hakuumbwa Mungu awaye yote, wala baada yangu mimi hatakuwapo mwingine" (Isaya 43:10).

"Mimi ni wa kwanza, na mimi ni wa mwisho; zaidi yangu mimi hapana Mungu" (Isaya 44:6).

"Je! Yuko Mungu zaidi yangu mimi? Hakika hapana Mwamba; mimi sijui mwingine" (Isaya 44:8).

Ona pia Isaya 45:5, 6, 14, 21-22, na Isaya 46:9 kwa ajili ya kuthibitisha kwamba hakuna Mungu mwingine.

"Mbingu zauhubiri utukufu wa Mungu, Na anga laitangaza kazi ya mikono yake" (Zaburi 19:1). "Nikiziangalia mbingu zako, kazi ya vidole vyako, Mwezi na nyota ulizoziratibisha; Mtu ni kitu gani hata umkumbuke" (Zaburi 8:3-4). Mungu si tu Mungu wa dunia hii, lakini ni Mungu na Muumbaji wa ulimwengu.

### (3) Mungu Baba sio mwanadamu.

**Kwa nini ni Muhimu**

Sababu ya baadhi ya dini kusema kwamba Mungu ni mwanadamu ni ili kumuinua mwanadamu ili kulinganishwa na Mungu. Hii inauchukua utukufu wa Mungu. Ona mistari kuhusiana na Mungu mwenye wivu chini ya kichwa cha Habari "Kuna Mungu Mmoja tu" hapo juu.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

"Mungu si mtu, aseme uongo; Wala si mwanadamu, ajute" (Hesabu 23:19).

"Mimi ni Mungu, si mwanadamu mimi" (Hosea 11:9).

"Wakijinena kuwa wenye hekima walipumbazika; wakaubadili utukufu wa Mungu asiye na uharibifu kwa mfano wa sura ya binadamu" (Warumi 1:22-23). Kumfanya Mungu kama sanamu ni ibada ya sanamu.

"Yesu akajibu, akamwambia, Heri wewe Simoni Bar-yona; kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili, bali Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 16:17). Baba si mwili na damu, kutokana na maelezo ya Yesu.

"Mungu ni Roho" (Yohana 4:24).

## (4) Mungu hajawahi Kubadilika.

**Kwa nini ni Muhimu**

Dini potofu zina sababu tofauti za kusema kwamba Mungu anaweza kubadilika. Wanaweza kutaka kusema kwamba aliwahi kuwa mwanadamu kama sisi, ambayo inamuinua mwanadamu kuwa sawa na Mungu. Wanaweza kutaka kusema kwamba kuna ubaya na uzuri katika Mungu, au kwamba Mungu anaweza kukosea.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

“Mimi, BWANA, sina kigeugeu” (Malaki 3:6).

“Tangu milele hata milele ndiwe Mungu” (Zaburi 90:2).

“Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika, wala kivuli cha kugeuka-geuka” (Yakobo 1:17).

## (5) Yesu ni Mungu.

**Kwa nini ni Muhimu**

1. Kwa sababu Yesu ni Mungu kifo chake cha kujitoa kina thamani isiyokoma — kinatosha kwa ajili ya msamaha wa dhambi za ulimwengu.
2. Kwa sababu Yeye ni Mungu, ana nguvu za kutuokoa sisi; Yeye ni njia, kweli, na uzima.
3. Kwa sababu Yeye ni Mungu, tunapaswa tumuabudu Yeye kama tunavyomwabudu Mungu Baba.

Endapo kuna dini inayosema kwamba Yesu aliumbwa na Mungu au kwamba alikuwa mwanadamu na si Mungu, wanamchukulia ibada anayostahili. Lakini pia wanaamini injili nyingine tofauti badala ya kuweka kikamilifu imani yao kwa Yesu kwa ajili ya wokovu.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

“Mimi na Baba tu umoja” (Yohana 10:30).

“Yeye Ibrahimu asijakuwako, mimi niko” (Yohana 8:58).

“Baba ...amempa Mwana hukumu yote; ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba” (Yohana 5:22-23).

Yesu aliumba vitu vyote na vyote ni mali yake (Wakolosai 1:16).

Yesu ni mfano kamilifu wa Mungu na anaushikilia ulimwengu kwa nguvu zake (Waebrania 1:3).

Yesu ni “kwanza, na mimi ni wa mwisho” jina ambalo analisema yeye mwenyewe kwa ajili yake (Ufunuo 1:8, 13, 17, Isaya 44:6).

Rejea nyingine ambapo Yesu anaitwa Mungu: Yohana 1:1, 14, Matendo ya Mitume 20:28, Tito 2:13, Isaya 9:6, 1 Timotheo 3:16, na Yohana 14:9.

Mistari inayoonesha kwamba Yesu ana sifa za Mungu: Mathayo 18:20, Mathayo 28:20, Wafilipi 3:21, Waebrania 13:8, Yohana 2:24-25, na Mika 5:2.

Mistari inayoonesha kwamba Yesu anaabudiwa kama ambavyo Baba anaabudiwa: Waebrania 1:6, 1 Wakorintho 1:2, Wafilipi 2:9-11 (kama Isaya 45:22-23), Ufunuo 1:6, Ufunuo 5:12-13, na Yohana 17:5 (ona Isaya 42:8, Isaya 48:11).

### (6) Yesu alifufuka kimwili kutoka kwa wafu.

#### Kwa nini ni Muhimu

Tangu nyakati za kanisa, ufufuo ulikuwa sehemu muhimu ya injili. Mitume walihubiri kwamba huo ulikuwa unathibitisha kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu na mwokozi wa ulimwengu. Ufufuo wake unathibitisha kwamba injili inaokoa na kutupa sisi uzima wa milele.

#### Uthibitisho wa Kimaandiko

Yesu alitabiri kuhusiana na ufufuo wake katika mwili: "Livunjeni hekalu hili, nami katika siku tatu nitalisimamisha… yeye alinena habari za hekalu la mwili wake" (Yohana 2:19-21).

Yesu aliwaambia wanafunzi wake baada ya ufufuo wake wa mwili: "Tazameni mikono yangu na miguu yangu, ya kuwa ni mimi mwenyewe. Nishikenishikeni, mwone; kwa kuwa roho haina mwili na mifupa kama mnavyoniona mimi kuwa nayo" (Luka 24:39).

Yesu alimwambia Thomaso, "Lete hapa kidole chako; uitazame mikono yangu; ulete na mkono wako uutie ubavuni mwangu, wala usiwe asiyeamini, bali aaminiye" (Yohana 20:27).

1 Wakorintho 15:20-23 inatueleza sisi kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu namna ile ile ambayo wakristo watafufuliwa. Sura yote inaonesha umuhimu wa ufufuo wa kimwili wa Kristo kwa Wakristo. Kama Kristo hakufufuliwa, basi hatuna tumaini la kufufuliwa, na kwa hiyo injili yetu ni bure (15:17). Kama Kristo hakufufuka, basi hatutafufuliwa, na hatufai kitu na masikini pasipo tumaini na milele (15:19).

Mitume walihubiri ufufuo kama sehemu muhimu sana ya injili (Matendo ya Mitume 2:31-32, Matendo ya Mitume 3:15, Matendo ya Mitume 4:10, Matendo ya Mitume 10:40-41, Matendo ya Mitume 13:30-37, Matendo ya Mitume 17:31, na Matendo ya Mitume 26:8, 23.

### (7) Roho Mtakatifu ni Mungu.

#### Kwa nini ni Muhimu

Dini ambayo inamkana Roho Mtakatifu mara zote inakana Utatu Mtakatifu wa Mungu na uungu wa Kristo. Mtu ambaye haamini kwamba Roho Mtakatifu ni Mungu hatamuabudu na kumpa heshima na hofu anayostahili

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

Roho Mtakatifu anaitwa Mungu (Matendo ya Mitume 5:4 na 2 Wakorintho 3:17).

Roho Mtakatifu anaufahamu ambao ni Mungu tu ndio anao: Anamuelewa Mungu kikamilifu (1 Wakorintho 2:10-11) na alitabiri katika nyakati za kale (1 Petro 1:10-11, 2 Petro 1:21).

Roho Mtakatifu yupo kila mahali kwa wakati mmoja (Zaburi 139:7).

Roho Mtakatifu anaitwa Roho wa Kristo na yupo na kila mwamini (Warumi 8:9).

Roho Mtakatifu anafanya yale ambayo ni Mungu tu anaweza kufanya (Luka 24:49, Yohana 16:8-11, Waefeso 3:16, Wagalatia 5:22-23).

Unaweza kumkufuru Roho Mtakatifu (Luka 12:10).

## (8) Mungu ni Utatu.

**Kwa nini ni Muhimu**

Watu wanaokana utatu mtakatifu mara nyingi wanakana kwamba Yesu na Roho Mtakatifu ni Mungu na hawaabudu. Kosa kubwa ambalo mwanadamu anaweza kufanya ni ama kumuabudu asiye Mungu, au kushindwa kumuabudu ambaye ni Mungu. Dini inayokana kwamba Yesu si Mungu itatengeneza injili nyingine.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

Fundisho la Roho Mtakatifu linatokana na kweli tatu.

1. Biblia inasema kwamba kuna Mungu mmoja tu.
2. Biblia inazungumza kuhusu Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu kama Mungu.
3. Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wako tofauti na wanaingiliana kila mmoja na mwenzake kama nafsi.

Kwa Ushahidi wa kimaandiko kuhusu kweli mbili za kwanza, ona sehemu katika kijitabu hiki chenye kichwa "Kuna Mungu Mmoja tu," "Yesu ni Mungu," na "Roho Mtakatifu ni Mungu."

Kwa Ushahidi kwamba Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu wanaingiliana wao kwa wao na waamini kama nafsi, ona Yohana sura za 14-16. Katika Yohana 14, ona mistari ya 10-13, 16, 21, 23, 24, 26, 28, na 31. Katika Yohana 15, ona mistari ya 1-2, 9, 10, 15, 23-24, na 26. Katika Yohana 16, ona mistari ya 7, 10, 13-16, 26-28, na 32.

## (9) Wokovu ni kupitia upatanisho wa Kristo pekee.

**Kwa nini ni Muhimu**

Dini potofu zinatoa mwongozo usio sahihi kwa mtu kutafuta rehema za Mungu. Kuna njia moja tu ya kuokolewa.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

“Hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa... litupasalo sisi kuokolewa kwalo” (Matendo ya Mitume 4:12).

“Damu yake Yesu, Mwana wake, yatusafisha dhambi yote” (1 Yohana 1:7).

“Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu” (Waefeso 2:8).

“Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo” (Warumi 5:1).

“Wote waaminio… wanahesabiwa haki bure kwa neema yake, kwa njia ya ukombozi ulio katika Kristo Yesu” (Warumi 3:22, 24).

“Basi zaidi sana tukiisha kuhesabiwa haki katika damu yake, tutaokolewa na ghadhabu kwa yeye” (Warumi 5:9).

“Karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu Bwana wetu” (Warumi 6:23).

**(10) Mungu Pekee ndiye anayepaswa Kuabudiwa.**

**Kwa nini ni Muhimu**

Endapo mtu anaabudu kitu kingine tofauti na Mungu, yeye ni adui wa Mungu na yuko chini ya nguvu za Shetani. Haiwezekani kumuabudu Mungu kikamilifu na pia kuabudu kingine chochote. Ni makosa kuwaabudu viongozi wa kibinadamu, watakatifu, au Mariamu. Ni makosa kuziomba roho na kuzitii.

**Uthibitisho wa Kimaandiko**

Mungu aliwaambia watu wake kutosujudia sanamu ya kitu chochote (Kutoka 20:4-5). Kwa sababu hiyo, tunajua kwamba si sahihi kuabudu chochote.

Shetani alimjaribu Yesu ili kumsujudia, lakini Yesu alisema ya kwamba imeandikwa tunapaswa kumwabudu na kumtumikia Mungu peke yake (Mathayo 4:10). Kwa hivyo, tunajua kwamba ni dhambi kumuabudu shetani.

Mtume Paulo alisema kwamba kuabudu mashetani ni kumfanya Mungu akasirike na awe na wivu (1 Wakorintho 10:20-22). Kwa hivyo, tunajua ni dhambi kuabudu roho nyingine ambazo ziko kinyume na Mungu.

Mtume Paulo alisema kwamba watu wanadanganyika kuabudu malaika (Wakolosai 2:18). Kwa hivyo, tunajua kwamba si sahihi kuabudu malaika.

Mtume Petro alimwambia Kornelio asimwabudu kwa sababu yeye pia alikuwa mwanadamu (Matendo ya Mitume 10:25-26). Kwa hivyo, tunajua kwamba si sahihi kuabudu wanadamu.

## (11) Tunapokea wokovu kwa Imani.

### Kwa nini ni Muhimu

Kwa sababu wokovu unatolewa kikamilifu kupitia upatanisho wa Kristo, watu hawawezi kufanya chochote ili kupata wokovu, hata kidogo. Hakuna taasisi ya kiuanadamu inayoweza kuuzuia wokovu kwa mtu mwingine kwa kuweka matakwa mengine.

### Uthibitisho wa Kimaandiko

"Hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki... kwa matendo ya sheria" (Warumi 3:20).

"Mwanadamu huhesabiwa haki kwa imani pasipo matendo ya sheria" (Warumi 3:28).

"Kwa hiyo ilitoka katika imani, iwe kwa njia ya neema" (Warumi 4:16).

"Basi tukiisha kuhesabiwa haki itokayo katika imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo" (Warumi 5:1).

"Kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa" (Matendo ya Mitume 2:21).

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani... ni kipawa cha Mungu... wala si kwa matendo" (Ephesians 2:8-9).

"Tukiziungama dhambi zetu, Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu, na kutusafisha na udhalimu wote" (1 Yohana 1:9).

"Mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaaniwe" (Wagalatia 1:9).

## (12) Tunaweza kuwa na uhakika binafsi wa wokovu.

### Kwa nini ni Muhimu

Kwa sababu wokovu ni zawadi ya bure ya Mungu, inayopokewa kwa Imani, mwanadamu anaweza kufahamu kwamba ameokoka. Endapo mtu atakiri dhambi zake kwa Mungu, na kuamini ahadi za Mungu kusamehe kwa msingi wa upatanisho wa Kristo, mtu huyo anaweza kuamini kwamba ameokoka. Mungu pia anatoa Ushahidi kwa Roho wake kwamba tumeokoka. Mara nyingi dini za uongo zinawaweka watu katika hofu.

### Uthibitisho wa Kimaandiko

"Nimewaandikia ninyi mambo hayo, ili mjue ya kuwa mna uzima wa milele" (1 Yohana 5:13).

"Tuwe na ujasiri katika siku ya hukumu" (1 Yohana 4:17).

"Mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani, Baba. Roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:15-16).

## (13) Wale ambao hawajaokoka watapata hukumu ya milele.

### Kwa nini ni Muhimu

Endapo dini inakana uwepo wa hukumu ya milele, inashusha thamani ya umuhimu wa uchaguzi wa mwanadamu na pia inashusha thamani ya heshima ya sheria za Mungu. Yesu alizungumza kuhusu jehanamu mara nyingi sana, akionesha umuhimu wa fundisho hili.

### Uthibitisho wa Kimaandiko

Yesu alisema kuhusiana na mtu Tajiri ambaye alikuwa katika jehanamu baada ya kifo (Luka 16:24).

"Moshi wa maumivu yao hupanda juu hata milele na milele, wala hawana raha mchana wala usiku" (Ufunuo 14:11).

"Wakiadhibiwa katika moto wa milele" (Yuda 1:7).

"Ondokeni kwangu, mliolaaniwa, mwende katika moto wa milele" (Mathayo 25:41).

"Na hao watakwenda zao kuingia katika adhabu ya milele; bali wenye haki watakwenda katika uzima wa milele" (Mathayo 25:46).

# Maswali ya Rejea

Maswali haya ni kwa ajili ya masomo ambayo yanazungumzia makundi ya dini.

Mwanzoni mwa kipindi cha darasa, mwalimu atatoa muhtasari Pamoja na baadhi ya maswali haya. Kila swali linaweza kujibiwa kwa sentensi moja. Maswali haya yatamsaidia mwanafunzi kukumbuka zaidi dondoo za muhumu zaidi kuhusiana na kila kundi la dini.

**Somo la 3 - Umomoni**

(1) Wamomoni wanaamini nini kuhusiana na Ukristo wa Kihistoria?

(2) Lengo kuu la Wamomoni ni nini?

(3) Wamomoni wanaamini nini kuhusu Yesu kabla hajazaliwa?

(4) Wamomoni wanafikiri nini kuhusiana na makanisa mengine?

(5) Mamlaka ya juu ya Wamomoni ni nini?

**Somo la 4 – Mashahidi wa Yehova**

(1) Mashahidi wa Yehova wanafikiri nini kuhusiana na makanisa mengine?

(2) Mashahidi wa Yehova wanaamini kwamba mtu anapaswa afanye nini ili aokoke?

(3) Mashahidi wa Yehova wanaamini ninin kuhusu Roho Mtakatifu?

(4) Ni imani gani potofu inayofundishwa na Mashahidi wa Yehova kuhusiana na Yesu?

**Somo la 5 - Iglesia ni Cristo (Inglesia ni Kristo)**

(1) Maana ya jina Iglesia ni Cristo?

(2) Imani muhimu sana ya Iglesia ni Cristo?

(3) Iglesia ni Cristo wanafundisha nini kuhusu Yesu?

(4) Kulingana na Iglesia ni Cristo, ni mambo gani mawili ambayo mtu anapaswa afanye ili aokoke?

(5) Ni imani gani kubwa potofu ambayo inafanana na Iglesia ni Cristo katika mafundisho?

**Somo la 6 - Eastern Lightning (Mwangaza wa Mashariki)**

(1) Jina rasmi la Imani Potofu inayoitwa Eastern Lightning ni nini?

(2) Eastern Lightning wanafundisha nini kuhusu Yesu?

(3) Kulingana na Eastern Lightning, mtu anapaswa afanye nini ili aokokewe?

**Somo la 7 – Imani Potofu Ya Kiapokaliptiki**

(1) Ni kwa namna gani Imani Potofu za Kiapokaliptiki zinajaribu kukutana na hisia na mahitaji ya watu wa kiroho?

(2) Ni kwa namna gani Imani Potofu za Kiapokaliptiki hutumia Biblia vibaya?

(3) Ni kwa namna gani nne ambazo Imani Potofu za Kiapokaliptiki ni haribifu?

(4) Dhana kuu ya maandiko ya kinaabii ni nini kutokana na Maandiko?

**Somo la 8 - Uhindu**

(1) Ni kwa namna gani maadili ya miungu ya Uhindu inatofautiana na maadili ya Mungu mmoja wa kweli?

(2) Brahman ni nini kulingana na Uhindu?

(3) Ni nini dhana ya Uhindu kuhusu Yesu?

(4) Lengo kuu la Uhindu ni kutafuta nini?

**Somo la 9 - Ubudha**

(1) Wabudha wanaamini nini badala ya Mungu?

(2) Taja na Ufafanue Lengo kuu ka Mbudha?

(3) Wabudha wanatoa mafafanuzi gani kuhusiana na mateso katika maisha?

(4) Kwa nini Wabudha wanafanya mazoezi ya kiakili na ya kiroho?

**Somo la 10 - Utao**

(1) Watao wanamuomba nani?

(2) Miungu wakuu wawili katika Utaoni nani?

(3) Lengo la Mtao ni nini?

(4) Kulingana na Utao, Yesu ni nani?

**Somo la 11 - Uislamu**

(1) Taja mungu, nabii, na kitabu kitakatifu cha Uislamu.

(2) Kweli nne kuhusu Yesu ambazo Waislamu wanazikataa?

(3) Waislamu wanaamini nini kuhusu Biblia?

(4) Waislamu wanaamini nini kuhusu Biblia?

**Somo la 12 - Uyudaizimu**

(1) Ni maandiko gani ambayo wote Wayudaizim na Wakristo wanayo?

(2) Dhana ya wokovu kwa Uyudaizimu ikoje?

(3) Yesu alikuwa nani, kulingana na Uyudaizimu?

(4) Uyudaizimu unamsuburi Masihi wa Aina gani?

**Somo la 13 - New Age**

(1) Ni kwa namna gani wafuasi wa New Age wanaingiliana au kuwasiliana na ulimwengu wa roho?

(2) Ni kwa namna gani wafuasi wa dini ya New Age hutazama dini nyingine?

(3) Dhana ya dini New Age kuhusu Mungu ni nini?

(4) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu Yesu?

(5) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu dhambi?

(6) Wafuasi wa New Age wanaamini nini kuhusu Wokovu?

**Somo la 14 – Dini za Asili**

(1) Je, imani na desturi za dini za asili zimejikita katika dini moja mahususi? Elezea.

(2) Ni kwa jinsi gani wale wanaojishughulisha na dini za asili wanawasiliana na kuingiliana na maroho?

(3) Ushirikina ni nini?

(4) Kwa nini Wakristo sio washirikina?

(5) Kwa nini Waabudu mizimu hawanuombi Mungu?

**Somo la 15 - Voodoo**

(1) Wanaojishughulisha na Voodoo wanaabudu nini?

(2) Ni kutoka kwa dini gani dini ya Voodoo imeazima taratibu za ibada, sanamu na picha, na majina ya watakatifu?

(3) Lengo la anayeabudu katika ibada za Voodoo ni nini?

(4) Ni vitu gani hutumiwa wakati wa sherehe za ibada za Voodoo?

**Somo la 16 - Kuelewa Usabato**

(1) Dhana ya Wasabato kuhusu Mungu ni nini?

(2) Dhana ya Wasabato kuhusu wokovu ni nini?

(3) Wasabato wanaamini nini kitatokea kwa watu katika ufufuo?

(4) Wasabato wanajulikana kwa fundisho lao gani?

**Somo la 17 - Kuelewa Uromani Katoliki**

(1) Waromani Katoliki wanadai nini kutokana na jina lao?

(2) Waromani Katoliki wanaamini nini kuhusu Mungu?

(3) Kwa nini Waromani Katoliki wanashutumiwa kwa kuabudu sanamu?

(4) Dhana ya Uromani Katoliki kuhusu wokovu ni nini?

(5) Fundisho la Toharani la Uromani Katoliki ni nini?

**Somo la 18 - Kuelewa Uorthodoxy wa Mashariki**

(1) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linadai nini?

(2) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha nini kuhusu Mungu?

(3) Kanisa la Uorthodoxy wa Mashariki linafundisha nini kuhusu Biblia?

(4) Kwa nini wafuasi wa Uorthodoxy wa Mashariki wanaomba kwa watakatifu?

(5) Kulingana na mafundisho ya Uorthodoxy wa Mashariki nini kinatokea katika *theosis?*

**Somo la 19 – Kuelewa Theolojia ya Mafanikio**

(1) Taja tabia nne zinazofanana za waalimu wa mafanikio ya uongo.

(2) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, imani ni nini?

(3) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, Mungu ni nani?

(4) Kulingana na theolojia ya mafanikio ya uongo, watu ni nani?

# Vyanzo Vinavyopendekezwa

Kujifunza Zaidi kuhusiana na mada zilizojadiliwa katika andiko hili, tafadhali ona vyanzo vifuatavyo.

**Uinjilisti**

Coleman, Robert. *The Master Plan of Evangelism*. Ada: Revell, 2010.

Comfort, Ray. *Hell's Best-Kept Secret*. New Kensington: Whitaker House, 2004.

Little, Paul. *How to Give Away Your Faith*. Downers Grove: IVP Books, 2019.

**Umomoni**

Martin, Walter. *The Kingdom of the Cults: The Definitive Work on the Subject*. Bloomington: Bethany House Publishers, 2019.

Geisler, Norman and William Nix. *From God to Us Revised and Expanded: How We Got Our Bible*. Chicago: Moody Publishers, 2012.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Mashahidi wa Yehova, Iglesia ni Cristo, na Eastern Lightning vinafaa katika somo hili pia.

**Mashahidi wa Yehova**

Strobel, Lee. *The Case for Christ: A Journalist's Personal Investigation of the Evidence for Jesus*. Grand Rapids: Zondervan, 2016.

Carlson, Ron and Ed Decker. *Fast Facts on False Teachings*. Eugene: Harvest House Publishers, 2003.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Umomoni, Iglesia ni Cristo, na Eastern Lightning vinafaa katika somo hili pia.

**Iglesia ni Cristo**

Strobel, Lee. *The Case for Easter: A Journalist Investigates the Evidence for the Resurrection*. Grand Rapids: Zondervan, 2018.

McDowell, Josh and Bob Hostetler. *Beyond Belief to Convictions*. Carol Stream: Tyndale House Publishers, Inc., 2002

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Umomoni, Mashahidi wa Yehova, na Eastern Lightning vinafaa katika somo hili pia.

**Eastern Lightning**

Strobel, Lee. *The Case for the Real Jesus: A Journalist Investigates Current Attacks on the Identity of Christ*. Grand Rapids: Zondervan, 2009.

Hattaway, Paul. *China's Christian Martyrs*. Grand Rapids: Kregel Publications, 2007.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Umomoni, Mashahidi wa Yehova, na Iglesia ni Cristo vinafaa katika somo hili pia.

**Imani Potofu ya Kiapokaliptiki**

Bird, Mark, Allan Brown, Philip Brown, Ben Durr, Stephen Gibson, Daniel Glick, Richard Miles, and Larry Smith. *I Believe: Fundamentals of the Christian Faith*. Cincinnati: Revivalist Press, 2006.

Ladd, Eldon. *The Blessed Hope*. Grand Rapids: Eerdmans, 1990.

**Uhindu**

Strobel, Lee. *The Case for Faith: A Journalist Investigates the Toughest Objections to Christianity*. Grand Rapids: Zondervan, 2014.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Ubudha, Utao, Uislamu, na Uyudaizimu vinafaa katika somo hili pia.

**Ubudha**

Strobel, Lee. *The Case for a Creator: A Journalist Investigates Scientific Evidence that Points toward God*. Grand Rapids: Zondervan, 2014.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Uhindu, Utao, Uislamu, na Uyudaism vinafaa katika somo hili pia.

**Utao**

Geisler, Norman. *Christian Apologetics*. Ada: Baker Academic, 2013.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Uhindu, Ubudha, Uislamu, na Uyudaizimu vinafaa katika somo hili.

**Uislamu**

Rhodes, Ron. *Reasoning from the Scriptures with Muslims*. Eugene: Harvest House Publishers, 2002.

Vitabu vilivyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Uhindu, Ubudha, Utao, na Uyudaizimu vinafaa katika somo hili pia.

**Uyudaizimu**

McDowell, Josh. *More than a Carpenter*. Carol Stream: Tyndale Momentum, 2009.

Kaiser, Walter C. *The Messiah in the Old Testament*. Grand Rapids: Zondervan, 1995.

Vitabu vinavyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Mashahidi wa Yehova na Iglesia ni Cristo vinafaa katika somo hili pia.

Tovuti kwa ajili ya Jews for Jesus inatoa Ushahidi wa Kikristo na majibu kwa yanayopingwa hasa hasa kwa ajili ya Wayahudi, katika https://jewsforjesus.org.

Huduma nyingine ambayo inatoa andiko na taarifa ni Chosen People Ministries, katika https://www.chosenpeople.com.

**Dini ya New Age**

Geisler, Norman and Ronald M. Brooks. *When Skeptics Ask: A Handbook on Christian Evidences*. Ada: Baker Books, 1990.

Chesterton, G.K. *The Everlasting Man*. Brooklyn: Angelico Press, 2013.

Lewis, C. S. *The Abolition of Man*. San Francisco: HarperOne, 2015.

vitabu vinavyopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Mashahidi wa Yehova, Iglesia ni Cristo, na Eastern Lightning vinafaa katika somo hili pia.

**Dini za Asili**

Richardson, Don. *Peace Child*. Bloomington: Bethany House Publishers, 2005.

Richardson, Don. *Eternity in Their Hearts*. Bloomington: Bethany House Publishers, 2006.

**Voodoo**

Spurgeon, Charles and Robert Hall. *Spiritual Warfare in a Believer's Life*. Edmonds: YWAM Publishing, 1993.

Middleton, David. *Victory Over the Forces of Darkness*. Salem: Allegheny Publications, 2010.

**Usabato**

Carson, D. A. *From Sabbath to Lord's Day: A Biblical, Historical, and Theological Investigation*. Eugene: Wipf and Stock, 2000.

**Ukatoliki**

Noll, Mark. *Turning Points: Decisive Moments in the History of Christianity*. Ada: Baker Academic, 2012.

Kitabu kinachopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Uorthodoxy wa Mashariki kinafaa katika somo hili pia.

**Uorthodoxy wa Mashariki**

Gonzalez, Justo. *A History of Christian Thought, Volume 1: From the Beginnings to the Council of Chalcedon*. Nashville: Abingdon Press, 1987.

Kitabu kinachopendekezwa kwa ajili ya somo juu ya Uromani Katoliki kinafaa kwa somo hili pia.

**Theolojia ya Mafanikio ya Uongo**

Hanegraaff, Hank. *Christianity in Crisis*. Nashville: Thomas Nelson, 2012.

Gibson, Stephen. *Prosperity Prophets*. Salem: Allegheny Publications, 2006.

Sider, Ronald. *The Scandal of the Evangelical Conscience*. Ada: Baker Books, 2005.

# Rekodi ya Mazoezi

Jina la Mwanafunzi ______________________________________

Katika jedwali hapa chini, herufi za awali za majina zitaandikwa kila wakati zoezi linapokamilika. Mazoezi yote yanatakiwa kukamilishwa kikamilifu ili kupokea cheti kutoka Shepherds Global Classroom.

| | Tarehe ya Majadiliano | Kundi la Dini Lililojadiliwa | Ripoti Iliyoandikwa Imewasilishwa |
|---|---|---|---|
| 1 | | | |
| 2 | | | |
| 3 | | | |
| 4 | | | |
| 5 | | | |
| 6 | | | |
| 7 | | | |
| 8 | | | |
| 9 | | | |
| 10 | | | |

Maombi ya cheti kutoka Shepherds Global Classroom yanaweza kukamilishwa katika tovuti yetu ya www.shepherdsglobal.org. Vyeti vitahamishwa kidijitali kutoka kwa raisi wa SGC kwenda kwa wakufunzi na wawezeshaji ambao watakamilisha maombi kwa niaba ya wanafunzi wao.